

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Tatu – Tarehe 10 Aprili, 2008

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua

MASWALI KWA WAZIRI MKUU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, leo ni siku ya kwanza, yaani Alhamisi ya kwanza katika historia yetu, ambayo tunatumia Kanuni ya 38 ya maswali ya papo kwa papo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Nimepata orodha ya majina 24 na nitakwenda kwa kulingana na orodha jinsi ambavyo Katibu amefikishiwa majina. Kwa hiyo, ninaanza na Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mbunge wa Jimbo la Chwaka.

MHE. YAHYA KASSIM ISSA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. Kwa kuwa Sera ya nchi yetu ni Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi; na kwa kuwa wananchi kwa kuleta mategemeo hayo, wamewekeza kwa kuweka vitega uchumi mbalimbali hapa Dodoma; je, Serikali inatueleza nini juu ya wananchi kutokana na matumaini na kuchukua kipindi kirefu hadi kufikia zaidi ya miaka 20 kitendo hicho hakijawezekana?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, kwanza, ninaomba nishukuru sana kwamba, umeanza utaratibu huu mzuri na mimi ninafikiri utatusaidia hata sisi Serikali kuweza kupevuka haraka zaidi.

Kwa hiyo, katika kumjibu Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, ninaomba nieleze kwa kifupi kwamba, azma ya Serikali kuhamia Dodoma haijabadilishwa na uamuzi wowote, yaani bado ipo palepale. Tamko hilo ni upande mmoja, utekelezaji wenyewe wa kuhamia kwa maana ya kuona kwamba sasa tunaona zipo juhudi za kuhamia Dodoma, unategemea mambo mengi.

Kwa hiyo, moja ambalo ni dhahiri kabisa kwamba, kukua kwa miji kunategemea vilevile *aspects* nyingine za ukuaji wa uchumi. Kwa sasa utakachoona kitaleta mvuto

pengine kwa Dodoma kukua haraka zaidi ni juhudi za Serikali za kuwa na barabara ambayo inatuunganisha kati ya Dar es Salaam na mikoa mingine Bara. Barabara ya kutoka Minjingu kupitia Dodoma kwenda Iringa itakapokuwa imekamilika, kwa sababu ni sehemu ya Ilani ya Uchaguzi, itaifanya Dodoma kuwa ni *centre* sasa ya shughuli nyingine kama hizo. Kwa hiyo, hili ni jambo la msingi ambalo ni lazima liwepo.

Miundombinu kwa maana ya umeme nayo ni lazima iwepo ya kumwezesha yeyote anayetaka kuhamia Dodoma, aweze kuitumia bila tatizo kubwa. Vilevile ni lazima kuwe na huduma ya maji. Sasa haya mambo ya msingi kwa sasa ninaweza kusema, Serikali imeyapigania na tupo katika hali nzuri zaidi kuliko ilivyokuwa katika miaka ya nyuma. Hii jamani tukubali, kuhamia Makao Makuu Dodoma si suala la Jengo la Serikali hata kidogo ni suala la jamii kuwa na sababu za kwenda Dodoma, kama haipo sababu hamtaweza hata kama mngepeleka majengo mengi kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilitaka niseme kwamba, kwa upande wa Serikali tulichokwisha kuamua tangu zamani na wengi mnajua, angalau Wizara moja ya TAMISEMI yenyewe iliamua kuishi Dodoma na pengine ndiyo ninaweza nikasema jambo la msingi. Bunge letu nalo vilevile kwa maana ya Makao Makuu lipo Dodoma, kwa hiyo, nalo ni uamuzi wa msingi sana na ni wa busara sana.

Hivi sasa vyuo vikuu vinavyoibuka, yaani Chuo Kikuu cha Dodoma na chuo kile kilichoanzishwa hivi karibuni na ujenzi sasa wa msikiti mkubwa sana na pia tutakuwa na Hospitali ya Rufaa hapa Dodoma, vyote hivi vitakuwa ni kichocheo na sababu ya watu kuja Dodoma.

Mheshimiwa Spika, changamoto kwa Serikali ni sasa baada ya kuona miundombinu ya msingi ipo, kwa dhati tuamue kwamba ni vizuri Wizara sasa fulani zikaanza ku-*move physically* kuja Dodoma hatua kwa hatua. Hiyo ndiyo changamoto kubwa ambayo mimi ninaiona na italeti kichocheo kikubwa sana katika kuendeleza ukuaji wa mji wetu wa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ninamwita sasa Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mbunge wa Ubungo.

MHE. CHARLES N. KEENJA: Mheshimiwa Spika, katika miaka ya 1970, kulikuwepo msisitizo mkubwa sana wa maendeleo vijijini na kuna wakati kama utakumbuka, tulianzisha miradi ya uwiano katika baadhi ya Mikoa, kwa sasa hatusikii tena msisitizo ule; ni nini kilichotokea na je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kurudisha msisitizo ule kama njia ya kuinua hali ya maisha ya wananchi?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ninaomba nitoe maelezo kuhusiana na swali ambalo ndugu yangu, Mheshimiwa Charles N. Keenja ameliuliza, juu ya maendeleo vijijini kwa ujumla.

Inawezekana kwamba, pengine msisimko tuliouona kweli miaka ya 1970 usilinganishwe na hali ilivyo hivi sasa na mimi naamini ziko sababu za kutosha. *Rural*

Development kwa sasa maana yake Serikali za Mitaa, *especially* ndiyo wanao-*deal* na maendeleo vijijini. Jambo hili mnaweza mkalionga kama halionekani sana, lakini mimi ninataka niseme kwamba, pengine kujua tu kwa undani, lakini ipo *component* kubwa sana ya maendeleo katika maeneo yetu ya vijijiji kwa sasa, ndiyo maana unaona juhudi za kujenga shule za msingi, sekondari na barabara vijijini, ambazo tunahangaika nazo na hivi karibuni tutaingia kwenye huduma za msingi kabisa za upande wa afya, kilimo ndiyo hicho kinapewa umuhimu mkubwa sana chini ya *ASPT*, lakini *activities* zote hizi ni kielelezo kuonyesha Serikali ilivyodhamiria kuleta mabadiliko katika maeneo yote ya vijijini. (*Makofi*)

Kwa hiyo basi, pengine kinachokosekana ni kwa sababu wakati ule kweli kaulimbiu ilikuwa inajionyesha waziwazi, lakini sasa kila wakati pengine kuna mabadiliko ambayo hatuwezi kuyakataa. Bado ninafarijika kwamba, shughuli za maendeleo vijijini kwa sasa ninaweza nikasema zinasimamiwa pengine vizuri zaidi na kwa utaratibu mzuri zaidi.

Kadri fedha zinavyoongezeka kupelekwa vijijini, tutaona mabadiliko makubwa zaidi lakini kubwa ni kuongezeka tu juhudi katika suala la Utawala Bora, tukifaulu hilo tunadhani mambo yatakwenenda vizuri. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Grace S. Kwelu.

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Je, kuna mkakati gani wa Serikali wa kuhakikisha kuwa Walimu na Askari Polisi wanapewa mafunzo ili kuweza kuendana na wakati?

Hivi majuzi tumeona kuna Walimu wamekwenda kusoma na wakasimamishwa kazi; je, Serikali ina mpango gani?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, jambo aliloliuza dada yangu, Mheshimiwa Grace S. Kiwelu ni zuri sana, kwa sababu vyombo hivi ni vya msingi sana, kama mnataka kuendesha nchi yenu vizuri. Sasa ninaloweza kusema tu ni kwamba, Askari hawa muda wote kwa kweli wanapata mafunzo ya namna moja au nyingine ili kuwawezesha kusimamia kazi zao vizuri.

Ninadhani changamoto tuliyonayo kubwa ni kwa sababu mambo yanabadilika haraka sana na kwa hiyo lazima na sisi Serikalini, tuhakikishe mafunzo nayo yanakwenenda kwa kasi ili kuwawezesha Askari hawa waweze nao kujua mbinu mpya za namna ya kukabiliana na hali inayotuzunguka hivi sasa. Kwa hiyo, hata katika maeneo ya jinai, makosa sio yale yale, yamebadilika sana katika namna ya kuyatenda. Kwa hiyo ni dhahiri kabisa kwamba, ulichokisema Mheshimiwa Grace Kiwelu ni kitu cha msingi kwetu Serikali na ndiyo maana ziko jitihada kubwa sana; tumekuwa tunajaribu kuzungumza na Wamarekani katika kujaribu kuona namna gani tunaweza kuboresha Idara hasa hii ya Polisi na hasa *CID* ili iweze kufanya kazi kwa ufanisi unaotakiwa.

Kwa hiyo, juhudi hizi tutaendelea nazo na mimi nina hakika zitatuwezesha kufika mahali pazuri katika kipindi kinachokuja.

SPIKA: Ninamwomba radhi Mheshimiwa Charles N. Keenja, alisimama kwa swali la nyongeza la ufafanuzi ambalo linaruhusiwa na Kanuni zetu, lakini bahati mbaya sikumwona. Kwa hiyo, kwa kuwa limeshapita, basi nitaendelea kuwa mwangalifu, ninaona Mheshimiwa Grace Kiwelu, yeye amefanikiwa kuweza kupata swali la ufafanuzi.

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kuna lile swala la Walimu ambalo nimeuliza kwamba, wamekwenda kusoma lakini wamesimamishwa kazi kwa kwenda kusoma. Ninaomba ufafanuzi.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, sijui walikwenda kusoma wapi maana nisipolijua hilo itaniwia vigumu sana, walikwenda wapi?

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Waziri Mkuu, walikwenda kusoma Vyuho Vikuu vya Dar es Saalam.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, sasa nimemuelewa. Tatizo hili limejitokeza kutokana na sababu Fulani fulani na pengine ni jambo ambalo ni vizuri tukalielewa. Hapa katikati kulikuwa na utaratibu ambao tuliruhusu baadhi ya Walimu ambao walikuwa kwenye vidato vya sita, kufundisha katika shule zetu za sekondari. Tulipokuja kuanza kuanza hii programu nyingine, wengine wakaondoka kwenda kujiendeleza, sasa tatizo lilikuwa ni taratibu za namna ya kuondoka, ndicho kilichojitokeza. Kwa hiyo, ninaamini kabisa taratibu zile zikirekebisha na kwa sababu ni ari ya Serikali kusomesha Walimu wetu hawa wengi watarudi tena, lakini shida ilikuwa ni utaratibu uliotumika katika kuondoka, haukuwa umezingatia taratibu zetu. *(Makofi)*

MHE. MOHAMED R. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili nimuulize maswali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Vivuko ni viungo muhimu sana kwa maendeleo katika nchi yetu na kuna vivuko vingine vina hali mbaya kama Kivuko cha Pangani sasa hivi ni kibovu mno na kinahatarisha maisha ya Wananchi wa Pangani. Hivi Serikali ina mpango gani wa dharura wa kukirabati kivuko kile, kwa maana ya kupata *engine* na *propeller units* mpya mpaka hapo kivuko kipya kitakapokuja?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Mohamed Rashed Abdallah. Nimekuwa kwa kweli mara nyingine ninazungumza naye moja kwa moja, juu ya tatizo la Kivuko cha Pangani na hata Mheshimiwa Andrew John Chenge, ninadhani anajua; kwa sababu tumekuwa mara nyingi tukijaribu kulieleza jambo hili.

Lengo la Serikali ni kupata kivuko kipya, ambacho kinaweza kufanya kazi vizuri zaidi, lakini tunajua adha wanayoipata wananchi pale na hata juzi kabla Mheshimiwa Andrew John Chenge hajasafiri kwenda nje, tulilizungumza hili hili unalolisema, kwa lengo la kujaribu kuona kama tunaweza tukawa na hatua za dharura, kuwezesha kile kivuko kiweze kufanya kazi kwa muda ambapo tunasubiri kivuko cha kudumu. Kwa hiyo, rai yako ni ya msingi na tutaizingatia. Akirudi nitajaribu tuone linalowezekana ili tuweze kuwasaidia Wananchi wa Pangani. (*Makofi*)

MHE. PASCHAL C. DEGERA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali kwa Waziri Mkuu.

Kwa kuwa, moja ya Sera ni pamoja na kusogeza huduma karibu na wananchi kwa kupunguza maeneo ya utawala zikiwepo Wilaya; na kwa kuwa Wilaya ya Kondoa ni kubwa sana na nimetuma maombi ya kuigawa kwa lengo la kusogeza huduma kwa wananchi; je, Serikali ina mpango gani wa kuigawa Wilaya hiyo ili kuweza kusogeza huduma karibu na wananchi?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba, Mheshimiwa Paschal C. Degera, alishatuma maombi yao ya kuomba Wilaya ile igawanywe na pengine si yeye tu, tunayo maombi mengine mengi tu kutoka Wilaya mbalimbali; maombi haya wala si ya Wilaya tu, wengine wanataka Mikoa igawanywe; yapo maombi yanataka Kata zigawanywe; yapo maombi yanataka Tarafa zigawanywe na yapo maombi yanayotaka Vijiji vigawanywe.

Kwa hiyo ni zoezi kubwa sana, lakini ninaomba tu kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa maana ya kazi za kiofisi, jambo hili lilishachambuliwa tangu wakati wa Mheshimiwa Edward N. Lowassa, kazi iliyokuwa imebakia ilikuwa ni ndogo tu ya kujaribu kuwasilisha maombi haya sasa kwa Rais. Tulidhani hapo katikati kwamba, pengine si vibaya jambo hili likapita kwenye *Cabinet*, kwa sababu ni Wilaya nyingi sana na ni kata nyingi sana na kuna *financial implications* pale kubwa. Kwa hiyo, tulitaka pengine Mawaziri wote, tujue mzigo ambao tutaubeba ambapo tutakubali maombi hayo yote ama kwa awamu.

Kwa hiyo, ninataka nimwombe Mheshimiwa Paschal C. Degera, avute subira lakini niwaombe na Waheshimiwa Wabunge pia ambao wameshawasilisha maombi haya, wasubiri tukamilishe huo mchakato halafu baadaye Serikali itoe sasa kauli kwamba, tumeamua kufanya lipi kwa sasa, kwa kuwa tunatambua umuhimu wa kusogeza huduma ya utawala karibu na watu ili kusimamia shughuli za maendeleo vizuri zaidi. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Paschal C. Degera swali la ufafanuzi tafadhali.

MHE. PASCHAL C. DEGERA: Mheshimiwa Spika, swali la ufafanuzi ni kwamba, kwa kuwa Wilaya ya Kondoa tangu imeundwa haijaweza kugawanywa na imezidi kuwa kubwa mno; je, Waziri Mkuu atakuwa radhi kutoa kipaumbele kwa Wilaya hiyo wakati wa kugawa?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Paschal C. Degera, bahati nzuri mimi nilifanya ziara kwenye Wilaya ya Kondoa kwa kweli ni kubwa sana na ni kubwa na ninaweza nikakutamkia hapa si siri kwamba katika mapendekezo yaliyowasilishwa Kondoa tulikubali igawanywe mara mbili, kwa hiyo, hilo ni jambo la ukweli.

Kama anavyosema, tutakapofikia kuamua jambo hili, Kondoa ipewe kipaumbele, sawa tutaliangalia lakini vipo vipaumbele vingi kwenye maombi, lakini kitakachotuongoza zaidi ni uwezo wa kifedha wa Serikali, tutajaribu kuangalia sana hilo. Ninaweza nikasema kwa upande wa Kondoa, kimsingi hatuna tatizo. (*Makofi*)

MHE. LAZARO S. NYALANDU: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali kwa maswali ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, siku ya Jumatatu ...

WAZIRI MKUU: Sauti tafadhali!

MHE. LAZARO S. NYALANDU: Jumatatu iliyopita, utanisamehe sana kwa muda huu, ninafikiri hii mashine yangu inabidi iangaliwe.

Siku ya Jumatatu iliyopita, nilitembelea Migodi ya Mererani, nikakutana na Wana Apollo, wale waliokuwa wanafanya juhudi za uokoaji kwa wale ndugu zetu ambao wamepoteza maisha yao, kati ya watu 45 ambao tayari miili yao ilikuwa imeokolewa; watu 25 walikuwa wametoka Mkoa wa Singida na ninafikiri hapa unaelewa kwamba, hili suala ni gumu sana na ni msiba mkubwa sana kwa vijiji vyetu vingi sana katika Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, swali hapa ni suala zima kwamba, watu hawa wote waliozama chini, hapakuwa na mtu hata mmoja ambaye na Bima ya Maisha. Bima ya Maisha ni utaratibu ambao unaweza ukafanywa na Serikali wa kuwalazimisha wamiliki na wale vijana ambao wanaingia chini waweze....

SPIKA: Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, lenga swali. Hapa yanahitajika maswali mafupi kabisa.

MHE. LAZARO S. NYALANDU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ninaomba kujua kiseri kwamba Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Bima ya Maisha ya lazima kabisa kwa watu wanaozama chini kwenye ile migodi kuweza kuwa nayo?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, kwanza, ninamshukuru Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, kwa kuturejesha kwenye suala hili la Mererani, *catastrophe* ile ni kubwa na mimi ninadhani tusingalie tatizo hili *in a segmented form*, yaani kwa vipande vipande hivi.

Mheshimiwa Spika, nilichojifunza kwa suala hili la Mererani, ninadhani ni vizuri Serikali ikachukua tukio hili tujaribu kujifunza kwa upana wake; ni mambo gani ya

msingi ambayo ni lazima Serikali sasa tujaribu kuyafanyia kazi ili iwe ni sehemu ya juhudi za Serikali katika kuboresha shughuli nzima za wachimbaji wadogowadogo wa Madini.

Nilichokiona pale Mererani wala si suala la Bima tu, lakini lipo suala la *safety* kwa ujumla wake, kwa sababu na mimi nilikwenda Mererani pale na nilitishika. Kwanza, nilivyoona vijana wenyewe walivyo, akina Apollo wale inatisha sana, mazingira yao yote si mazingira ambayo ukienda Mererani ninayoisikia mimi inasifika, kwamba ukienda kile ndicho unachokiona. Migodi yenyewe ile ambayo inasemekana ni migodi; mazingira ambayo kwa kweli niliyaona, bado ni migodi ya hatari kabisa kwa maisha ya binadamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilichojifunza mimi ni kwamba; ni vizuri Serikali sasa tukae chini, tuangalie Sera ya Wachimbaji Wadogowadogo, kwa kutumia mifano halisi kama ile ya Mererani, mambo gani ya msingi tung'ang'anie kwa wale wenye migodi lakini na wanaofanya kazi kwenye migodi hiyo, yaweze kuwekwa katika utaratibu ambao utatuwezesha labda kuleta mabadiliko katika uchimbaji wa migodi ya aina ile.

La pili ni zana wanazotumia kuchimba migodi ile; kwa kweli kama Serikali hatutajiuliza hili jambo na tuseme ni namna gani tunaweza tukawawezesha wale wachimbaji, maana tusipowafanya wachimbaji wadogowadogo waweze kuwa na vifaa vya kisasa zaidi, matatizo haya hayawezi kuisha hata kidogo.

Kwa hiyo, ninadhani tukio lile tujifunze kwa upana zaidi, tuone Serikali tunafanye na mimi ninadhamiria jambo hili kulifanyia kazi kwa kina, kwa kujaribu kukutanisha wadau wengi kadri itakavyowezekana tulizungumze kwa upana wake, halafu tutakayojifunza tuyatumie sasa kuweka katika mfumo wa Sera.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, swali la ufafanuzi tafadhali.

MHE. LAZARO S. NYALANDU: Mheshimiwa Spika, katika kinachoendelea Mererani na juu ya matatizo ...

WAZIRI MKUU: Sauti tafadhali rafiki yangu!

MHE. LAZARO S. NYALANDU: Katika kinachoendelea Mererani na juu ya matatizo ambayo tumeyaona pale, kumekuwa na *mysterious killing diseases*; wanasema mwaka 1999 wakati wa *El-Nino* walikufa watu wote ambao walishiriki katika zoezi la uokoaji kwa wakati ule na hao vijana wanaoookoa wenzao, wanahofia sana maisha yao, kwa sababu wanapokwenda kuopoa miili kule chini, hali kule ni mbaya sana tena sana. Ninaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, atuambie juhudi ambazo Serikali inadhamiria kufanya za kiafya za kuweza kuhakikisha kwamba, hawa vijana watapata matibabu na *health care* baada ya zoezi hili la uokoaji kukamilika?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, kwamba hawa vijana watapata matibabu, mimi sidhani kama hilo ni tatizo kwa Serikali hata kidogo ni dhahiri kabisa na ndiyo maana kumekuwa na juhudi za kuona ni nini kifanyike pale kwa maana ya dawa na mambo mengine.

Ninarudia kusema, *problem* ya wachimbaji wadogo jamani ni kubwa sana, tena kubwa sana, kwa sababu hata ile migodi unayoisema, ningekwambia wewe Mheshimiwa Lazaro Nyalandu nenda huko chini kaangalie kukoje, wala usingethubutu, *it needs to be looked into*, tena *with seriousness* ili tuweze kuona ni namna gani haya yote unayoyasema; dawa ni kuzuia yasitokee kuliko kuzungumza baada ya kutokea kwa sababu haitusaidii sana. (*Makofi*)

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuhusu Zimbabwe. Nchi yetu imekuwa katika juhudi mbalimbali za kimataifa za kuleta amani. Leo tunapozungumza ni wiki ya pili toka uchaguzi ufanyike Zimbabwe, matokeo hayajatangazwa na kuna juhudi za dhahiri kabisa za Chama cha ZANUPF, ambacho ni marafiki wa chama chako, kukataa kukubaliana na matokeo yatakavyokuwa. Serikali ya Tanzania inasemaje kuhusiana na uchaguzi wa Zimbabwe?

WAZIRI MKUU: Haya ningekuwa na uwezo wa kukuuliza na mimi ningesema Kabwe unanishauri nini; tuseme nini wote? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la Zimbabwe ni kitendawili si kwa Serikali ya Tanzania, lakini ninaweza nikasema kwa Afrika yote na ninaweza nikasema hata kwa *International Community* yote; si jambo linalopendeza hata kidogo, yaani halipendezi hata kidogo. Unapokwenda kumsaidia mtu, si lazima aonyeshe dalili ya kukuomba kwamba mzee njoo unisaidie; kama hujaombwa unaweza ukainuka tu akakwambia nani kakutuma!

Kwa hiyo, unalolisema ni *concern* kwa kila mtu; sisi sote hapa *we are very much concerned* lakini ninasema tusemba tuone litakalotokea ni nini. Tunaye Mwenyekiti wa Nchi za SADC, ninadhani pengine inaweza ikawa ni kiungo cha karibu zaidi kuliko pengine hata *Chairman* wa AU. Kweli sisi Tanzania tume-*play role* kubwa sana kwa uhuru wa Zimbabwe, sasa tusemba tuone litatokea nini, maana mimi sina jibu la haraka haraka kwenye eneo hili hata kidogo. (*Makofi*)

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, mara nyingi tumekuwa tukingoja na matokeo yake maafa yanatokea na huo ni mfano ambao ulitokea Kenya.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, keshokutwa SADC wanakutana; iwapo wataamua kupeleka jeshi Zimbabwe kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunaweka amani na aliyeshinda uchaguzi anapewa haki yake ya kushinda; Tanzania itakuwa tayari kupeleka Jeshi kama ilivyopeleka Comoro? (*Kicheko*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, bahati nzuri umeliweka vizuri kwamba, je, kama itaonekana kwamba aliyeshinda uchaguzi na Serikali inaombwa kwenda

kuhakikisha huyo aliyeshinda na mifumo mingine inaendelea na kazi zake bila matatizo; je, Serikali itakuwa tayari kuridhia jambo hili?

Kwa sababu msingi wake mkubwa unaanzia hapo lakini *so far*, hatujui nani ni mshindi; tuna taarifa za juu juu tu juu ya jambo hili, kwa hiyo, ninadhani tungoje. *International Pressure* na mimi ninajua ipo kubwa, tutakapopata *a break through* na kwa kweli kama ni lazima kupeleka jeshi, *AU* nina hakika itakaa chini itatazama *what to do* na kama hapana budi watafanya hivyo. (*Makofi*)

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali.

Kwa kuwa ni sera ya Serikali kujenga zahanati kila kijiji na kujenga kituo cha afya kila Kata; na kwa kuwa hivi sasa kuna upungufu mkubwa sana wa wataalamu wa afya katika Wilaya zetu; kwa mfano, Wilaya ya Mpwapa ina upungufu wa watumishi wa afya 117; je, Serikail imeweka mikakati gani kuhakikisha kwamba wananchi watakapojenga zahanati na vituo vya afya wanapatikana watumishi wa kutosha?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa George M. Lubeleje, kwa jambo hili aliloliulizia na ninataka niseme kwamba, ndiyo maana kwenye bajeti ya mwaka huu wa 2007/2008, tuliondoa kabisa *component* ya ujenzi wa vituo vya afya na zahanati kwa sababu tuliona tutakuwa ni watu wa ajabu sana, wakati tuna upungufu mkubwa sana; tuna vituo na zahanati zaidi ya 250 ambavyo havijafunguliwa mpaka leo halafu tuseme tunaongeza vingine.

Kwa hiyo, busara iliyotumiwa na Serikali ikawa ni kufanya uamuzi wa msingi kwamba, kwa mwaka huu wa fedha, Wizara ya Afya katika bajeti yake itenge fedha kwa ajili ya *training program* kwa madaktari, wauguzi, mafamasia na watu wengine wa kundi hilo.

Kwa hiyo, *intake* ya mwaka huu itakapokuwa imemaliza masomo yake, hatua ya kwanza itakuwa kwanza, kurudi nyuma kujaza vituo na zahati ambazo hazina wataalamu wa kutosha. Wale watakaobakia, kama tutaweza kukidhi mahitaji hayo yote, ndiyo maana hata ujenzi wa zahanati na vituo vya afya mtauona utapangwa kwa namna ambayo inatuwezesha tuweze kukabiliana na hali ya upungufu hatua kwa hatua, kwa sababu tusipolifanya hilo, tunaweza tukakuta tena tuna zahanati nyingi zaidi na vituo vingi zaidi.

Kwa hiyo, tunataka tu-*merge* uwezo wa wataalamu kuwepo na ujenzi wa vituo na zahanati zitakazokuwa zinajengwa, lakini tunaamini tutakapoanza kwenye bajeti ijayo, ujenzi wa vituo na zahanati utakuwa ni mwaka wa pili wa programu ya *training*. Kwa hiyo, tutakapomaliza vituo vingi vitakuwa vimekamilika na tunaamini tutakuwa na uwezo mkubwa zaidi wa kutoa wataalamu. Huo ndiyo mkakati ambao Serikali iliutumia katika kujaribu kuhakikisha hilo alilouliza Mheshimiwa Mbunge halijitokezi.

SPIKA: Swali la mwisho kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa leo, Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas Dewji.

MHE. HASNAIN G. DEWJI: Mheshimiwa Spika, mimi swali langu ni kuhusu barabara ya kutoka Somanga kwenda Nyamwage, yenye urefu wa kilomita 65 kwa kiwango cha lami. Mwaka jana, kwenye bajeti tulitenga zaidi ya Sh. 10bn na tuliambiwa barabara hii atakabidhiwa mkandarasi mwezi wa Pili; mpaka leo Mikoa yetu ya Kusini; Lindi, Mtwara na Ruvuma, tunateseka sana kwa jambo hili; je, ni lini mkandarasi atakabidhiwa barabara hii? (*Makofi*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, anachokisema Mheshimiwa Hasnain Dewji ni kweli; tuna tatizo kubwa la kilomita zile 60 au 65 ambazo mpaka leo hazijaweza kutengenezwa kwa kiwango cha lami na tunajua ni adha kubwa sana kwa Watanzania wanaosafiri kwenda Kusini, vilevile na watu wa Kusini kuja upande wa Dar es Salaam. Si jambo ambalo Serikali ilitaka lifanyike au litendeke hata kidogo, lakini kumekuwa na mazingira ambayo yalifanya zoezi hilo likachelewa sana.

Ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Dewji kwamba, katika mchakato ambao unaendelea hivi sasa ni matarajio yetu kwamba, jambo hili tutakuwa tumelimaliza mapema. Kabla ya Juni, tutakuwa tumekwishapata mkandarasi na *process* ile itaanza kwa sababu mambo mengi yameshatatuliwa kwa kiasi kikubwa sana. Nitahakikisha jambo hili tunalisimamia vizuri na kwa bahati nzuri, taarifa hizi zimetoka ndani ya Wizara yenyewe kwamba, hadi Juni; Waswahili wanasema matatizo yote yatakuwa yamekwisha. Kwa hiyo, tufanye subira kidogo, kwa kweli haipendezi hata kidogo. Ninajua watu wanaumia sana lakini hatukuwa na njia isipokuwa kusubiri kidogo. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa jambo hili.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nina hakika nitakuwa ninawakilisha maoni na mawazo yenu nikisema kwamba, tumeanza vizuri sana. (*Makofi*)

Ninapenda nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu, Mungu huwa anachagua viongozi. Ninasema kwa dhati kabisa, namna ambavyo Mheshimiwa Pinda alivyojibu maswali hivi leo, inatupa fahari sisi Watanzania wote kwamba, tumepata Waziri Mkuu anayefaa kabisa. Tuzidi kumwomba Mwenyezi Mungu, ampe hekima na afya, aendelee kuisaidia Serikali hii ya Awamu ya Nne. (*Makofi*)

Ninawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge, mmeuliza vizuri tu, bado nitakaa na *Presiding Officers* wenzangu; huwa tunakaa tunatathmini mambo yamekwendaje ili tufanye kilicho bora zaidi siku za usoni. Ahsanteni nyote na sasa tunaendelea na shughuli inayofuata.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 31

Fedha Zilizotumika Kueleza Utekelezaji wa Bajeti

MHE. MHONGA S. RUHWANYA aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilieleza kuwa ilitumia kiasi cha shilingi 142,960,000 katika ziara ya Mawaziri kuelezea bajeti ya mwaka 2007/2008, licha ya kuwa na nafasi ya kutoa maelezo ya utekelezaji wa bajeti ndani ya Bunge la Bajeti kwa utaratibu wa kila Wizara kueleza bajeti yake:-

(a) Je, Serikali itakubaliana nami kuwa, kupanda kwa bei ya mafuta kulikosababisha mfumuko wa bei ndio sababu ya msingi iliyosababisha ziara za Mawaziri baada ya wananchi kulalamikia bajeti iliyoongeza ugumu wa maisha na kupoteza dira ya maisha bora kwa kila Mtanzania?

(b) Je, Serikali haioni kuwa hakukuwa na haja ya kutumia fedha kiasi hicho ambazo zingetumika kwa kazi nyingine zenye tija kuliko ziara ambazo hata hivyo Mawaziri walizomewa na wananchi?

(c) Je, Serikali inaweza kueleza kwa nini Mawaziri walizomewa na haioni kuwa hakuna haja ya kuendelea kuelezea utekelezaji wa bajeti bali itekeleze kwa vitendo kwani ndio matarajio ya wananchi?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, bila shaka utaniruhusu nami pia kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Ruhwanya, nikupongeze kwa dhati kwa jinsi ambavyo umekiendesha kipindi hiki cha kihistoria cha maswali kwa Waziri Mkuu. Umekiendesha kipindi hiki kwa umakini na umahiri mkubwa. Ninakupongeza sana na pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa jinsi alivyojibu maswali hayo kwa kina na kuliridhisha Bunge na Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa ninaomba nijibu swali lililoulizwa, lakini kabla sijajibu ninaomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa Kumi nilijibu swali namba moja hapa Bungeni, alilouliza Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum, akitaka kujua ni sababu zipi zilizosababisha Baraza la Mawaziri kutawanywa Mikoani, kuelezea utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi sana, Serikali ilijibu kuwa katika bajeti ya 2007/2008, ilipanga kutumia shilingi trilioni 3.141 sawa na asilimia 52.1 ya bajeti yote kwa sekta tano za vipaumbele ambazo ni Elimu, Miundombinu, Afya, Kilimo na Maji. Pili, Serikali ilisema kuwa, katika kutekeleza Sera ya kupeleka madaraka kwa wananchi (*D by D*), Serikali imehamisha kutoka Serikali Kuu, kiasi cha shilingi bilioni 286 kwenda kwenye Halmashauri; kiasi ambacho ni kikubwa kupelekwa kwenye Halmashauri kuliko wakati mwingine wowote katika historia ya nchi yetu. Kutokana na ukweli huu, Serikali

iliamua kuwatuma mikoani Mawaziri na Naibu Mawaziri ili kufafanua na kuhimiza Halmashauri, Waheshimiwa Madiwani na wananchi kwa ujumla, wasaidiane kwa pamoja kuimarisha usimamizi wa matumizi ya fedha hizo ili kuleta matokeo yaliyokusudiwa na Serikali katika Bajeti ya 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, baada ya ziara ya Mawaziri Mikoani, Serikali ilifanya tathmini kwa kupokea na kujadili taarifa za Mawaziri kutoka kila Mkoa. Pamoja na madhumuni ya Serikali yaliyoelezwa hapo juu, kupitia mikutano ya hadhara, wananchi waliupongeza utaratibu huu wa Serikali wa kuelezea bajeti na kuomba uendeleo. Aidha, wananchi walipata fursa ya kuelezea kero zao mbalimbali, ambazo baadhi zilijibiwa na nyingi zimechukuliwa na Serikali na tayari zinaendelea kushughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, kwa niaba ya Waziri Mkuu, sasa ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, sikubaliani hata kidogo na Mheshimiwa Mbunge kuwa, kupanda kwa bei ya mafuta kulikosababisha mfumuko wa bei, ndio sababu ya msingi iliyosababisha kufanyika kwa ziara za Mawaziri Mikoani. Kupanda kwa bei ya mafuta kulikosababisha mfumuko wa bei, kwa sehemu kubwa kulitokana na kupanda kwa bei ya mafuta katika soko la mafuta la dunia, hali iliyoiathiri Tanzania na nchi nyingine zote duniani. Kwa mfano, mwaka 2005, bei ya pipa la mafuta duniani lililuzwa kwa Dola 50.25, mwaka 2007 lilipanda na kufikia Dola 100 na hadi kufikia mwezi Machi, 2008 pipa hilo hilo linauzwa kwa Dola 105.90.

(b) Fedha zilizotumika katika ziara za Mawaziri ni fedha zilizoidhinishwa hapa Bungeni, kwa safari za kawaida za Mawaziri katika utekelezaji wao wa kazi wanazopaswa kufanya. Serikali inasisitiza viongozi kwenda kwa wananchi, kuwaelekeza nini wanatakiwa kufanya ili kujiletea maendeleo. Hapa hakuna anayeamini kuwa, kukaa maofisini kutawaletea wananchi maendeleo. Hivyo, Mawaziri walipaswa kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa bajeti iliyopitishwa na Bunge hili.

(c) Kutokana na mafanikio ya ziara hizi Mikoani, Serikali itaendelea kuelezea utekelezaji wa bajeti kila itakapona inafaa. Taarifa anazozungumzia Mheshimiwa Mbunge kuhusu kuzomewa Mawaziri sio za kweli, ila inawezekana kuna ushabiki wa baadhi ya watu, wasiopenda kuona mafanikio makubwa ya Serikali iliyoko madarakani sasa. *(Makofi)*

Na. 33

Masharti ya Dhamana

MHE. SAID A. ARFI aliuliza:-

Kwa kuwa, dhamana ni haki ya msingi ya mshtakiwa katika makosa ambayo mshtakiwa anaweza kupewa dhamana: Je, kulipia michango ya ujenzi au michango yoyote ile inayokusanywa na Watendaji ni sharti la lazima kabla ya kupewa barua ya utambulisho wa kuwekewa dhamana?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Said A. Arfi, Mbunge wa Mpanda Kati, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, dhamana ni haki ya msingi ya mshtakiwa yeyote yule katika nchi yetu ya Tanzania. Haki ya dhamana hutolewa kwa kuzingatia Ibara ya 13(1) na (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20; ambayo imeainisha pamoja na mambo mengine, makosa ambayo mshtakiwa hawezi kupatiwa dhamana mathalani mauaji, unyang'anyi wa kutumia silaha na ubakaji.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo, mtu anayetaka kumdhamini mtuhumiwa anayestahili kupatiwa dhamana, hupaswa kutoa nyaraka zinazomtambulisha kama kitambulisho cha ajira au barua ya Serikali ya Mtaa ili aweze kutambulika na kuaminika.

Mheshimiwa Spika, iwapo kuna mtu au taasisi yoyote itaweka kigezo kuwa michango ya ujenzi au michango yoyote inayokusanywa na watendaji wa ngazi yoyote ile katika Serikali kuwa masharti ya kutoa barua ya utambulisho wa mdhamini, huo utakuwa ni ukiukwaji wa sheria za nchi yetu na mimi ninaukemea. (*Makofi*)

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Spika, ninapenda nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa majibu yake mazuri na kwa kauli kali ambayo ameitoa hapa Bungeni, lakini nilikuwa na maswali mawili ya nyongeza. Inapotokea Wakuu wa Wilaya wanapotekeleza majukumu yao na wakatoa amri halali kwa mujibu wa madaraka waliyokuwa nayo na watendaji katika kutekeleza hiyo amri halali wakaweka sharti la kulipa hiyo michango; je, watakuwa wametenda kosa?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili ni kwamba; je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari sasa kutoa Waraka kuupitishia TAMISEMI ili watendaji katika ngazi hasa hizo za Vijiji na Mitaa waweze kutekeleza haki hii ya msingi ya mtu kupewa dhamana?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, endapo DC atatoa amri halali ya utekelezaji wa jambo lolote lile katika sehemu yake ya kazi, hakuna mtendaji anayetakiwa kuweka masharti ambayo ni kinyume cha sheria; kwa mfano, dhamana ni haki ya kila mshtakiwa katika nchi hii, isipokuwa kwa makosa fulani fulani ambayo niliyasema. Sasa endapo kuna mtu ataweka masharti ya kupewa dhamana nje ya Mahakama, inayoweza kuweka masharti ni Mahakama tu lakini nje ya Mahakama mtu huyo atakuwa hatendi haki na hastahili kufanya hivyo; ndiyo maana nikasema ninachukua nafasi hii na pia katika kujibu hili lako la pili kwamba, tumesema sheria

inasema nini. Kwa hiyo, ninachukua nafasi hii kuwataka watendaji wote wazingatie sheria, kanuni na taratibu katika utendaji wao wa kazi. Vinginevyo, watakuwa wanaweka amri zao wenyewe, watakuwa wanafanya mambo yao wenyewe ambayo hayaruhusiwi na itakuwa ni kinyume cha uendeshaji wa nchi yetu.

Na. 35

Fidia kwa Mazao Yanayokatwa na Serikali

MHE. MUSSA A. ZUNGU (K.n.y. MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH)
aliuliza:-

Kwa kuwa hivi sasa kuna malalamiko mengi kutoka kwa wananchi wanaokatiwa mazao yao na Serikali Kuu au Serikali za Mitaa kwa ajili ya ujenzi wa barabara, shule na kadhalika kwa kulipa fidia kidogo kwa mazao hayo kama minazi, mikorosho, miembe, migomba, mihogo na kadhalika kwa kulipa fidia kidogo sana kama Sh. 6,500 kwa mti mmoja wa mkorosho au mnazi:-

- (a) Je, Serikali inaweza kutaja bei ya fidia kwa kila zao kwa hayo niliyoyataja na mengine?
- (b) Je, ni nani anayewajibika kulipa fidia ya mazao hayo?
- (c) Je, ardhi inayotumiwa kwa ajili ya shughuli zilizotajwa hapo juu nayo hulipiwa fidia na ni kwa thamani gani?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mbunge wa Mafia, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Hivi sasa Serikali haipangi fidia kwa kila zao kama ilivyokuwa hapo awali. Utaratibu wa kulipa fidia ya mazao ya kilimo umebadilika kwa kuzingatia Sheria ya Ardhi Na.4 ya mwaka 1999. Chini ya utaratibu huu mpya ambao umeanza kutumika tangu mwaka 2006, viwango vya fidia vitakadiriwa kwa kuzingatia maeneo na wakati kulingana na nguvu za soko. Utaratibu huu pia utazingatia mali nyingine zilizoko kwenye eneo atakazopoteza mkulima kama majengo (nyumba/banda), miundombinu (mifereji). Aidha, kwa utaratibu huu, fidia ya zao moja mara nyingi hutofautiana kutoka eneo moja hadi lingine. Ukadiriwa wa thamani ya mazao ya kilimo utafanywa na wathamini (*Valuers*) waliopo katika Ofisi za Wilaya, wakishirikiana na Wataalamu wa Kilimo wa Wilaya. Taarifa kuhusu utaratibu huu mpya zilisambazwa katika mikoa yote ili zifikishwe kwa wakulima wote nchini.

(b) Mamlaka au mtu yeyote anayetaka ardhi, ndiye atakayewajibika kulipa fidia. Mamlaka inaweza kuwa Serikali Kuu, Halmashauri za Wilaya, Vijiji, Makampuni au Mashirika. Aidha, watu binafsi watakapohitaji ardhi watawajibika kulipa fidia.

(c) Mheshimiwa Spika, endapo yatakuwepo makubaliano kati ya wananchi na Serikali Kuu au Serikali za Mitaa, kutoa na kuchukua ardhi kwa ajili ya maendeleo yao wenyewe kwa mfano, kwa ajili ya shughuli za ujenzi wa shule, hospitali na barabara, fidia inaweza isilipwe. Aidha, yapo mazingira ambapo Serikali zenyewe zinaweza kuamua kuchukua ardhi ya wananchi kwa ajili ya maendeleo ya Taifa; kwa mfano, upanuzi wa barabara, inahitajika kulipa fidia.

MHE. MWINCHOUM A. MSOMI: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Kwa kuwa matatizo haya pia yanalikumba Jimbo la Kigamboni hasa katika uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam kwa upimaji wa viwanja.

Je, Serikali haioni kwamba, sasa umefika wakati wa kuangalia viwango hivi na kuweka viwango ambavyo kwanza vitakidhi kuwaondoshea umaskini wananchi hawa hasa kwa kuzingatia pia kwamba ndiyo uhai wa maisha yao, kwani baada ya kuwakatia mazao haya wanakuwa hawana njia mbadala ya haraka ya kukidhi maisha yao; je, Serikali haioni kwamba umefika wakati wa kungeza viwango hivi?

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa wa Kilimo, Chakula na Ushirika, ningependa kumjibu Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi, Mbunge wa Kigamboni, kama ifuatavyo:-

Kwanza, ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu mazuri na sahihi. Sasa kuhusu swali la Mheshimiwa Mbunge; ni kweli yapo malalamiko miongoni mwa wananchi kwamba, viwango vya fidia vya sasa havitoshelezi na Mheshimiwa Mbunge amesema ni vizuri tuvitazame na kwamba Mthamini Mkuu yuko Wizarani kwangu. Tumeanza kulizungumza jambo hili, kwa hiyo, ninataka nikuhakikishie Mheshimiwa Spika na Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali mara kwa mara wanatazama upya viwango vya fidia. Mara ya mwisho viliwekwa kwenye miaka ya 1990, mwaka 2004 vikatazamwa upya, mwaka 2006 vikatazamwa upya, ndiyo hivi vya sasa na hivi sasa tena tupo katika zoezi la kuvitazama upya ili vilingane na hali halisi ya gharama ya sasa.

Na. 36

Hifadhi ya Chakula Kupambana na Njaa

MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA aliuliza:-

Kwa kuwa tatizo la njaa linalosababishwa na upungufu wa chakula limekuwa la kawaida hapa nchini:-

(a) Je, uwezo wa nchi kuhifadhi chakula kupitia *SGR* umekuwa kwa kiasi gani kwa kipindi cha miaka kumi iliyopita?

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga uwezo wetu wa kuhifadhi chakula cha kutosha ili njaa iwe historia?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Charles Ogesa Mlingwa, Mbunge wa Shinyanga Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kisheria, *SGR* imewekewa kiwango cha kununua nafaka kwa mwaka kiasi cha tani 150,000. Kiwango hiki cha nafaka kimewekwa kwa sheria kwa kuzingatia kuwa kinatosheleza mahitaji ya watu watakaobainika kuwa na upungufu wa chakula (*vulnerable*) na sio kwa Watanzania wote. Aidha, kiwango hiki cha tani 150,000 za nafaka, kinatosheleza kukabiliana na upungufu wa chakula kwa waathirika wa njaa kwa muda wa miezi mitatu, muda ambao Serikali itakuwa inatafuta chakula kutoka nje ya nchi kama itabidi.

Mheshimiwa Spika, *SGR* sasa itakuwa Wakala wa Serikali hivyo, sheria yake itabadilika na viwango ambavyo *SGR* inaruhusiwa kuhifadhi vitaangaliwa upya.

(b) Mheshimiwa Spika, mahitaji ya chakula kwa watu wote hapa nchini ni tani milioni kumi kwa mwaka. Kwa kuzingatia mahitaji haya, jitihada za Serikali za kuijengea *SGR* uwezo wa kuhifadhi chakula cha kutosha ni kuweka mkazo kwanza katika kuongeza uzalishaji wa chakula hapa nchini. Hatua ya Serikali ya kuwa na utaratibu wa kuwapatia wakulima pembejeo zenye ruzuku ni moja ya jitihada hizo za kuongeza uzalishaji wa chakula hapa nchini. Kama jitihada hizo za kuongeza uzalishaji wa chakula zitafanikiwa, suala la *SGR* kuhifadhi chakula cha kutosha kwenye maghala yake na wakulima kuhifadhi chakula chao kwenye ngazi za kaya zitaimarika. Kwa kuzingatia ukubwa wa mahitaji ya chakula kwa watu wote hapa nchini, jukumu la kuhifadhi chakula hapa nchini ni la kila mtu na jukumu la *SGR* ni kuhifadhi chakula la cha dharura.

MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniruhusu kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza, ninampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Swali la kwanza, ningependa tu kufahamu uwezo wa *SGR*, Kituo cha Shinyanga ni kiasi gani na kuna mpango gani wa Serikali kuipanua kwa kuwa kinahudumia eneo kubwa la Ukanda wa Magharibi?

Mheshimiwa Spika, la pili, kwa kutumia takwimu za mvua, mimi ninafahamu kuna mzunguko wa miaka kumi, ambapo ndani yake miaka mitatu mfululizo huwa kuna uhaba wa mvua unaosababisha upungufu wa uzalishaji wa mazao ya chakula. Je, Wizara inalifahamu hilo na ina utaratibu gani wa kuwaandaa wananchi kukabiliana na hilo katika maana ya usalama wa chakula?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwa hivi sasa siwezi nikakupa idadi kamili au uwezo kamili wa *SGR* ya Shinyanga

kwamba, unahifadhi chakula kiasi gani. Taarifa hizo ninaweza kukupa baada ya kikao hiki cha asubuhi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, Serikali inachokifanya ni kusisitiza wananchi walime chakula cha kutosha, kwa kutumia kanuni bora za kilimo na kuhifadhi chakula hicho ili kiweze kutosha hadi msimu mwingine utakapofika. Kama alivyosema kwamba, kunakuwa na vipindi vya uzalishaji mzuri wa chakula na vipindi ambavyo havina uzalishaji wa chakula; kipindi kile ambacho ni kizuri basi chakula hicho kihifadhiwe ili kiweze kuwasukuma wananchi, wasiuze chakula chote kama walivyofanya kipindi cha msimu uliopita, waliuza mchele kwa wingi nchi za Uganda na Burundi mpaka wakafikia hatua ya kusaidiwa chakula na Serikali kupitia SGR. Kwa hiyo, kama nilivyosema mwanzoni, jukumu la kutunza chakula ni la mkulima mwenyewe, linaanza katika ngazi ya kaya, Serikali inaingia pale ambapo ni dharura tu ya kusaidia wakati tunaandaa jitihada nyingine za kuagiza chakula kutoka nje.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa kuniona ili niulize swali la mwisho la nyongeza. Kwa kuwa mbolea hiyo ya ruzuku ambayo imekuwa ikitolewa na Serikali kwa nia njema ili kusaidia uzalishaji wa chakula huko Vijijini, mpaka sasa hivi kwa kweli bado haijawasaidia kabisa wakulima wa kule vijijini; bei bado ni kubwa na haipatikani kwa wakati; je, Serikali sasa haioni kwamba kuna haja ya kufanya mapitio katika suala zima la usambazaji wa mbolea ya ruzuku ili wakulima wetu kule vijijini waweze kunufaika na uzalishaji wa chakula cha ziada na pia kutoa mazao yenye tija ya kuwasaidia na wao wenyewe? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwanza, nikiri kwamba bei ya mbolea kwa msimu huu iliongezeka takriban mara mbili. Kwa hiyo, bajeti iliyokuwa imepangwa ya Sh. 14.5bn ilikuwa haitoshi kupeleka mbolea ambayo ilitakiwa kupelekwa kule. Niseme kwamba, jukumu la kuwa na mbolea ya kutosha na pembejeo za kutosha kwa kila mkulima ni la mkulima mwenyewe. Serikali haina uwezo wa kusambaza mbolea ya ruzuku kwa kila mkulima nchini; kwa mfano, mahitaji ya mbolea hapa nchini, yaani *effective demand* ni tani 385,000. Kutokana na bajeti ambayo tunaiandaa hapa hapa kwenye Bunge hili Tukufu, Serikali haiwezi ikapeleka mbolea ya kutosha nchi nzima kwa maana ya kwamba, kila mkoa upate na kila zao lipate haitaweza, jukumu hilo ni la mkulima mwenyewe.

Pili, ni kweli sasa hivi tunafanya mapitio, wananchi watapata mbolea kwa kupitia njia ya vocha. Mtindo huu ambao tulikuwa tunaufanya tumegundua kwamba, ulikuwa na matatizo mbalimbali ambapo tumeshajifunza kutoka Malawi. Wakulima wale watakuwa wanapata mbolea kwa njia ya vocha, ambayo itamhakikishia mkulima yule kupata. Wapo pia mawakala ambao watapata mafunzo kutokana na fedha ambazo tumezipata kutoka kwa wafadhili. Kwa mfano, *Merinda Gate Foundation*, tutapata fedha ambazo zitawapa mafunzo na baadhi yao watapata mikopo Benki ya Taifa ya Biashara ili waweze kuwafikishia wananchi mbolea hiyo kule walipo.

Viwanda vya Dawa za ARVs

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR (K.n.y. MHE. HALIMA M. MAMUYA) aliuliza:-

(a) Je, ni viwanda vingapi vinatengeneza dawa za kurefusha maisha ya waathirika wa UKIMWI (ARVs) hapa nchini?

(b) Kati ya viwanda hivyo; je, ni vingapi vinamilikiwa na Watanzania wenye asili ya Kiafrika?

(c) Je, Serikali imenunua kiasi gani cha dawa hizo kutoka kwenye viwanda hivyo ikionyeshwa kiwango kilichonunuliwa toka kwenye kila kiwanda tangu dawa hizo zianze kutengenezwa hapa nchini?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Halima Mamuya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kipo kiwanda kimoja tu kilichoidhinishwa na Mamlaka ya Chakula na Dawa, kutengeneza dawa za kupunguza makali ya UKIMWI (ARVs). Kiwanda hicho kinaitwa *Tanzania Pharmaceutical Industries Limited* na kipo Mjini Arusha.

(b) Kiwanda hicho kinamilikiwa na Watanzania wenye asili ya Kiafrika kwa asilimia 60 ya hisa na Serikali asilimia 40.

(c) Kiwanda cha *TPI* kilianza kuzalisha ARVs na kuziingiza katika soko baada ya kupata kibali cha *TFDA* mwaka 2005. Katika miaka miwili ya mwanzo, yaani 2005/2006 na 2006/2007, Serikali haikuweza kununua dawa za kupunguza makali ya UKIMWI kutoka Kiwanda cha *TPI*. Aidha, kwa mwaka 2007/2008, hadi kufikia mwezi Machi, 2008, Serikali imekwishanunua dawa za kupunguza makali ya UKIMWI kutoka Kiwanda cha *TPI*, zenye thamani ya shilingi 3,600,335,698.00. Kiasi hiki cha dawa zilizonunuliwa kutoka *TPI* ni sawa na uwiano wa kutibu wagonjwa 25,970 kwa mwaka.

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninaomba kuuliza swali lifuatalo: Kwa kuwa baadhi ya wagonjwa au waathirika wa UKIMWI wanaotumia dawa hizo za kurefusha maisha, wanalalamikia juu ya dawa hizo kuharibu ngozi, macho kutokuona vizuri, kupungua kwa makalio na vilevile kuongezeka kwa matiti; je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba waathirika wa UKIMWI wanapata dawa ambazo hazisababishi athari hizo?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, kuna baadhi ya waathirika wanaotumia dawa hizi wamekuwa wakilalamika kwamba, wanapata madhara ambayo ameyataja Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema ni kwamba, tunapotoa dawa hizo za kurefusha maisha kama kunatokea kuna malalamiko yoyote, huwa kawaida mgonjwa anakwenda kutoa ripoti kwa daktari aliyemwandikia dawa na yule daktari anajaza fomu fulani ambayo inatakiwa ipelekwe kule *TFDA*, ambao wanaziangalia tena upya zile dawa na kuweza kuona kama kuna tatizo lolote ambalo linahusiana na dawa hizo. Hivyo basi, tunaomba kwamba, iwapo mgonjwa atapewa dawa za kurefusha maisha na ataona kwamba dawa hizo zinampa matokeo kinyume cha yale yaliyotarajiwa, basi arudi kwa mtaalamu aliyemwandikia dawa hizo ili aweze kujaza fomu. Fomu hizo zitapelekwa *TFDA* na uchunguzi wa ziada utafanywa kwa dawa hizo ili kuona kama kweli zinaathiri kama alivyozungumza Mheshimiwa Mbunge. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, suala hili ni zito, kwa hiyo, nitaruhusu maswali mawili ya nyongeza mafupi sana. Mheshimiwa Zaynab Vulu, halafu Mheshimiwa Yahya Kassim Issa.

MHE. ZAYNAB M. VULU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Mimi ninarudia swali la msingi la wenye viwanda vya uzalishaji wa dawa za *ARVs*. Kwa kuwa ni kiwanda pekee au kuna viwanda vingine, lakini kwa kuwa imesemwa kwamba ni kiwanda pekee ambacho kinamilikiwa na Waafrika Watanzania; je, Serikali ina mkakati gani wa kuongezea uwezo wa kuzalisha dawa hizo kutokana na ongezeko kubwa la waathirika wa *UKIMWI* ambao kila siku idadi inaongezeka na majibu ya msingi yamesema kwamba wameweza kununua dawa za shilingi 25,000 tu? Hilo swali la kwanza.

Swali la pili, je, ...

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge swali moja tu.

MHE. ZAYNAB M. VULU: Mheshimiwa Spika, ni swali hilo hilo lakini limeunganika.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, haiwezekani.

MHE. ZAYNAB M. VULU: Kwa kuwa *WHO* ...

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, kanuni haziruhusu. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, ninaomba uniruhusu nifanye marekebisho kwamba, mimi nimesema thamani ya fedha zilizotumika kununua dawa na nimesema uwiano wa kutibu wagonjwa 25,970 na

nikasema kwamba kiasi tulichonunua ni shilingi 3,600,335,698. Ninaomba nifanye marekebicho hayo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba nimjibu kwamba, hiki kiwanda kwa sababu ni cha wazawa, wanapotaka kuuza dawa Serikalini, kawaida huwa wanaenda kwa mtindo wa *tender*. Sasa Serikali huwa inaangalia bei ambazo wana-*tender* wale wazawa na kawaida hata kama wenyewe wata-*bid* kwa bei ambayo iko chini. Mara nyingi sisi kama Serikali, huwa tunawapa nafasi ya kutuuzia dawa hizo ukilinganisha labda na wale ambao wame-*bid* toka makampuni yanayotoka nje ya nchi. Hiyo ndiyo mikakati ambayo tunaifanya ili kuweza kuvisaidia hivi viwanda vya wazawa wa Tanzania.

MHE. YAHYA KASSIM ISSA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Kwa kuwa Serikali inachukua jukumu la kununua dawa ili kuwapa wagonjwa hao kuendeleza siku zaidi katika maisha yao; je, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha kwamba hao wanaopewa dawa hawaendelezi vitendo viovu wakati wakishapata dawa inapotokezea kwamba hakuna dawa itakayoweza kuwafanikisha wale waliowarithisha?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, nilivyomuelewa Mheshimiwa Mbunge, anataka kuona kwamba hawaendelei kuambukiza watu wengine kwa sababu wanapata dawa.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba watu wote tumeambiwa kwamba, lazima tuhakikishe kwamba hatuambukizani Ugonjwa huo wa UKIMWI. Kwa hiyo, tusieneze maambukizo mapya. Kwa wale ambao wanapata dawa, huwa wanapata maelekezo kwamba kutumia dawa haina maana kwamba hutaweza kuambukiza mtu mwingine. Kwa hiyo, Serikali au wataalamu huwa wanawafuatilia na kuona kama wanatumia dawa kama inavyotakiwa, vlevile hawapati maambukizi mapya, lakini wakati huo huo pia hawawaambukizi watu wengine kwa kisingizio kwamba wanatumia dawa.

Na. 38

Vikao vya Waganga na Wauguzi vya Asubuhi

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE aliuliza:-

Kwa kuwa, Waganga na Wauguzi hufanya vikao kila siku asubuhi kabla ya kuanza matibabu na kwamba, vikao hivyo huchukua muda mrefu; na kwa kuwa wakati huo wote wagonjwa wengi hurundikana sana wakisubiri huduma:-

- (a) Je, huo ndio utaratibu uliowekwa?
- (b) Je, hivi ni lazima vikao hivyo vifanyike asubuhi tu, tena kila siku?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, ningeomba utumie *microphone* ya hapa, naona hiyo ina kasoro hausikiki vizuri.

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, huduma za afya katika vituo vyote vya kutolea huduma, hutolewa kwa saa 24. Tofauti na mchana, wakati wa usiku huduma hutolewa na watumishi wachache ambao wako zamu. Kwa sababu hiyo, umewekwa utaratibu maalum kwa menejimenti ya vituo hivyo, kupokea taarifa ya huduma zilizotolewa kwa kipindi cha saa 12 za usiku, kwa mfano, kupata taarifa ya wagonjwa waliolazwa, hali zao, huduma walizopatiwa na ni mgonjwa au wagonjwa gani wanahitaji huduma ya haraka. Vilevile wakati wa kupokea taarifa hizi, menejimenti hujadili matatizo yanayohitaji ufumbuzi wa pamoja. Hii ndiyo sababu kubwa ya wahusika kukutana pamoja asubuhi.

Mheshimiwa Spika, katika vituo vya kutolea huduma za afya ngazi ya kwanza na ya pili, utaratibu unaotumika ni wa menejimenti ya vituo husika kukutana pamoja kila siku asubuhi. Aidha, katika Hospitali za Rufaa, kila Idara huwa ina utaratibu wa kujadili hali za wagonjwa na masuala mengine kila siku.

Mheshimiwa Spika, ni vyema vikao hivyo vifanyike asubuhi kwa sababu watoa huduma waliokuwa zamu ya usiku ndiyo hutakiwa kutoa taarifa ya huduma zilizotolewa kabla ya kwenda kupumzika. Kama nilivyosema hapo juu, wanaohudhuria vikao hivyo ni Wakuu wa Idara na wa Sehemu mbalimbali za Hospitali, watumishi wengine huendelea kutoa huduma kwa wagonjwa kama kawaida. Aidha, kama kutatokea mgonjwa kuhitaji huduma ya mtumishi anayehudhuria kikao, mtumishi huyo huruhusiwa kwenda kutoa huduma hiyo. Vikao hivi ni muhimu kufanyika kila siku, kwa sababu watoa huduma wako zamu kila siku na hivyo ni lazima taarifa itolewe kila siku kwa manufaa ya wagonjwa na watu wengine wanaokuja kupata huduma katika hospitali hapo kila siku.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali ya nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri:-

(a) Kwa kuwa mara nyingi wagonjwa wanapokuwa wanasubiri Waganga wengine huzidiwa, pengine kuzimia na kupoteza maisha; je, ni kwa nini Serikali isibadili utaratibu wakawepo Waganga wengine wa kuwepo *OPD* kuendelea kutoa huduma wakati Waganga wengine wanapokuwa wanaendelea na vikao vingine? (*Makofi*)

(b) Kwa kuwa mara nyingi huduma ya kutibu huanza saa 2.00 asubuhi, lakini kutokana na vikao hivyo huduma huanza kutolewa saa 4.00 asubuhi au saa 5.00 na hali hii imejitokeza mara nyingi na wagonjwa wengine hutoka nje ya Makao Makuu ya Wilaya kwenda kupata huduma katika Makao Makuu ya Wilaya kutokana na rufaa wanazozipata kutoka kwenye Zahanati; je, ni kwa nini usiwepo utaratibu wa kuanza

kutibu wagonjwa mapema ili wagonjwa wanaokuwa na matatizo kama kung'olewa meno waweze kupata huduma mapema na kurejea nyumbani mapema?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi, nimesema kwamba, wakati vikao hivi vinapokaa na wale viongozi wa Idara wanapokutana, shughuli zinatakiwa ziendelee kufanyika kama kawaida. Kwa maana hiyo, kama kuna mgonjwa yeyote atakuwa amezidiwa kwenye foleni akisubiria madaktari ni lazima mgonjwa huyo awe anaonwa na iwapo atahitaji huduma ya ziada labda kwa yule ambaye yupo anahudhuria kikao, basi anatakiwa aitwe mara moja ili aweze kwenda kuendelea kumshughulikia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu (b), huduma kama alivyosema ni kweli zinatakiwa zianze asubuhi, lakini nimesema katika ngazi ya kwanza na ya pili, huduma ni saa 24. Kwa maana hiyo, mimi sioni mantiki gani na kwa nini mgonjwa aendelee kusubiri mpaka saa 4.00.

Mheshimiwa Spika, ninapenda niseme kwamba, kawaida wagonjwa wote saa 24 wanatakiwa waendeleo kupata huduma na kwa maana hiyo basi, wanapokuwa wanafanya vikao vyao vya asubuhi, uwekwe utaratibu wale wengine waendeleo kutoa huduma na kama itaonekana kwamba wengine wanahitajika waendeleo basi wakaitwe.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, ninachukua nafasi hii kutoa wito kwa wote wanaotoa huduma, kujipanga vizuri ili kuhakikisha kwamba, wagonjwa wanahudumiwa saa 24 na wakati huo huo vikao hivyo vya asubuhi viendelee kama utaratibu unavyotaka. *(Makofi)*

Na. 39

Kurekebisha Mfumo wa Umeme Tunduma

MHE. DR. LUKA J. SIYAME aliuliza:-

Kwa kuwa, Mji Mdogo wa Tunduma Wilayani Mbozi hupata umeme wenye nguvu hafifu ya KVA 11 badala ya KVA 33 ambazo zinahitajika kukidhi mahitaji; na kwa kuwa mwezi Oktoba, 2007 Serikali kupitia aliyekuwa Waziri Mkuu iliahidi kurekebisha mfumo huo wa umeme haraka inavyowezekana: Je, ni lini mfumo huo wa umeme utarekebisha ili pamoja na mambo mengine uweze kuendesha mashine za majokofu ya kuhifadhi maiti katika Kituo cha Afya cha Tunduma?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Luka Jelas Siyame, Mbunge Mbozi Magharibi, ninapenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, hali ya upatikanaji umeme Wilayani Mbozi si nzuri na ni kweli kwamba, ilitoa ahadi ya kutafuta ufumbuzi wa tatizo hili kwa muda mfupi mwezi Oktoba, 2007. Hatua ya kubadilisha upatikanaji wa umeme kutoka KVA 11 hadi KVA 33 ina gharama kubwa lakini hata hivyo hatua za lazima za kutekelezwa, zitachukuliwa kulingana na ahadi ya Serikali. Serikali inapenda sana kuwahakikishia Wananchi wa Wilaya Mbozi na Wilaya nyingine kwamba, tunafanya kila jitihada kupata umeme wa uhakika ili wananchi wake wautumie katika kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Luka Jelas Siyame, Mbunge wa Mbozi Magharibi, kama ifuatavyo: Tatizo kubwa la umeme Wilayani Mbozi linatokana na matatizo ya upatikanaji umeme unaotoka nchini Zambia, ambako Shirika la Umeme (*TANESCO*), hununua umeme ili kuyapatia umeme maeneo ya Tunduma na Mbozi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo mafupi hapo juu, Serikali itafanya marekebisho ya kubadilisha njia ya umeme kutoka Kilovoti 11 hadi Kilovoti 33, mara fedha za kufanya kazi hiyo zitakapopatikana. Pia Serikali itaendelea kufuatilia kwenye Shirika la Umeme *ZESCO* la Zambia ili kutafuta ufumbuzi wa upatikanaji wa umeme mdogo katika maeneo ya nchi yetu yanayotumia umeme unaotoka nchini Zambia. Taarifa tulizopokea ni kwamba, Zambia nako kama nchi nyingine za maeneo yetu, inakabiliwa na matatizo katika uzalishaji wa nishati ya umeme, hali inayoathiri upatikanaji wa umeme kwa ujumla. Serikali itasimamia Shirika letu la *TANESCO* wawasiliane na wenzao wa *ZESCO*, wafanye tathmini ili tufahamu matarajio ya uwezekano wa kupunguza tatizo hili kwa kipindi kifupi kijacho kulingana na hali ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, ufumbuzi wa kudumu upo katika kuwekeza katika vyanzo vyetu wenyewe ili kuzalisha na kusambaza umeme kwa kiwango kikubwa zaidi na cha uhakika.

Mheshimiwa Spika, uhaba wa fedha na ufinyu wa bajeti vimekuwa tatizo kubwa katika kutekeleza mipango na mahitaji mbalimbali ya Serikali na miradi ya umeme katika kuyapatia huduma ya umeme maeneo mbalimbali nchini.

MHE. DR. LUKA J. SIYAME: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Ninapenda kabla ya yote niseme, ninasikitika kuwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri hayakuniridhisha. Kwa sababu katika ile ziara tuliyokuwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu tuliyokuwa tumepata kwa Meneja wa Ugavi wa *TANESCO* juu ya urekebishaji wa mfumo wa umeme pale Tunduma, ilikuwa kwamba ni suala dogo tu linahitaji Meneja wa Mkoa wa Mbeya kwenda pale na kubadilisha nyaya na si suala la kuhitaji fedha za ziada.

Baada ya hapo, ninaomba sasa niseme hivi sasa pale Tunduma kuna matukio mawili mabaya ambayo yametokea kutokana na matatizo ya umeme. Moja, hivi sasa hata ile *transfoma* ambayo walikuwa wameileta mwaka jana imekwishakuharibika na

hivyo kusababisha giza kuu katika eneo la Tunduma Kati na kama mnavyoelewa Tunduma ni Mji ambao watu hawalali. Lirilotokea hivi sasa ni wimbi kubwa kabisa la uhalifu ikiwa ni pamoja na ujambazi. Pili tulikuwa katika utaratibu wa kuchimba visima viwili vya maji kwa ajili ya kutatua matatizo hapo. Hivi sasa tunaomba kufahamu ni hatua gani za dharura ambazo zitachukuliwa na Serikali kuweza kunusuru maisha ya watu na mali zao pale Tunduma?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, ninatumaini majibu yatakuwa mafupi, swali la nyongeza lilikuwa refu kupita kiasi.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, katika majibu yangu ya swali la msingi nilikuwa nimesema kwamba, kuna matatizo ya ujumla ya upatikanaji mdogo wa umeme unatokana na umeme unaotoka Zambia. Umeme unapotoka Zambia ukifika pale Tunduma, bado kuna hatua za kufanywa pale pale Tunduma; kama suala hilo la *transfoma* ambayo ni mbovu. Sasa nilichomwambia ni kwamba, Shirika la *TANESCO* ambalo ndilo inabidi lishughulikie suala hili; kwanza, itabidi lidhibiti tatizo la umeme mdogo unaotoka Zambia kuja huku, halafu hapo hapo hata umeme huo ukija, bado kuna masuala ya kuzingatiwa katika kuubadilisha. Sidhani kama tatizo ni *transforma* iliyoharibika na bado tatizo litakuwa ni kubadilisha nyaya tu. Kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Mbunge, atupe muda ili *TANESCO* wafanye tathmini ya mambo yote mawili; kwanza, upatikanaji wa umeme kutoka Zambia, lakini pili ni usambazaji wa umeme huo huo ukishafika pale Tunduma. Ahsante sana.

SPIKA: Ninadhani nimpe haki jirani yake Mheshimiwa Godfrey Zambi, swali la nyongeza.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa mwaka jana niliwahi kuuliza swali linalohusiana na matatizo ya umeme tunaopata kutoka Zambia; na kwa kuwa Serikali ilijibu kwamba, itaifanyia kazi sasa ni takriban mwaka mzima; kwa nini Serikali leo tena inakuja na majibu kwamba itazungumza na Shirika la Umeme la Zambia, wakati mwaka mzima umepita?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, labda nikiri tu kwamba, Serikali ilitoa majibu hayo. Ukweli ni kwamba, tatizo la umeme la Zambia, upatikanaji wa umeme ambako kusema kweli Wilaya ya Mbozi ndiko inakotegemea umeme wake utoke kwa hivi sasa hadi sisi kama Taifa tutakapoweza kutegemea kuzalisha umeme mkubwa zaidi wa kujitegemea sisi wenyewe, bado tatizo la umeme kule Zambia ni kubwa kwamba umeme unaokuja ni mdogo. Sasa ninamwomba Mheshimiwa Godfrey Zambi, amekwishakuja Wizarani na tumekubaliana kwamba tutalifuatilia tatizo la upatikanaji wa umeme huo unaotoka Zambia. Tutahakikisha kwamba, tutakapoanza kuzalisha umeme wetu wenyewe wa ndani, maeneo ya jirani toka Kanda nzima yatakayotegemea uzalishaji wa umeme utakaozalishwa badala ya Kiwira kuingia kwenye *generation*, basi ninaomba tuvute subira, lakini tuendelee kufuatilia kwa pamoja ili tulipatie ufumbuzi tatizo hili katika muda ujao.

Hitaji la Umeme Rukwa

MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA aliuliza:-

Kwa kuwa, umeme toka Zambia umeonekana kuwa hautoshi, hali inayosababisha ukosefu wa umeme katika Mji wa Sumbawanga mara kwa mara:-

(a) Je, ni lini Serikali itaanza mradi wa kuunganisha Mkoa wa Rukwa katika *Grid* ya Taifa kutoka Mkoa wa Mbeya ili Mikoa yote ipate umeme wa kutosha kwa maendeleo yake?

(b) Kwa kuwa wananchi katika Jimbo la Kalambo wameomba umeme uteremshwe katika Mji Mdogo wa Matai na usambazwe katika Jimbo lote; je, ni lini hilo litafanyika?

(c) Je, isingekuwa busara kwa *TANESCO* kutafuta vyanzo vingine vya umeme kwa kutumia maji ya mito iliyopo Rukwa na mitambo ya kuendeshwa kwa makaa kwa kushirikiana na wazalendo kama anavyofanya Casiano Kayegele wa *Upendo Group* ili umeme huo uingizwe kwenye gridi ya Mkoa wa Rukwa kwa lengo la kuvipatia umeme Vijiji vya Kalambo na Nkasi?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ludovick John Mwananzila, Mbunge wa Kalambo, ninapenda nieleze kuwa, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, umeme wa kutoka Zambia kama nilivyosema katika majibu ya swali lililopita, unakatika mara kwa mara na hauna nguvu ya kutosha. Vilevile mgao wa umeme husababishwa na kuharibika kwa mitambo ya kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Ludovick John Mwananzila, Mbunge wa Kalambo, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kuunganisha Mkoa wa Rukwa katika Gridi ya Taifa kutoka Mbeya, kumejumuishwa katika mpango wa umeme ujulikanao kama *North West Grid*. Mpango huu unahusu kuunganisha kwenye Gridi ya Taifa; Miji ya Mbeya, Tunduma, Sumbawanga, Mpanda, Kigoma, Kibondo, Nyakanazi na Maporomoko ya Rusumo. Kwa sasa Serikali inatafuta wafadhili wa kuweza kuufadhili mradi huo kwa ujumla wake.

(b) Mheshimiwa Spika, Mji Mdogo wa Matai uko karibu na umeme wa msongo wa kilovoti 66 unaotoka Zambia. Ili kuweza kuusambaza umeme huo, inabidi kwanza kijengwe kituo cha kupoza umeme kutoka kilovoti 66 hadi kilovoti 33. Gharama za ujenzi wa kituo ni zaidi ya Dola za Marekani milioni 1.5.

Mheshimiwa Spika, mahali ambapo umeme wa kilovoti 66 unachukuliwa nchini Zambia ili usafirishwe kuletwa nchini kwetu, matumizi ya umeme katika sehemu hiyo yamekuwa makubwa. Hivyo, umeme unaposafirishwa hadi maeneo ya nchi yetu yanayotumia umeme wa Zambia, unakuwa umeshapungua nguvu kiasi kwamba si busara kuongeza watumiaji wengine upande wa nchi yetu kabla ya kuongeza uwezo wa njia hii. Ili umeme wa uhakika uweze kupatikana katika maeneo ya nchi yetu yanayotumia umeme wa Zambia, inabidi miundombinu ya umeme upande wa Zambia pia iboroshwe.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali ikiendelea na jitihada za kutafuta njia muafaka ya kufikisha umeme katika Mji wa Matai na hatimaye Jimbo lote la Kalambo, ninaomba Wananchi wa Jimbo la Kalambo waendeleo kuvuta subira.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali ikishirikiana na *TANESCO*, pamoja na wadau wengine, imekuwa ikitafuta vyanzo mbalimbali vya kuweza kufikisha umeme maeneo mbalimbali hapa nchini. Kikwazo kimeendelea kuwa ukosefu wa fedha, kuweza kutekeleza miradi iliyopendekezwa. Kwa Mkoa wa Rukwa, utafiti ulifanywa kwenye Maporomoko ya Mto Nzovwe, ambayo yana uwezo wa kuzalisha megawati nane. Gharama za kujenga kituo hicho cha kuzalisha umeme katika maporomoko hayo, zinakadiriwa kuwa Dola za Marekani milioni 21.8. Serikali inatafuta fedha ndani na nje ya nchi, kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho.

MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri, ni jambo la kusikitisha kwamba, Wilaya ya Mbozi na Mkoa wa Rukwa, tunazungumzia tatizo la umeme unaotoka Zambia ambao hautoshelezi na umekuwa ni tatizo kubwa na yeye mwenyewe Naibu Waziri amekiri. Mwaka 2001 nilizungumza na aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Daniel Yona, kuhusu kiwango cha fedha cha Dola za Marekani 200 zilizokuwa zimebakishwa katika mradi ule kwa ajili ya kuangalia ni jinsi gani ya kukarabati au kuongeza miundombinu.

Fedha hizo zipo *TANESCO* na mpaka leo zimefichwa hawataki kuzizungumzia; kwa nini fedha hizo zisitumike ili kujaribu kusaidia kupata umeme wa Gridi ya Taifa kutoka Kidatu, Mbeya, Tunduma, Sumbawanga mpaka Mpanda kuliko kufikiria mradi mkubwa ambao wanafikiri sijui utakuwa ni *North West Grid* ambao hatujui utapatikana namna gani?

Pili, Mheshimiwa Naibu Waziri anaelewa kwamba maendeleo ya Mkoa wa Rukwa na nchi nzima bila umeme ni kazi bure. Pia vyanzo anavyovizungumzia vya Mto Msovyo, amesahau kuzungumzia suala la mkaa wa mawe unaopatikana pale Sumbawanga. Je, ni lini *TANESCO* au Serikali watafanya juhudi ya kuweza kuhakikisha kwamba umeme wa kutumia mkaa wa mawe wa Namwele unasaidia kupata umeme katika eneo hili la Mbozi, Sumbawanga, Mpanda na Nkansi?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, nakubali kwamba Mheshimiwa Mbunge amezungumzia tatizo hili la umeme katika Wizara ya Nishati na Madini kwa muda mrefu uliopita. Lakini labda nieleze tu kwamba tatizo la kubadilishana umeme kutoka nchi moja hadi kwenda nyingine sio jambo la ajabu. Nadhani ni jambo la kawaida. Zambia wanachukua umeme kutoka Congo, Zambia wenyewe wanapopata umeme wao, wanagawa Zimbabwe, halafu tunachukua umeme kutoka Zambia mpaka huu wa Kaskazini na Kenya upande wa Horohoro, tunawapa Kenya na Namanga. Kwa hiyo, tunatarajia tupate umeme kutoka kwao na haya ni mambo ambayo kusema kweli yanategemea na miundombinu iliyopo kwa kila upande.

Mheshimiwa Spika, tukubaliane tu kwamba katika suala la miundombinu ya umeme iliyokuwepo kwa sasa hivi na uwekezaji ambao umekuwa unafanywa kwa miaka yote, uwezo wa leo na kesho kupata umeme kwa maeneo haya tunayoyazungumza yanatokana na umeme wa Zambia. Kwa hiyo, tukae na wenzetu tuzungumze nao tuangalie namna ambavyo wanaweza kuboresha upatikanaji wa umeme kutoka kwao. Lakini vile vile tutambue kwamba wana tatizo la umeme kama ilivyo kwa Tanzania, Zambia, Zimbabwe, Afrika ya Kusini, kote tu tuna matatizo. Lakini nikubali kwamba ni jambo ambalo tunatakiwa tulifanyie kazi na naahidi tutalifanyia kazi na nitampatia majibu Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge amezungumzia kwamba kuna fedha zimefichwa *TANESCO* tangu mwaka 2001 ambazo zingesaikia kuboresha miradi hii. Labda nitamke ukweli kwamba sina taarifa ya fedha hizo zilizofichwa kwa sababu kwa ufahamu wangu *TANESCO* yenyewe ina matatizo ya fedha. Lakini ni jambo ambalo naomba Mheshimiwa Mbunge tukutane nipate maelezo ya ziada ili baadaye tulifuatilie jambo hili na tulifanyie kazi. Kama fedha zimefichwa na zimekaa tu maeneo yanayohitajika kufanyiwa kazi nadhani sio jambo la sawasawa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mkaa wa mawe nadhani kwa sasa hivi kama nilivyosema, uwekezaji mkubwa unaofanywa kwa kanda nzima ile ni umeme wa Kiwira ambao tunatarajia utaingia kwenye *generation* ya uzalishaji mwaka 2009. Tulitaja mradi wa umeme wa Msovyo ili kutoa picha kamili ya uzito wa miradi ya umeme kulingana na gharama lakini pia na muda. Hata tukianza kufanya kazi leo mradi wa Msovyo utaingia kwenye *generation* baada ya miaka mitatu au minne.

Kwa hiyo, ndiyo maana tukasema tunaomba kwa hivi sasa umeme unaopatikana ni huu unaotoka Zambia lakini hatuwezi kutegemea umeme kutoka Zambia. Jambo la busara kama ulivyosema.

Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, kwa sababu tuna makaa ya mawe, tuna maji ya Rusumo, Somve, Ruhuji ambapo Ruhuji peke yake inaweza ika-*generate* kilowati 300, sasa ni wakati muafaka wa Serikali na Bunge hili kukaa kuendeleza vyanzo vya umeme ili kutathmini kuendeleza vyanzo vya umeme ambavyo ni vya kwetu sisi wenyewe. (*Makofi*)

MHE. BENSON M. MPESYA: Mheshimiwa Spika, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika majibu ya Mheshimiwa Waziri hayaonyeshi dhamira ya wazi kwamba umeme utakaozalishwa Kiwira utaelekezwa maeneo ya Tunduma na Sumbawanga kwa sababu hapo ni jirani. Ni kwa nini hawaonyeshi nia kabisa kwamba umeme utakaozalishwa Kiwira *megawatt* 200 utaelekezwa maeneo hayo ili kutatua matatizo?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, umeme utakaozalishwa Kiwira *megawatts* 200 kwa mahitaji ya jumla ya maeneo ya karibu pale ni umeme mwingi sana. Kwa hiyo, ni wazi kabisa kwamba hata katika misingi ya biashara tu umeme wenyewe lazima utafute masoko ya watu na masoko ya karibu ni maeneo ya pale pale karibu ambapo kuna mahitaji ya umeme kama tulivyosema.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie rafiki yangu Mheshimiwa Benson Mpesya amesema tuonyeshe nia ya dhahiri. Naomba nimhakikishie kwamba nia yangu ni ya dhahiri kabisa na kwamba kwa misingi tu ya kibiashara achilia mbali misingi mingine maeneo ya Mbozi, Tunduma, Mbeya ndiyo masoko ya awali kabisa ambayo umeme huu unatarajiwa kupelekwa.

MASWALI YALIYOJIBIWA KWA MAANDISHI

Na. 32

Mapendekezo ya Tume Juu ya Wafanyakazi Wanaofukuzwa Kazi

MHE. MKIWA A. KIMWANGA aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwa na malalamiko kutoka kwa baadhi ya watumishi wa Serikali wanaofukuzwa kazi kuwa hawalipwi hata nauli ya kuwarejesha makwao; na kwa kuwa malalamiko hayo yalipelekwa mbele ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na baada ya uchunguzi Tume ilitoa mapendekezo yake kwa ajili ya utekelezaji:-

Je, ni mapendekezo yapi yaliyotolewa na Tume na ni kiasi gani yameshatekelezwa hadi sasa?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, kuhusu watumishi wa Serikali kupatiwa usafiri wa kwenda kwao baada ya kufukuzwa kazi, inaonyesha kuwa kati ya mwaka 2005/2006 na mwaka 2007/2008, Tume ilipokea jumla ya malalamiko 62 kutoka kwa watumishi wa umma waliofukuzwa kazi bila ya kupatiwa usafiri wa kurejeshwa kwao (*place of domicile*) kama ifuatavyo: Mwaka

2005/2006 watumishi 16, mwaka 2006/2007 watumishi 35 na mwaka 2007/2008 watumishi 11.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa hiyo Tume ilipendekeza kwa Serikali kuwa, watumishi hao wanayo haki ya kurejeshwa kwao baada ya kufukuzwa kazi. Kifungu cha 40(1) cha Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003 kinaelekeza kuwa, baada ya mkataba wa ajira kumalizika (*termination of contract*), mtumishi atapaswa kupatiwa usafiri wa kumrejeshwa kwao yeye na familia yake, pamoja na mizigo yake. Hata hivyo, kifungu cha 40(2) kinafafanua kuwa, haki hiyo ya kupatiwa usafiri huo, haitawahusu watumishi ambao mkataba wao wa ajira utakuwa umesitishwa kutokana na kupatikana na makosa ya rushwa au matumizi mabaya ya fedha/mali ya umma. Aidha, kifungu cha 43 cha Sheria ya Ajira na Mahusiano ya Kazi kinaelekeza kuwa, mkataba wa ajira unapositishwa, mtumishi anayo haki ya kurejeshwa kwao pamoja na mizigo yake.

Na. 34

Kuwawekea Vijana Mazingira Mazuri ya Kilimo Vijijini

MHE. SALIM HEMED KHAMIS aliuliza:-

Kwa kuwa, Tanzania ina eneo la hekta milioni 44 linalofaa kwa kilimo lakini ni asilimia 4.3 ya eneo hilo ndio inayolimwa; na kwa kuwa vijana wengi kutoka vijijini wanakimbilia mijini kufanya kazi zisizo halali na kukiacha kilimo kwa wazee waliochoka:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka mazingira yatakayofanya vijana wabaki vijijini na kuendeleza kilimo?

(b) Je, Serikali inazo takwimu kwa kila Mkoa za vijana wasio na kazi na maeneo ambayo hayalimwi?

WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Salim Hemed Hamis, Mbunge wa Chambani, ninapenda kutoa maelezo ya awali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, ninaomba nisikubaliane na Mheshimiwa Mbunge ya kwamba, vijana wengi hutoka vijijini kukimbilia mijini kwenda kufanya kazi zisizo halali na kazi ya kilimo huko vijijini inaachiwa kufanywa na wazee waliochoka. Ukweli ni kwamba, vijana wengi wanaotoka vijijini kwenda mijini, huenda kujitafutia kazi halali za kujipatia riziki na wala kazi ya kilimo huko vijijini haifanywi na wazee waliochoka; wapo vijana wengi na watu wazima wenye nguvu wanaojishughulisha na kazi za kilimo vijijini.

Mheshimiwa Spika, kuna sababu kadhaa zinazosababisha baadhi ya vijana kutoka vijijini kwenda mijini, ikiwemo dhana iliyojengeka kuwa, mijini kuna maisha mazuri zaidi, huduma muhimu za maisha hupatikana kirahisi zaidi na miundombinu ni bora zaidi kuliko zilizoko vijijini. Pamoja na hayo yote, hali ya watu kuhamia mijini ni ya kwaida kwa nchi nyingi duniani na hali hii inaweza kuwa na matokeo ya maendeleo ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Salim Hemed Hamis, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, baadhi ya mipango iliyowekwa na Serikali ili kuweka mazingira yatahayawavutia vijana kwenye shughuli za kilimo vijijini ni pamoja na:-

(i) Kuwaongezea vijana ufahamu kupitia mafunzo mbalimbali kuhusu Sera na Mikakati ya Kilimo ikiwa ni pamoja na kuainisha fursa mbalimbali zilizopo vijijini, hususan kwenye kilimo na shughuli nyingine za uzalishaji na kuwahamasisha vijana kuzitumia.

(ii) Kuhamasisha uanzishwaji wa vikundi vya vijana na SACCOS ili kuweza kuwapa huduma muhimu pale walipo kiurahisi zaidi. Huduma hizo ni pamoja na upatikanaji wa mitaji, mafunzo ya taaluma mbalimbali, mafunzo ya ujasiriamali na kadhalika.

(iii) Kupeleka huduma muhimu vijijini kama maji, umeme, mawasiliano na vituo vya starehe ili kuwafanya vijana wasilazimike kuzifuata mijini.

(iv) Kuongeza tija kwenye kilimo kwa kuboresha huduma za ugani, upatikanaji wa pembejeo, masoko ya uhakika na fursa za kupata zana za kisasa kirahisi ili kilimo kiweze kuwapatia tija zaidi.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa majibu wa matokeo ya utafiti kuhusu watu wenye uwezo wa kufanya kazi, wasio na kazi (*Integrated Labour Force Survey*) ya 2006, yaliyotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu, yanaonyesha kuwa, vijana (miaka 15 – 35) waliokuwa na uwezo wa kufanya kazi lakini hawana kazi ni 1,398,677; kati yao wanaume ni 598,015 na wanawake ni 800,666. Takwimu hizo zinaonyesha kwa mfano, Mkoa wa Dar es Salaam una vijana 463,343 wasiokuwa na kazi; kati yao wanaume ni 172,765 na wanawake ni 290,578. Miji mingine yote ya Tanzania Bara ina jumla ya vijana 348,620 wasio na kazi; ambao kati yao 128,322 ni wanaume na 220,304 ni wanawake. Kwa upande wa vijijini, wapo jumla ya vijana 586,708; ambapo kati yao wanaume ni 296,928 na wanawake ni 289,780.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa takwimu zinazohusu kilimo, nchi yetu ina hekta 43 milioni zinazofaa kwa kilimo, ambapo eneo linalolimwa hivi sasa ni hekta milioni saba, ambayo ni sawa na asilimia 16.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wa maswali umekwisha. Kama kawaida kuna matangazo. Naanza na wageni. Leo Waheshimiwa

Wabunge wageni wetu ni kama wafuatao: Kwanza, wageni wa Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana – Mheshimiwa Prof. Juma Kapuya na Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa pamoja. Ni wageni 18 wakiongozwa na Dr. D. N. Komba, Katibu Mkuu wa Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana na Ndugu William Erio Mkurugenzi Mkuu wa PPF. Sijui wako wapi? Ahsante sana na karibuni sana.

Wapo pia wageni wa Mheshimiwa Chiza na Mheshimiwa Genzabuke nao ni Ndugu Genofeva Bisama - Diwani (Viti Maalum) nadhani kutoka Wilaya ya Kibondo. Ahsante sana. Karibu sana Mheshimiwa Diwani. Pia yupo ndugu William Simbagie, yule pale! Safi sana! Huyu hakutamkwa cheo chake wala uhusiano na hawa Waheshimiwa.

Wapo pia wageni wa Mheshimiwa Balozi Seif Idd, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ni Wenyeviti wanne wa Mashina wa Jimbo la Kitope Zanzibar. Wageni wetu kutoka Zanzibar Jimbo la Kitope karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wanafunzi 50 na walimu wanne wa Shule ya *Saint John Primary School* Tanga. Wale pale na walimu wao, ahsanteni sana. Hawa vijana ni nadhifu kabisa. Tunawaomba msome kwa bidii nchi inawahitaji katika fani mbalimbali. Ahsante sana walimu kwa kuwaleta vijana wajionee wenyewe tangu awali jinsi Bunge linavyofanya kazi. Karibuni na safari njema mnaporejea Tanga na masomo mema. Wapo wanachama 20 wa Taasisi ya *TASODASE* ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Omar Kwaangw' - Mwenyekiti Kamati ya Huduma za Jamii, ameniomba nitangaze kuwepo kwa Kikao cha Kamati ya Huduma za Jamii leo tarehe 10 Aprili, 2008 ukumbi Na. 219 mara baada ya matangazo haya. Iliandikwa saa 4.30, kwa hiyo Kamati ya Huduma za Jamii mara baada ya matangazo haya mnahitajika.

Mheshimiwa Mussa Zungu - Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ameniomba niwatangazie kwamba leo saa 5.00 asubuhi katika ukumbi 428 kutakuwa na kikao kifupi cha Kamati hiyo ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Jenista Mhagama - Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii ameniomba nitangaze kwamba kutakuwa na Kikao cha Kamati hiyo ya Maendeleo ya Jamii saa 5.00 asubuhi katika ukumbi Na. 231. Kwa hiyo, leo saa 5.00 ukumbi namba 231 Kamati ya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa William Shellukindo - Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, ameniomba nitangaze kwamba leo saa 7.00 mchana kutakuwa na Mkutano wa Kamati ya Nishati na Madini ukumbi na. 427, jengo la Utawala ghorofa ya nne.

Waheshimiwa Wabunge, katika matangazo mengine, napenda kutangaza kwamba zoezi la kuwa na kanuni zetu rasmi katika kitabu kimoja sasa ni tayari. Naomba kwanza zigawiwe, hii ndiyo sura ya Kanuni za Bunge Toleo la 2007 likiwa limekamilishwa pamoja na nyongeza zote. Mtaona liko katika rangi tulivu kidogo, iliyo rasmi na ndiyo nitakuwa naitumia, ni hii hapa na ndiyo itatuongoza katika kipindi chote kijacho. Kwa

hiyo, wahudumu naomba muwagawie Waheshimiwa Wabunge kila mmoja aweze kupata nakala yake na ufafanuzi kidogo kuhusu kipindi cha maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Waheshimiwa Wabunge, leo kati ya Waheshimiwa 24 walioomba kuuliza maswali, imewezekana kuwapatia nafasi tisa tu. Ni dhahiri kanuni hii itabidi tuibadilishe ili kipindi hiki kiwe ni cha saa moja kwa sababu kina faida sana. Namhurumia Mheshimiwa Waziri Mkuu, sijui atakuwa anasimama hapo saa nzima! Lakini ndiyo kazi yenyewe! “Ukipikia kuni usiogope moshi.”

Kwa hiyo, tangazo ni hivi, haitawezekana kutumia orodha hii siku inayofuata au Alhamisi inayofuata. Hatuwezi! Kwa sababu kwanza inawezekana aliyejaza Alhamisi hii, Alhamisi ijayo akawa hayupo. Kwa hiyo, kutakuwa na usumbufu ambapo pengine hawapo na pili, kama umeachwa na swali na kweli ni la haraka, Serikali ipo. Una siku saba nzima za kuendelea kujaribu kupata jibu kwa Waziri Mkuu mwenyewe, Waziri wa Nchi, Mambo ya Bunge na Waheshimiwa Mawaziri.

Kwa hiyo, ndiyo maana hatuwezi kuitumia orodha hii iwe ndiyo orodha ya Alhamisi ijayo. Kwa hiyo, siku ikifika, utaratibu ni kwamba, siku ya Alhamisi asubuhi wale wanaotaka kuuliza maswali kabla ya saa 2.30 basi wanamwarifu Katibu na hii orodha ndiyo inamwongoza yeyote atakayekuwa *Presiding Officer* hapa.

La mwisho, Waheshimiwa Wabunge nimearifwa kwamba Muswada unaofuata, kama kawaida kwenye *Order Paper* unapona Muswada huwa tunapenda tuanze kuona majina ya wachangiaji. Kwa hiyo, Muswada unaofuata wa Sheria ya Mikopo ya Ukodishaji Raslimali (*Financial Leasing*) bado nafasi tele yeyote ambaye anataka kuchangia ajaze fomu au aandike jina lake ili tuweze kulichambua. Ahsante sana.

MHE. HAFIDH ALI TAHIR: Mwongozo wa Spika!

SPIKA: Mwongozo wa Spika.

MHE. HAFIDH ALI TAHIR: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nipate mwongozo kutoka kwako na kwenye kiti chako na nina maelezo mafupi kabla sijaomba huu mwongozo wenyewe.

Mheshimiwa Spika, ninavyofahamu Bunge la Jamhuri ya Muungano ni chombo muhimu sana na ni chombo cha Kitaifa kinachothaminiwa na Watanzania kwa ujumla. Lakini Serikali ndani ya Bunge hili limetuletea Wizara mbalimbali zinazohusiana na utendaji mzima wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na yale yaliyotendwa na Wizara hizo nadhani itakuwa ni sahihi na yamefanyiwa utafiti wa kina ili Watanzania wasipotoshwe.

Mheshimiwa Spika, tulipoingia katika kikao hiki cha Kumi na Moja kwenye *pigeon holes* zetu tulikuta *disc* hii inayozungumzia utalii katika Tanzania. *Disc* hii ukiiangalia na wale wenzangu ambao tayari wameshaiangalia, kuna mama mmoja hapa

anafanya *comments* katika mambo yanayohusiana katika *disc* hii. Lakini *introduction* yake anaisifu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasema kwamba Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilipatikana baada ya Tanganyika kujitawala katika uhuru mwaka 1961. Halafu hapo anarudia kwamba Zanzibar walipata uhuru mwaka 1963 na hatimaye Zanzibar na Tanganyika wakaungana Aprili 26. Akasimamia hapo.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema hapa, Wizara zinapofanya vitu kama hivyo, wawe waangalifu sana katika kuangalia hali halisi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kabla hawajatuletea *documents* hizi ndani ya Bunge hili Waziri, Naibu Waziri na watendaji wake wawe wana hakika kinacholetwa ni hicho na hakipotoshi ukweli wa Jamhuri hii ya Muungano wa Tanzania. Zanzibar haikuungana na Tanganyika baada ya uhuru wa mwaka 1963. Sio sahihi! Sio kweli kwamba baada ya uhuru wa mwaka 1963 na uhuru wa mwaka 1961 ndiyo ikapatikana Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni upotoshaji mkubwa!

Tanganyika imeungana na Zanzibar baada ya Mapinduzi ya tarehe 12 Januari. Sasa zinapotawanywa *cassettes* kama hizi katika Bunge kubwa kama hili kwa kweli halitusaidii na haliwasaidii Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nini kinachotokea sasa hivi? Kinachotokea sasa hivi, Wapinzani hasa *CUF* wanazitafuta sana hizo *CD* na kuna Waheshimiwa Wabunge tayari humu wameshaombwa wanazitafuta kwa sababu kile kitendo cha kusema uhuru mwaka 1963 wa Zanzibar wao ndiyo kinachowavutia na wanataka kujulisha ulimwengu kwamba hata huko Tanzania kwenyewe wanasema kwamba uhuru wa mwaka 1963 ndio uliungana na Tanganyika mwaka 1961.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako kwamba Wizara ilituletea *disc* hii na haikufanya sahihi na kwamba *disc* hizi ikiwezekana zikusanywe tena na zikafanyiwe ukarabati na zieleze Muungano wa Tanzania ulipatikana vipi kwenye *disc* hii ya utalii. Huo ni mwongozo wa kwanza.

Mheshimiwa Spika, pili, ulipokuwa unazungumzia habari ya masuala ya Waziri Mkuu...

SPIKA: Mheshimiwa siwezi kukuruhusu ukaendelea tu kunafuta miongozo ya masuala mbalimbali ambayo yanakusibu. Kwa hiyo, nitatoa mwongozo kuhusu hilo moja kuhusu utaratibu.

Mwongozo kuhusu suala moja mahsusi kama ulivyolieleza, nitamwomba Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kesho na nitampa nafasi na natoa ombi hili kupitia kwa Waziri Mkuu ili Serikali iweze kusema jambo kuhusu hilo alilolisema Mheshimiwa Hafidh. Sio sahihi kwa Mheshimiwa Spika kujiingiza kutoa jibu kuhusu makala ambayo haikutoka Ofisi ya Spika. Sisi tulisaidia tu mawasiliano, basi ili ziwafikie Waheshimiwa Wabunge. Sasa ni juu ya Serikali kuona kama inaweza kusema nini kuhusu hilo.

Kwa hiyo, kwa kuwa kesho ni Ijumaa na sio vizuri jambo hili likakaa hadi wiki ijayo, kupitia kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba Wizara ya Maliasili itusaidie kidogo maelezo ya ufafanuzi na hilo litakuwa limesaidia kujibu hoja ya Mheshimiwa Hafidh. Ahsante sana.

MHE. HASSAN RAJAB KHATIB: Mheshimiwa Spika, nimekuletea utoe tangazo muhimu sana lakini ninafikiri ulisahau kidogo.

SPIKA: Ooh ndiyo, ndiyo nitalitoa.

MHE. BENSON M. MPESYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu, ninaomba mwongozo wako kanuni 38(1) inatueleza kwamba tutawasilisha kabla ya saa 2.30 kwenye Ofisi ya Katibu ya Spika. Lakini kilichojitokeza leo asubuhi wakati Waheshimiwa wanapeleka majina tukaambiwa majina yaliwasilishwa toka jana jioni. Kwa hiyo, wale ambao tulizingatia kanuni hatukupewa fursa ya kuweza kuuliza leo. Sasa tunaomba mwongozo wako, majina yanatakiwa yaletwe siku moja kabla au siku hiyo ya asubuhi?

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mwongozo kuhusu maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu unatamka wazi kabisa kwamba maswali yanahitajika katika ule mwongozo wenyewe chini ya kanuni 38(4). Nitasoma.

“Wabunge wanaotaka kumwuliza Waziri Mkuu swali wakati wa kipindi cha maswali cha Waziri Mkuu watawasilisha majina yao kwa Katibu kabla ya saa 2.30 asubuhi siku hiyo na maswali kwa Waziri Mkuu.”

Kwa hiyo, hapo utendaji ulikosewa, hayapokelewi muda wowote tu, mradi unasema kabla ya saa 2.30 asubuhi, ukasema leo mathalan kwa kuwa ni Alhamisi ijayo na kwa sababu hata leo ni kabla ya saa 2.30 ya Alhamisi inayofuata, ukasema unawahi, ukayapeleka leo, haiwezekani! Maswali haya yanatakiwa yawe ya papo kwa papo. Kwa hiyo, umekaa umetafakari jambo ukasema hapana, hili nimwulize Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Kwa hiyo, mwongozo wangu ni kwamba tufuate fasili ya pili ya mwongozo huu uliosambazwa, ya Waheshimiwa Wabunge wote kwamba ni siku hiyo hiyo na tafsiri yangu ya ofisi maana yake sio kumfuata ofisini, hakuna urasimu wa namna hiyo. Watumishi wote walioko kwenye ofisi, hawa mnaowaona unaweza ukamkabidhi hata pale njiani inatosha. Kwangu mimi hilo limetimia. Sio lazima uende kujipanga ofisini ili kuweza kukabidhi jina lako. Utakapowaona hawa ambao wote mnawafahamu, basi umekabidhi iwe ni saa 1.00 asubuhi, saa 2.00, 2.15, 2.25, 2.29, 2.30 siku hiyo hiyo ya Alhamisi. Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge kutakuwa na Mkutano wa dharura wa Kamati ya Uongozi wa Umoja wa Bunge wa Chama cha Mapinduzi. Sio Kamati ya Uongozi (*Steering Committee*) hapana, Kamati ya Uongozi ya Wabunge wa Chama cha

Mapinduzi, leo saa 6.00 katika ukumbi wetu wa kawaida, ni cha dharura. Nashukuru sana kwa kunikumbusha hilo, ahsante.

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Mikopo ya Ukodishaji Raslimali wa Mwaka 2007 [(The Financial Leasing Bill, 2007)]

(Kusomwa Mara ya Pili)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Mikopo inayotolewa kwa njia ya Ukodishaji Raslimali (*Financial Leasing Act,*) 2007 pamoja na marekebisho yake sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kutoa shukrani zangu za dhiti kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda - Mbunge wa Handeni kwa kuujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri wakati Kamati ilipokutana mjini Dar es Salaam, tarehe 25 Januari, 2008. Nawashukuru pia Waheshimiwa Wabunge wote waliotoa michango yao wakati wakichangia katika Semina ya Waheshimiwa Wabunge iliyoandaliwa na Wizara ya Fedha siku ya Jumamosi, tarehe 2 Februari, 2008 hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba tumezingatia michango ya Kamati ya Fedha na Uchumi na michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge wengine wakati wa semina hiyo na tutaendelea kuifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Fedha imeshuhudia mabadiliko makubwa katika kipindi cha zaidi ya miaka 15 sasa na mabadiliko yaliyofanyika yamechangia kwa kiasi kikubwa katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini. Mabadiliko ambayo yametokelezwa na Serikali katika kipindi cha kuanzia mwaka 1991 ni pamoja na kupitishwa kwa Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha Sura Na. 342, Sheria ya Benki Kuu Sura Na.197 na Sheria ya Masoko na Dhamana Sura Na.79.

Mheshimiwa Spika, sheria hizi zimechangia kwa kiasi kikubwa, maendeleo yaliyokwishapatikana katika Sekta ya Fedha na hivyo kuwezesha sekta hii kutoa mchango katika kukuza uchumi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua zilizochukuliwa na Serikali upatikanaji wa mikopo ya muda mrefu na ya kati umekuwa mgumu kutokana na Mabenki na Taasisi za fedha kuweka sharti la kuwepo kwa dhamana wakati wa kutoa mikopo hiyo na hivyo kusababisha wananchi kushindwa kupata mikopo ambayo pamoja na kuwawezesha kujiongezea kipato na maisha bora mikopo hii ingekuwa chachu katika kukuza uchumi na pato la Taifa.

Tathmini iliyofanywa na Benki Kuu ikishirikiana na Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa mwaka 2003 ilibainisha kwamba Sekta ya Fedha inahitaji marekebisha zaidi ili kuweka mazingira ya kuwawezesha wajasiriamali wananchi kunufaika na huduma za kifedha zinazotolewa na Mabenki na Taasisi za fedha na hatimaye kuchangia katika kukuza uchumi na kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, utafiti huo vile vile ulibainisha umuhimu wa kuweka utaratibu wa kisheria utakaowezesha wananchi kupata huduma mbalimbali za kifedha ikiwa ni pamoja na utaratibu wa mikopo itakayotolewa kwa njia ya ukodishaji wa rasilimali, yaani karadha ya fedha.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unakusudia kuweka utaratibu wa kisheria utakaoisukuma Sekta ya Fedha kutoa mikopo kwa wananchi na wawekezaji wa ndani walio wengi kwa njia ya ukodishaji rasilimali katika sekta ya uzalishaji na hivyo kuchochea uwekezaji mitaji nchini ili kukuza pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, mambo muhimu yaliyozingatiwa katika Muswada huu ni kama ifuatavyo:-

Kwanza utaratibu wa ukodishaji wa rasilimali unahusisha pande tatu. Yaani mkopesaji au mkodishwaji na muuzaji au mzalishaji bidhaa. Hata hivyo mkataba kwa ajili ya ukodishaji rasilimali unahusisha pande mbili, yaani taasisi inayotoa mkopo na mkopaji au mkodishwaji.

Pili, jukumu la kuchangia rasilimali kwa ajili ya kukodisha litakuwa ni la mtu au taasisi inayofaidika na mkopo. Kampuni inayouza rasilimali au bidhaa itawajibika kuthibitisha ubora wa rasilimali au bidhaa husika kwa ajili ya matumizi yanayokusudiwa na hivyo kuifanya taasisi inayotoa fedha kulipia rasilimali hiyo kutohusishwa na rasilimali hiyo endapo hitilafu za kiufundi na nyinginezo zitakapojitokeza. Taasisi inayotoa mkopo itakuwa na haki ya kuchukua rasilimali iliyokodishwa endapo mkodishwaji atashindwa kutekeleza masharti ya mkopo katika kipindi kilichokubaliwa.

Aidha, endapo mkodishwaji atafariki au atafilisika, mkodishwaji atakuwa na haki ya kuchukua rasilimali iliyokodishwa kwa Marehemu au kwa mtu aliyefilisika au taasisi iliyofilisika na mkodishwaji huyo atapaswa kulipa malipo yote ya gharama za ukodishaji yaliyosalia kwa kipindi cha mkataba kilichobaki endapo mkataba wa ukodishaji utakuwa haujabainisha taratibu nyingine kuhusu malipo haya.

Tatu, mkopaji atawajibika kufanyia matengenezo rasilimali husika katika mkataba wa mkopo kutokana na uharibifu utakaosababishwa na watu wasiohusika na mkataba huo.

Nne, mkodishwaji hapaswi kutumia rasilimali inayohusika katika mkataba wa mkopo kwa njia ya ukodishaji kuweka rehani kwa ajili kupata mkopo mwingine.

Tano, Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atakuwa na mamlaka ya kuteua Masjala itakayohusika na uandikishaji wa rasilimali zinazohusika na mikataba ya mikopo kwa njia ya ukodishaji kwa njia ya Tanzania Bara na kwa upande wa Zanzibar, Waziri wa Fedha na Uchumi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar atateua Masjala husika.

Aidha, Masjala hii itaruhusu wananchi kufanya upekuzi. Hatua hii itasaidia kudhibiti rasilimali zilizokopeshwa kwa utaratibu wa ukodishwaji wa rasilimali kuwekwa rehani kwa ajili ya mikopo mingine na wakopaji wasio waaaminifu.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu sita ambazo kwa ujumla wake na kwa pamoja zinatujengea maudhui ya Muswada wenyewe.

Sehemu ya kwanza yenye Ibara ya kwanza hadi ya tatu, inahusu masuala ya utangulizi kama vile jina la sheria, matumizi ya sheria ambayo itatumika katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na tafsiri ya maneno mbalimbali.

Sehemu ya Pili yenye Ibara ya nne hadi tisa inabainisha utaratibu wa kuingia mikataba ya ukodishaji rasilimali ambapo kanuni zinazotawala katika kuingia mikataba kwa mfano umri unaoruhusiwa kisheria zitazingatiwa kama zilivyobainishwa chini ya sheria za mikataba zinazotumika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Aidha, sehemu hii inaweka utaratibu wa misingi inayohusu vifaa vinavyoweza kutumika kwa ajili ya mikataba ya mikopo kwa ajili ya ukodishaji rasilimali na utaratibu wa malipo ya gharama za ukodishaji.

Sehemu ya Tatu yenye ibara ya kumi hadi ya kumi na tatu kama ilivyorekebishwa inaainisha haki na majukumu ya mkodishaji, mkodishwaji na taasisi inayouza rasilimali husika ambapo kifungu cha awali cha kumi kimefutwa kwa kuwa maelezo yaliyopo katika kifungu cha nne cha Miswada yanakidhi dhana halisi ya utaratibu wa kuingia mikataba ya ukodishaji.

Mheshimiwa Spika, aidha, sehemu hii inabainisha taratibu za mgawanyo wa madhara yanayoweza kujitokeza kwa wahusika kutotimiza wajibu wao kisheria ambapo mkodishaji wa rasilimali iliyokodishwa katika Mkataba wa mkopo atakuwa na haki ya kudai kurejeshewa rasilimali iliyokodishwa endapo mkodishwaji atashindwa kutimiza masharti ya mkataba ikiwa ni pamoja na kutolipa malipo ya ukodishaji.

Sehemu ya nne yenye ibara ya kumi na nne hadi ishirini inabainisha yafuatayo:-

Kwanza, mkodishaji anaweza kuhamishia kwa mtu mwingine haki na wajibu wake chini ya mkataba wa ukodishaji baada ya kutoa taarifa kimaandishi kwa mkodishwaji. Aidha, mkodishaji anaweza pia kuhamishia haki ya kupokea haki ya malipo ya ukodishaji kwa mtu mwingine pasipo kuhitaji ridhaa ya mkodishwaji.

Pili, mkodishwaji atawajibika kufanya matengenezo ya rasilimali aliyokodishwa kutokana na madhara yatokanayo na watu au taasisi zisizohusika moja kwa moja na mkataba.

Tatu, mkodishwaji ana haki ya kudai kurejeshewa gharama kutoka kwa mtu asiyehusika na mktaba wa ukodishaji aliyesababisha uharibifu kwa rasilimali iliyokodishwa. Aidha, sehemu hii inabainisha kwamba mkodishwaji hapaswi kutumia rasilimali iliyokodishwa kuweka rehani kwa ajili ya kupata mkopo kutoka kwa wakopeshaji wengine.

Sehemu ya tano, inahusu ibara ya ishirini na moja ambayo Waziri mwenye dhamana ya fedha katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atakuwa na mamlaka ya kuteua Masjala itakayohusika na uandikishwaji wa rasilimali zinazohusika na mikataba ya mikopo kwa njia ya ukodishaji rasilimali kwa upande wa Tanzania Bara na kwa upande wa Tanzania Zanzibar Waziri wa Fedha na Uchumi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar atateua Masjala husika. Aidha, Masjala hii itaruhusu wananchi kufanya upekuzi. Hatua hii itasaidia kudhibiti ukodishaji wa kuweka rehani kwa ajili ya mikopo mingine na wakopaji wasio waaminifu.

Sehemu ya Sita na ya mwisho yenye ibara ya ishirini na mbili hadi ishirini na sita, inahusu mambo yafuatayo:-

Kwanza, inampa mamlaka Waziri anayesimamia sheria hii kutunga kanuni kuwezesha utekelezaji wa Sheria hii;

Pili, inawapa uwezo wahusika katika mikataba ya mikopo kwa njia ya ukodishaji rasilimali kubadili mambo yanayoashiria uvunjaji wa masharti ya mkataba; na

Tatu, inaweka misingi ya kisheria kuhusu kiwango cha fidia kwa mkopeshaji au mkopeshwaji panapotokea ukiukwaji wa masharti ya mkataba wa ukodishaji.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo awali na pia kutokana na mifano halisi iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge katika Semina ya Wabunge endapo Muswada huu utapitishwa kuwa Sheria, wananchi watakaokopa watapata fursa nyingine ya kuwawezesha kuinua vipato vyao, kuboresha maisha yao na kwa ujumla kuchangia katika kukua kwa uchumi na pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, naomba Waheshimiwa Wabunge waujadili Muswada huu na baadaye nitaomba Bunge liweze kupitisha ili hatimaye kwa kadri itakavyokuwa imempendeza Mheshimiwa Rais akiutia saine, basi uwe sheria.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MHE. ABDALLAH O. KIGODA – MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili nitoe maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi baada ya kumaliza kazi ya kuchambua na kujadili Muswada wa Mikopo inayotolewa kwa njia ya Ukodishaji Rasilimali wa Mwaka 2007 (*Financial Leasing Bill, 2007*) kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Bunge toleo la mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako, naomba nitumie fursa hii kwa dhati kabisa kuwashukuru Wabunge wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwa kunipa heshima kubwa ya kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwa mara ya pili hadi hatima ya kipindi cha Bunge lako hii Tukufu. Nafasi hii tutaitumia kwa juhudi kubwa kupitia dhana ya *contractive criticism* kwa maslahi ya Bunge letu na Taifa yetu kwa ujumla. Tutaendelea kuishauri Serikali yetu kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kabla ya Mkutano wa Kumi, Kamati ya Fedha na Uchumi ilikuwa na jukumu la kuchambua na kupitia Muswada wa Mikopo kwa njia ya Ukodishaji wa Rasimali (*Financial Leasing Bill, 2007*). Ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati ilitokeleza jukumu hilo na hatimaye Muswada huu kuletwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, katika hatua za kuchambua na kuupitia Muswada wa Karadha ya Fedha, Kamati ilishirikiana vyema na Wizara ya Fedha, Wataalam kutoka Benki Kuu, Wanasheria kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na Wadau wengine wa fedha. Katika hatua za kuupitia Muswada huo, Wizara ya Fedha kupitia Benki Kuu ya Tanzania, iliandaa semina maalum kwa ajili ya Kamati iliyofanyika Jijini Dar es salaam tarehe 24 Januari, 2008. Aidha, Wizara ya Fedha iliandaa Semina nyingine kwa Wabunge wote kuhusu Karadha ya Fedha ambayo ilifanyika tarehe 2 Februari, 2008 hapa Dodoma. Semina hiyo ilitoa elimu kubwa kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki tunashuhudia maendeleo na mageuzi makubwa katika Sekta ya Fedha hapa nchini pamoja na maendeleo ya kiuchumi ambayo yanahitaji uwepo wa sheria itakayosaidia kumrahisishia mjasiriamali wa kati na wa chini kufaidika na mageuzi hayo.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika kwamba katika mchakato wa uzalishaji mali, wananchi wanategemea nyenzo tatu za uzalishaji: Nguvu kazi (*labour*), ardhi (*land*) na mtaji (*capital*). Teknolojia na juhudi ni vionjo mahsusi vya ziada. Hali ilivyo sasa, wengi wa wananchi wanakosa mitaji na hivyo kuathiri uwezo wao wa kujiajiri na kupata mapato. Aidha, pamoja na jitihada za Serikali za kisera na utekelezaji, bado hazijawalenga wengi wa wananchi hawa wa kipato cha chini hasa katika upatikanaji wa mikopo kutokana na kutokuweza kutimiza masharti yanayowekwa hususan lile la kuwa na dhamana inayothaminika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukuaji na uwingi wa vyombo vya fedha hapa nchini, Kamati inaona kwamba bado mwananchi ama mjasiriamali mdogo na wa kati hajawezeshwa vya kutosha katika kurahisishiwa mchakato mzima wa upatikanaji wa

mikopo ambayo ndiyo mitaji ya uwekezaji, hususan yule anaojishughulisha na Sekta ya Kilimo. Ikumbukwe kuwa sekta binafsi hasa wajasiriamali wadogo na wa kati ndio wenye mchango mkubwa katika uwekezaji wa mitaji na ukuzaji wa uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida mikopo ya Benki ama taasisi za fedha imekuwa na masharti yanayomtaka mkopaji kuwa na dhamana ama ya nyumba au ardhi, jambo ambalo limekuwa gumu kwa mjasiriamali wa kati na wa chini kutokana na kutokuwa na dhamana kama hizo.

Kwa kuwa, masharti ya kupata mkopo kwa njia ya ukodishaji rasilimali yanamtaka mteja kulipa sehemu tu ya gharama ya bidhaa au kifaa anachohitaji na kisha kwa mujibu wa mkataba atakaoingia na Benki au Kampuni ya Karadha atatakiwa kutoa marejesho kidogo kidogo kwa muda utakaopangwa, lakini wakati huo akitumia kifaa au bidhaa aliyokopa kuzalishia na kisha akimaliza marejesho anakuwa na uwezo wa kumiliki kifaa au bidhaa hiyo, basi ni dhahiri kuwa utaratibu huu ni ukombozi hasa kwa wananchi wa kipato cha chini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuridhiwa kwa Muswada huu haraka ili kuondoa upungufu wa kukosekana kwa sheria ya Mikopo kwa njia ya Ukodishaji Rasilimali ambapo matokeo yake Benki zinazotoa huduma za karadha ya fedha zinalazimika kutumia au kuazima sheria nyingine ili kuhalalisha shughuli za mikopo ya aina hii. Kwa mfano, sheria ambayo imekuwa inatumiwa ni pamoja na sheria ya mikataba (*Contract Law*).

Aidha, matumizi ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la thamani (*VAT*) katika utoaji wa karadha inaonekana kutokuwa wazi katika kutenganisha aina tofauti za karadha, hivyo kufanya wakopaji chini ya karadha ya uwekezaji kulipa kodi sawa na wakodishaji wa karadha ambapo matokeo yake ni kuwafanya wawekezaji kuwa kundi moja na walaji.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati ni kwamba, kuwepo kwa sheria ya Karadha ya Fedha kutasaidia kurahisisha na kuhamasisha uwekezaji mkubwa katika taasisi za fedha na hivyo wajasiriamali wadogo na wa kati kuwa na fursa kubwa ya kupata mikopo ya rasilimali na hivyo kuinua uzalishaji nchini ambao hatimaye utakomboa wananchi walio wengi kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliweza kuchambua Muswada wa Mikopo kwa njia ya ukodishaji rasilimali na kutoa maoni na ushauri mbali mbali kwa Serikali kama ifuatavyo:-

(i) Kamati inaishauri Serikali kuwa makini na kutokuharibu utaratibu huu mzuri kwa kuondoa urasimu hasa ikizingatiwa kuwa zitatumika nyaraka mbalimbali kabla ya wajasiriamali kupata mikopo hiyo.

(ii) Kamati inaishauri Serikali kutoruhusu utaratibu huu udhoofishwe na tatizo la ujenzi wa tabaka la soko (*market stratification*) na tabaka la wateja (*customer*

stratification) hasa ikizingatiwa kuwa walengwa ni wajasiriamali, wataalamu, wafanyabiashara na wenye viwanda. Kwa mfano, hadi mwaka 2006, takriban Dola za Marekani milioni 44.9 zimetumika kama karadha ikijumuisha Sekta ya Ujenzi asilimia 20, usafiri asilimia 77 na vifaa vya uzalishaji asilimia tatu tu.

Ni vyema walengwa wengi wawe ni wale wanaokwazwa na utaratibu wa sasa wa kupata mikopo kutoka Benki. Benki ya *STANBIC* kwa utaratibu huu wa karadha imeishatoa asilimia 20 kwa biashara kubwa, asilimia 70 kwa wateja wa kati na wateja wadogo (wajasiriamali) asilimia 10.

(iii) Kwa kuwa taasisi nyingi za fedha ziko mijini, Kamati inashauri Benki na kampuni za karadha ziweke mkakati madhubuti wa kuwalenga wananchi wa vijijini ambao ndiyo wazalishaji wakubwa katika Sekta ya Kilimo. Aidha, vifaa kama matrekta ni vyema vikachukuliwa kama zana za uzalishaji badala ya zana za usafiri ili kuwapa wakulima muda wa kutosha wa kulipia zana hizo.

(iv) Kamati inashauri na kusesitiza kuwa riba katika malipo yatakayorejeshwa iwe ya chini kuliko inayotolewa na Benki na taasisi nyingine zinazotoa mikopo ya kawaida. Kamati inaipa changamoto Benki Kuu kushughulikia eneo hili.

(v) Kamati inashauri kuwa, elimu kuhusu karadha ya fedha itolewe kwa upana zaidi, kwa lugha rahisi na iwafikie wananchi wengi hasa huko vijijini.

Waheshimiwa Wabunge, eneo hili pia tulichukulie kama changamoto kwetu.

(vi) Mikataba ya Mikopo kwa njia ya ukodishaji rasilimali kati ya Benki au Kampuni ya Karadha na Mjasiriamali hasa anayewekeza katika kilimo, haina budi kuzingatia kuwa mkulima anazalisha kwa msimu. Hivyo, masharti ya mikopo ya rasilimali yaendane na hali halisi ya uzalishaji wa kilimo.

(vii) Kwa vile Muswada huu unaingiliana na Sheria nyingine za kodi, mabadiliko muhimu katika mfumo wa sheria na kodi ni hatua ya lazima. Mabadiliko hayo ni lazima yawasaidie na kuwanufaisha wajasiriamali. Kwa mfano, maeneo yote yanayohusu kodi ya *VAT* katika biashara ya karadha ya fedha yaainishwe.

(viii) Serikali iandae mazingira ya kuwarahisishia wawekezaji wa karadha ya fedha, usalama wa mitaji yao ikiwa ni pamoja na kuangalia sheria zile zinazompa haki mteja kushitaki Mahakamani na hivyo kusimamisha shughuli (*court injunction*) za kampuni husika huku ikiendelea kufuatilia kesi.

(ix) Kwa tahadhari kubwa, ipo dhana inayoshehereshwa kwamba hivi sasa mfumo wa uchumi wetu umebadilika na kupata sura mpya kwa maana ya kwamba sekta zetu za asili kama vile hazichangii zaidi katika pato letu la Taifa na badala yake sekta nyingine kama vile madini na utalii ndizo zilizoboreka na kutoa mchango mkubwa katika pato la Taifa.

Dhana hii sio sahihi ya kuthibitisha kuwa mfumo wa uchumi wetu umebadilika. Hii ni kwa sababu na ni dhahiri kuwa bado hatujaibua na kutumia fursa zote katika kilimo licha ya mipango na rasilimali nyingine ziendezo kati sekta hii. Kwa mfano, chini ya programu ya *ASDP* na kadhalika. Kwa hiyo basi, Kamati yangu inaishauri Serikali kwamba utaratibu huu wa mikopo inayotolewa kwa njia ya ukodishaji rasilimali utoe kipaumbele mahususi katika utoaji wa vifaa na zana za kilimo ili tuondokane na matumizi ya zana duni katika kilimo yasiyoendeleza tija na ufanisi katika sekta hii isiyochangia ipasavyo hivi sasa katika pato letu la Taifa kwa vile tu hatujaibua uwezo uliopo. Tutakapofika kiwango cha kuibua fursa zote za kilimo ndipo tutakapoweza kusema kuwa mfumo wetu wa uchumi umebadilika na umechukua sura mpya, ama sivyo kusherehesha dhana hii hivi sasa ni kudhoofisha na kusahau mchango unaopaswa na dhahiri wa kilimo katika uchumi wetu unaochangia asilimia 75 ya Watanzania wengi vijijini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Fedha - Mheshimiwa Mustafa Mkullo pamoja na Manaibu wake. Aidha, Kamati inawashukuru Gavana na Manaibu Gavana pamoja na Watalaam mbalimbali wa Benki Kuu ambao wamewezesha Muswada huu kufikia hatua hii.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi ambao wameweza kutoa maoni na michango ya mawazo yao mbalimbali katika kuboresha Muswada huu ili hatimaye uletwe mbele ya Bunge hili Tukufu. Naomba nitumie nafasi hii kuwatambua Wajumbe wote ambao baadhi yao baada ya mabadiliko ya Kamati, wameteuliwa kuwa Wajumbe wa Kamati nyingine za Bunge pamoja na Mheshimiwa Adam Malima kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda - Mwenyekiti, Mheshimiwa Adam K. Malima - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Ania S. Chaurembo Mjumbe, Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni, Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, Mheshimiwa Parmoukh S. Hoogan, Mheshimiwa Eustace O. Katagira, Mheshimiwa Devota M. Likokola, Mheshimiwa Clemence B. Lyamba, Mheshimiwa Ledian M. Mng'ong'o, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Elisa D. Mollel, Mheshimiwa Kilontsi M. Mporogomyi, Mheshimiwa Felix C. Mrema, Mheshimiwa Omar S. Mussa, Mheshimiwa Victor K. Mwambalasa, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Dr. Omari Mzeru Nibuka, Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mheshimiwa Suleiman Ahmed Saddiq, Mheshimiwa Zubeir Kabwe Zitto na Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kutoa shukrani kwa Katibu wa Bunge Ndugu Damian S. L. Foka pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake. Aidha, napenda kuwashukuru Ndugu Anselm Mrema na Ndugu. Patson A. Sobha, Makatibu wa Kamati hii kwani sote kwa pamoja

tumeweza kukamilisha maandalizi ya Muswada huu wa Mikopo kwa njia ya Ukodishaji Rasilimali (Karadha ya Fedha) wa mwaka 2007 (*Financial Leasing Bill, 2007*).

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MHE. LUCY F. OWENYA – MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI:
Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa sheria ya Karadha ya Fedha ya mwaka 2007 (*Financial Leasing Act, 2007*) Kwa mujibu wa kanuni za Bunge toleo la 2007, kanuni ya 53(6) (c) na kanuni ya 86(6).

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa familia za wale wote waliofiwa na wazazi wao, watoto wao na wake zao.

Pia napenda kutoa pongezi zangu za dhiti kwa Mheshimiwa Mizengo Pinda kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Tanzania. Aidha, pongezi hizo ziende kwa wale wote walioteuliwa kushika nyazifa za Uwaziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa dhana nzima ya karadha za fedha ni ngeni au mpya kwa nchi yetu, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa pamoja na mikataba ya karadha kutofautiana, yaani mali zinazohitajiwa na wajasiriamali kama vile mashine za kusaga, matrekta, *pump* za kumwagilia mashambani, mitambo ya kuchimbia dhahabu na kadhalika, lakini kutokana na uelewa mdogo wa wananchi, ni vyema kukawa na “*standard agreement*” ambayo itatoa uelewa kwa wakopaji kama vile kulivyo na “*standard agreement*” kwenye kuuziana, au katika kuingia ubia katika Sekta ya Madini. Hii ni kutokana na upya wa dhana yenyewe hapa kwetu. Hivyo ni vyema hili likafanyiwa kazi. Kwa njia hii itasaidia sana kuepusha utapeli kutoka kwa baadhi ya watumishi katika vyombo vya fedha ambao sio waaminifu.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa katika sheria kuwepo na kipindi maalumu toka mwombaji anapomaliza taratibu zote zinazohitajika ambacho karadha ya fedha itatumia hadi mteja wake kupatiwa karadha yake ya uwekezaji. Hili ni muhimu sana katika kuondoa ukiritimba ambao unaweza kusababisha sheria hii kuonekana kama haiwanufaishi wajasiriamali.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 3(c) kinachohusiana na tafsiri ya maneno, neno “*asset*” kwenye tafsiri yake imekuwa ni pamoja na mali asili (*natural resources*), Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge lako Tukufu tafsiri ya neno *natural resources* katika Muswada huu linahusisha mambo gani, maana gani na linaishia wapi. Hii ni kutokana na ukweli kuwa Muswada huu haujatoa tafsiri yoyote juu ya maana ya neno “*natural resources*.”

Mheshimiwa Spika, Katika kifungu cha nne cha Muswada kinachozungumzia suala zima la Mkataba wa Karadha (*Financial Lease Agreement*) hakuna sehemu inayoonyesha kama kutakuwa na asilimia yoyote ya malipo ya awali (*security deposit in*

percentage). Lakini inaonyesha kuwa *leasee* ndiye atakuwa na jukumu la kuhakikisha kuwa gharama zote zinazohusiana na ufungashaji (*handling charges*) toka kwa mzalishaji hadi sehemu anayofanyia biashara anatoa yeye. Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri atupe ufafanuzi kuhusiana na suala hili.

Mheshimiwa Spika, mwomba karadha anaweza kuwa na ile asilimia inayohitajika ili apate karadha ya uwekezaji lakini akakosa fedha za kulipia ushuru wa kuendesha biashara ili aweze kulipa mkopo. Kwa kuwa katika Muswada huu wa sheria hakuna ufafanuzi wa hilo, Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi, ni vipi mkaradha ataweza kuendesha biashara bila ya mtaji wa kuendesha biashara, hasa ikizingatiwa kuwa lengo la sheria hii ni kuwasaidia wafanyabiashara au wajisiriamali wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 4(7) cha Muswada kinasomeka kuwa mwisho wa kipindi cha mkataba wa karadha na kwa kutegemea kukubali kwa *lessor*, *leasee* anaweza kununua *asset* vinginevyo anairudisha *asset* hiyo kwa *lessor*.

Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi kwa hili. Katika hali hii gharama ya kurudisha amana hiyo itakuwa juu ya nani?

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 11(1)(b) kinachosema kuwa *Leasor* hatawajibika na ubovu au mapungufu yoyote yatakayojitokeza kwenye mashine/bidhaa iliyo kwenye karadha. Kambi ya Upinzani inashauri kuwa shirika la Bima au masharti ya bima yaambatanishwe/yahusishwe na ununuzi ikiwa ni pamoja na *guarantee* ya muuzaji kwa vyombo vipya au hata vilivyokwishatumika.

Utaratibu huu utawahakikishia wajasiriamali uhakika wa amana hiyo hata pale patakapotokea makosa ambayo hayahusiani na utumiaji wao. Tumepata uzoefu kutoka mipango ya karadha iliyopita, hivyo tusirudie makosa hayo tena. Aidha, kifungu cha 11(2) kinachosema, nanukuu “*for defects in legal title to the leased asset shall not be limited by the agreement.*” Tunataka maelezo kuhusiana na kifungu hiki.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 11(6) kinachosema *Leasor* hatawajibika kwa *leasee* kutokana na uharibifu utakaotokea kwenye *asset* ila pale tu itakapokuwa imeelezwa katika sheria hii.

Kambi ya Upinzani inaona hapa hakuna haki, kwani katika sheria hii hakuna kifungu kinachoeleza aina ya uharibifu ambao *lessor* atawajibika nao, vinginevyo ni kiini macho tu, kwa kusema ila pale sheria itakapotaja aina ya uharibifu. Hivyo basi, tunaitaka Serikali ikiangalie upya kifungu hiki.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 12(1) kinachosema kuwa *supplier* wa bidhaa atamtaka *leasee* afanye majukumu yale yale kama *lessor* kuhakikisha ubora na uimara wa bidhaa kulingana na mkataba wa manunuzi (*supply agreement*). Kambi ya Upinzani inauliza ni kwanini *supplier* ampe majukumu *leasee* wakati mkataba ni kati yake na *lessor*? Jukumu hili litatekelezwa vipi wakati hakuna mkataba kati ya wawili hao?

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 12(3) kinachosema kuwa *leasee* anaweza moja kwa moja kumchukulia hatua za kisheria *supplier* kuhusiana na matatizo kwenye bidhaa za karadha (*material defects in the leased asset*). Pale pale kinasema: “*Supplier* hatowajibika kwa *lessor* au *leasee* kutokana na uharibifu huu.” Kambi ya Upinzani inaona hapa kuna utata. Tunaitaka Serikali itoe ufafanuzi kuhusiana na utata huo. Iwapo *supplier* yuko nje ya nchi kifungu hicho kitasimamiwa vipi wakati hakuna mkataba kati ya *supplier* na mkodishaji yaani *leasee*. Utata huu unatakiwa ufafanuliwe kwa kina iwapo tunataka sheria hii kufanya kazi. Maelezo katika kifungu cha 12(4) yanaleta utata mkubwa kwa kuwa *lessor* anatakiwa tu kumsaidia (*to assist*) lakini hana jukumu la kisheria kumsaidia mkodishaji yaani, *leasee*.

Mheshimiwa Spika, Katika kifungu 12(4) kinaongelea *privity of contract*, ni dhahiri kuwa *leasee* hana uwezo kisheria kuchukua hatua zozote za kisheria kwa *supplier*. Hivyo ni bora kifungu hicho cha 12(3) kikaondolewa kwani kinaongelea jambo ambalo haliwezekani kiutekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 23(1) bila maelezo yoyote kinatoa mamlaka kwa Gavana wa Benki Kuu kutengeneza Sheria ndogo ndogo *by-laws* kuhusiana na mikataba inayohusika na sheria hii. Kambi ya Upinzani inaona hapa kutakuwa na kuingiliana kwa majukumu kati ya Gavana na Waziri ambaye pia kifungu cha 23(1) kimempa majukumu ya kutengeneza Kanuni zitakazowezesha utekelezaji wa sheria hii. Kambi ya Upinzani haioni kwanini ghafla Gavana wa Benki Kuu ambaye hakuelezwa popote katika Sheria hii na wala majukumu yake kufafanuliwa apewe majukumu haya muhimu badala ya kuachiwa Waziri ambaye ndiye msimamizi mkuu kwa mujibu wa sheria hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

SPIKA: Mheshimiwa Lucy Owenya, asante sana kwa niaba ya Kambi ya Upinzani. Waheshimiwa Wabunge, ninao hapa wachangiaji watano, naona bora niwasome ili wajiandae. Wa kwanza, atakuwa Mheshimiwa Eustace Katagira, wa pili Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, wa tatu Mheshimiwa Castor Ligallama, wa nne Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia na wa tano, Mheshimiwa John M. Cheyo.

Kama nilivyosema, bado tu ipo nafasi kwa sababu tuna siku nzima hadi jioni kuweza kuzingatia Muswada huu. Kwa hiyo, bado nakaribisha majina. Kwa sura hiyo, sasa nitamwita msemaji wa kwanza Mheshimiwa Eustace Katagira, wakati huo Mheshimiwa Siraju kaboyonga ajiandae.

MHE. EUSTACE O. KATAGIRA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kufungua mjadala huu. Muswada huu ni muhimu sana, unaleta taratibu kati ya zile ambazo tumeziomba na kuzidai sana katika Kamati yetu ya Fedha. Utaratibu mwingine ambao tumekuwa tunauomba katika Kamati yetu ya Fedha sambamba na huu wa kukodisha ni utaratibu wa kuweza kuweka fursa ya kuwezesha wananchi waweze kupata *mortgage finances* za kuweza kujijengea nyumba. Nao bado tunaudai na

tunauomba na tunahimiza Serikali iweze kuandaa utaratibu wa namna hiyo. Lakini, tunafarijika kwamba sasa huu utaratibu wa kuweza kutoa mikopo ya ukodishaji wa vifaa unaletwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu utasaidia kuweza ku-*release* mitaji kwa wajasiriamali. Badala ya mitaji ile kutumika katika kununua vifaa, wataweza sasa kupata vifaa waweze kutumia kuendeleza biashara zao na uwekezaji wao ili waweze kuzalisha kwa uwezo mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, pia utaratibu huu utawezesha mwekezaji au mjasiriamali aweze kutumia vifaa ambavyo ni vya kisasa zaidi. Utaona kwamba katika utaratibu wa kawaida wa kununua vifaa vya kutumia katika biashara, katika shughuli za uzalishaji, mwekezaji anakuwa amenunua vifaa na anakaa na vifaa hivyo mpaka vinachakaa. Lakini sasa katika utaratibu huo wa ukodishaji ni kwamba, mwekezaji, mjasiriamali anaweza akakodisha vifaa, akatumia na jinsi teknolojia inavyobadilika kwa haraka, akaweza pia sasa kuacha kukodisha vifaa vile, akakodisha vifaa ambavyo ni vya kisasa zaidi. Fursa hii itampatia nafasi nzuri ya kuweza kuzalisha vizuri zaidi na kuweza kupata mapato na faida kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu utaweza kuwasaidia wajasiriamali katika nyanja nyingi sana na hasa katika nyanja ambazo tunasema *capital intensive*. Kwa mfano, katika nyanja ya kilimo, mimi nimekuwa ninaongea na marafiki zangu ambao wamesoma masuala ya kilimo na mara nyingi nimewalaumu na kusema kwamba, mbona ninyi hamtusaidii, mkawekeza na kuzalisha katika nyanja ya kilimo ambayo mmeisomea? Kwa nini hamlimi mashamba makubwa na nyie ni watalaam wa kilimo? Mbona wanasheria, wana makampuni ya sheria? Mbona sisi Wahasibu tuna makampuni ya Uhasibu? Kwa nini ninyi hamzalishi katika hii sekta? Lakini, kumbe matatizo yao ni makubwa zaidi kuliko ya kwetu.

Mheshimiwa Spika, Mwanasheria unaweza ukaenda na kalamu yako na akili yako, ukaanza kampuni ya Wanasheria na ukasonga mbele. Lakini, katika nyanja ya kilimo, unahitaji vifaa ghali kabisa, unahitaji matrekta, unahitaji ma-*harvesters*, unahitaji vifaa vya umwagiliaji. Kwa hiyo, haikuwa rahisi kwa marafiki zangu hawa kuweza kuwekeza katika nyanja ya kilimo. Lakini, sasa nina imani kwamba katika utaratibu huu ambao sheria hii inauleta, wataweza sasa vijana wetu na ndugu zetu kuwekeza katika nyanja ya kilimo kwa sababu wataweza kukopa matrekta, ma-*harvesters* na mtaji hautakuwa mgumu zaidi kama ilivyokuwa zamani.

Mheshimiwa Spika, lakini pia katika nyanja ya ujenzi, ndugu zetu wengi hasa wazawa wamekuwa wanatatizwa katika kupata vifaa vya ujenzi. Unakuta hata kule ndani kabisa ya nchi, unakuta watu wa nje ndio wanaotengeneza barabara, wanachimba malambo, ni kwa sababu watu wetu hawana vifaa vya kuweza kuchukua tenda za *construction*. Akitaka greda, anakwenda kuazima, akitaka kifaa cha kushindilia, mpaka aende kuazima au kukodisha. Lakini, sasa nina hakika kwamba wenzetu wazawa, Watanzania wa hapa hapa wataweza sasa kutumia fursa hii kupata vifaa vya kisasa zaidi, watapata vifaa kwa njia nafuu, kwa njia muafaka na wataweza sasa angalau kujikita katika shughuli za ujenzi za kiasi cha kawaida.

Mheshimiwa Spika, tukikumbuka kwamba hawa wajenzi wanaokuja kutoka nje ndio kweli wanasaidia katika *construction*, lakini pia faida inayopatikana wanai-*repatriate*, wanapeleka nje, inasaidia, lakini haisaidii sana uchumi wetu kwa sababu kila kinachozalishwa kile cha ziada inabidi kiende nje ukiondoa pesa zetu za kigeni, lakini pia, kiki-*weaken* hata shilingi yetu ya kitanzania kwa sababu kama wakipata hapa pesa ya kitanzania, inabidi waibadilishe, wa-*repatriate* pesa za kigeni.

Lakini pia katika uvuvi, wako vijana wetu kule Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, hawawezi kuwa na vifaa vyao vya uvuvi kwa sababu hawawezi kununua injini na mitumbwi mizuri. Lakini sasa kwa fursa hii, itawezekana kabisa vijana wetu hawa kujikita katika uvuvi kwa kujiajiri wao wenyewe, siyo mpaka atafute tajiri mkubwa, mtu wa nje awapatie injini au mitumwi halafu awasimamie na kuwapatia kile kidogo ambacho anataka kuwapatia. Sasa hivi wataweza wenyewe kupata fursa ya kupata vifaa vyao wenyewe na wakafanya biashara zao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, lakini pia katika usafirishaji, hivyo hivyo, siku hizi treni haifanyi kazi. Nyie wenyewe Waheshimiwa Wabunge mnaona barabarani, mnakutana na magari mengi sana yamebeba makontena. Lakini, nyingi ya kampuni hizi siyo kampuni za Watanzania kwa sababu magari makubwa kama ma-*scania*, ma-*lorry* makubwa hawawezi kuyapata. Kwa hiyo, fursa hii ambayo ingekuwa ni biashara nzuri kwa watu wetu, inachukuliwa na watu wa nje. Kwa hiyo, ni muhimu sasa wananchi wetu wakatambua fursa hii, wakapata magari makubwa, wakapata ma-*trailer* na ma-*semi-trailer*, wakaweza kupeleka mkono wao na kukamata fursa hii na biashara hii ya kuweza kusafirisha mizigo kutoka hapa kwenda ndani ya nchi na hata nchi za jirani.

Mheshimiwa Spika, hili pia ni kwa mashirika yetu sisi wenyewe, kwa mfano, Vyama vya Ushirika vinasafirisha mazao mengi sana, vinashindwa kupata vifaa vya kisasa hasa magari kwa kusafirisha mazao haya. Sasa Vyama vya Ushirika vinaweza pia kujikita katika kusafirisha mazao yao wenyewe. Pia wajasiriamali katika nyanja ya utalii ni muhimu sasa wanaweza kupata *fleets* za magari na vifaa vya kusafirisha watalii bila kutegemea wenyewe kuajiriwa na watu wa nje.

Mheshimiwa Spika, pia sheria hii ilivyotungwa na jinsi ilivyo na utaratibu ulivyo katika nchi nyingine zote, baada ya kutumia kifaa chochote, mkodishaji anakuwa na fursa ya kuweza kuchukua kifaa chenyewe ikawa mali yake.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoielezwa ni kwamba, kwa sasa ni vigumu kupata mikopo ya kibenki kwa watu wetu wa hapa hapa. Lakini, sheria hii inaweka mwanya wa kupunguza kutegemea hii mikopo ya kibenki ili kununua vifaa. Ilikuwa kwamba, uende benki, ukope pesa, ulipe riba ya juu sana, halafu hiyo pesa uende ukanunue vifaa vya kutumia na shughuli zote ngumu za kuweza kupata ile mikopo. Sasa hivi itakuwa rahisi kidogo kwa sababu ile sehemu ya vifaa utaweza kupata kwa utaratibu wa ukodishaji, itabakia ile sehemu ya mtaji wa kuendesha biashara ambayo unaweza sasa ukaenda benki kwa pesa kidogo zaidi.

Mheshimiwa Spika, ukikodisha vifaa vya kutumia katika shughuli yako ya biashara, inakupatia mwanya mzuri kwa wewe kufanya kile ambacho unakifahamu zaidi kuendesha ile biashara. Lakini, utakuta kama hujakodisha vifaa, tuseme ni *fleet* ya magari, maana yake katika kukodisha, inawezekana ukakodisha hata ile *maintenance* na *repair* ikawa inafanywa na yule aliyekodisha kile kifaa. Sasa kama ukimwachia yule mkodishaji akuletee kifaa, akiangalie uendeshaji wake, inakuwa ni rahisi kujikita katika ile shughuli yenyewe ambayo unaifahamu kuifanya zaidi na uzalishaji na faida itakuwa nzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, kila kitu huwa kinakuja na matatizo yake. Naomba kuiasa Serikali iangalie machache yafuatayo:- Suala la kwanza ni ile riba. Serikali ijitahidi kwamba shughuli hii ya ukodishaji wa vifaa na mitambo iweze kuja katika riba ndogo. Nina hakika kabisa na nafahamu kwamba Serikali hili inaliweza ingawa kila mara imetueleza kwamba hili ni gumu, ni nguvu ya soko. Lakini Serikali ina njia ambazo inaweza ikatumia hizi riba zikateremka, zikawa *affordable* kwa wakopaji wa vifaa hivi. Njia mojawapo ni ile ya Serikali yenyewe kuacha kutoa riba kubwa inapokopa katika Benki. Inapokopa katika Benki inalipa riba kubwa na riba hii inafanya Benki ziwapandishie wananchi riba ambayo zinawatoza kwa kulinganisha na zile riba anazopata kutoka katika ukopeshaji wa Serikali. Lakini pia, ningependekeza kwamba wakopaji wote katika utaratibu huu waangalie mikataba kwa makini sana wanapokopa.

Mheshimiwa Spika, tatizo la kusaini mikataba bila kuwa makini siyo la Serikali peke yake, inaweza ikawa hata kwa watu binafsi. Tafadhali atakayekopa yeyote achukue muda, asome mkataba ambao anaungia na shirika ambalo linamkopesha kabla ya kuweka saini yake kwa sababu ni muhimu kuangalia zile *clause* ndogo ndogo, tunasema *fine prints, small print*. Ni muhimu kuelewa unasaini nini, riba ni kiasi gani, *maintenance* na *repair* zitakuwa juu ya nani, bima nani atailipa na ni muhimu kuelewa kama huu mkataba anaousaini, unatoa fursa ya bima ya maisha. Mikataba mizuri mingi inatoa fursa ya bima ya maisha ya yule mkopaji ili punde ikitokea amefariki dunia, basi ile kampuni ya bima itamalizia kulipa lile deni, hakutakuwa na mtafaruku kwa wale watakaorithi mali za marehemu.

Mheshimiwa Spika, ningependekeza kwamba iwepo fursa ya kufanya baadhi ya hii mikataba katika lugha ya Kiswahili, maana wakopeshaji wengi watakuja na lugha ya Kiingereza. Lakini nadhani iwepo fursa kama mkopaji anakopa na ana shida na kiingereza, mikataba hii iandikwe kwa lugha ya Kiswahili ili mkopaji aweze kuweka saini na kuingia katika mkataba ambao anauelewa kwa undani kabisa.

Mheshimiwa Spika, lakini pia ningependa kuiasa Serikali na mamlaka nyingine, ziweke mkakati kwamba, ambao tutakuwa tunakopa tuweze kukopa vifaa ambavyo ni bora, visiwapatie fursa ambao wanakuja kwa ujanjajanja kuweza kupenyeza vifaa ambavyo siyo vya ubora ambao unafaa na ubora ambao utatusaidia.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, ninapenda tena nikushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia katika hoja hii na ninaunga mkono hoja hii iliyo mbele yetu. Asante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Eustace Katagira, asante sana kwa mchango wako. Waheshimiwa Wabunge, ninahusika na kikao kitakachoanza saa sita kule kwenye jengo la utawala. Kwa hiyo, sasa hivi namwomba Mwenyekiti - Mheshimiwa Job Ndugai aje ashike Kiti na kuendeleza shughuli zilizosalia za kupokea majadiliano ya Muswada huu.

Hapa Mwenyekiti (Mheshimiwa Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii muhimu iliyo mbele yetu. Kama maudhui ya Muswada yanavyoelezea, ni kwamba tunapiga hatua katika soko la namna ya kukopeshana hapa nchini. Tumezoea mtu anapotaka kukopa, anakwenda Benki, anatarisha mradi wake, baadaye anapewa pesa ambazo anazitumia kukidhi haja ya mradi wake.

Sasa leo hii tunajadili utaratibu mwingine wa kumwezesha mjasiriamali kukopa. Uaratibu huu ni wa kukopa kwa kupitia njia ya mjasiriamali kupewa kifaa ambacho anakihitaji katika shughuli zake za kiuchumi kwa utaratibu wa kulipa pole pole. Kwa hiyo, nitaanzia pale ambapo waliotutangulia wamechangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na nafasi ya Gavana katika Muswada huu. Ukienda kwenye *definition* ndani ya Muswada huu, *lessor* anazungumzwa kwamba ni kampuni yoyote itakayosajiliwa kufanya shughuli hii. Kwa maana hiyo, kampuni yoyote sio lazima iwe Benki au taasisi ya fedha.

Kwa maana hiyo, kama tunataka sana kumweka Gavana kwenye usimamizi wa Sheria hii, basi tutamweka kwa kadri tu ya vyombo vya fedha kwa maana ya benki na taasisi za fedha zinavyohusika katika utekelezaji wa Muswada huu. Lakini, ilimradi yatakuwepo na makampuni mengine yatakasajiliwa kufanya shughuli hii ambayo sio ya kibenki. Sasa usimamizi wa Gavana unakujaje hapa? Nadhani hiyo ndiyo hoja ya msingi ambayo waliotuletea Muswada huu wajaribu kuitafakari kwamba yapo makampuni mengine zaidi ya Benki ambayo yatafanya shughuli hii. Benki ziko chini ya himaya ya Gavana, sawa! Haya makampuni mengine je? Kwa nini Gavana ahusike?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu ni mzuri na mimi naukubali kwa asilimia mia moja kwamba tuupitishie. Lakini nataka tupendekeze tahadhari zifuatazo pamoja na ile ya kwanza niliyoitoa. La kwanza ni eneo la kodi. Kifaa ambacho mjasiriamali atakuwanacho na atakitumia kuzalishia shughuli yoyote ambayo ameikusudia, iwe ni kiwanda au ni shamba, kifaa hiki kitakuwa kinachakaa. Katika lugha ya kitaalamu, kwa lugha ya kigeni wanasema inabidi kuwe na *aspect* ya *depreciation*. Ili mradi kifaa hiki si cha mjasiriamali, maana kiko katikati ya mjasiriamali na yule anayeki-*finance*. Suala la kujiuliza, nani baina ya hao wawili ataweka *depreciation* kwenye vitabu vyake? Maana yake *depreciation* itakuwa kwenye vitabu vya nani? Vya mjasiriamali au vya yule aliye-*facilitate* hiyo mashine au huo mtambo kuwa ndiyo sasa utumike kwa kufanya shughuli ambayo mjasiriamali ametumia? Sasa utata huu ni muhimu ukapatiwa jawabu kwa sababu ya masuala ya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *section* ya tisa ya sehemu ya kwanza, inazungumzwa kwamba huu mkataba utakaoingiwa baina ya *lessor* na *lessee* ni *irrevocable* ana *independent*. Hapa nataka nisisitize umuhimu wa *section* hii ni kwamba tunatarajia na ni lazima iwe hivyo kwamba utaratibu wetu wa baadhi yetu tunaokopa, ukishindwa kukopa unakimbilia Mahakamani kwenye kuchukua hati ya dharura kusimamisha usifanyiwe mambo yoyote ya kisheria kwa sababu umeshindwa kukopa.

Katika sheria hii iwe wazi na dhahiri kabisa kwamba ukishaingia kwenye mkataba, wewe ni mtu wa ku-*perform* kama mkataba unavyotaka, ukishindwa, hatua za kukufilisi zinachukuliwa. Habari ya kwenda Mahakamani kuchukua hati ya dharura usifanyiwe hivyo, haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya saba ya sehemu ya tatu, inazungumzia kwamba kama mjasiriamali atakuwa na mtambo, mtambo huo malipo yake kwa vipindi vipindi yatatengenezwa kwa kuzingatia thamani ya ule mtambo pamoja na faida ya kampuni ambayo inaukopesha ule mtambo kwa njia ya taratibu. Lakini, eti itakapofika mwisho, yaani yule mjasiriamali akishalipa, kunakuja habari ya kuzungumza kama kile chombo auziwe huyo mjasiriamali au asiuziwe.

Nataka kushauri kwamba, suala la kusema kwamba mjasiriamali ameshalipa, halafu mwisho pale tunasema tuzungumze sasa hiki chombo ndiyo ukinunue au vipi! Lakini, Muswada kama ulivyo mbele yetu ni kwamba mkodishaji ndiye mwenye sauti kubwa kwamba anaweza akaendelea kuwa na kile chombo au afanye mazungumzo na yule anayekikodisha kwamba pamoja na kunilipa zile *instalments* zote umemaliza, lakini sasa leo tuzungumze habari ya je, unataka kukinunua au vipi! Hiyo nadhani itakuwa siyo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale watakaokuwa wanakodisha vyombo hivi, wawakodishe wakodishwa wakijua kwamba yule mkodishwaji akilipa malipo yote kwa mtiririko uliokubalika, siku ya mwisho analipa sehemu ya mwisho ya ule mkataba, basi na kile chombo ni chake, kusiwe tena na mazungumzo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili vile vile hatuna budi tulizingatie kwamba yule anayekodisha vyombo hivyo au vifaa hivyo, atakapokuwa anafanya mahesabu yake ya malipo ya kidogo kidogo yawe kiasi gani, sheria au Muswada tunaoadili unasema atatengeneza mahesabu yake akizingatia gharama ya ule mtambo kama ni mtambo, faida yake atakayopata.

Sasa ndani ya neno “faida” kwa kuwa hii ni habari ya kukopeshana kwa njia ya kutumia na kulipa taratibu, ndani ya ile faida kuna *implicit interest rate*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliotangulia wamezungumzia juu ya hili, nami nasisitiza. Ili utaratibu huu uwe kweli ni mkombozi kwa wananchi watakaoutumia, basi

haina budi ile riba itakayojengwa ndani ya zile sehemu ndogo ndogo zinazolipwa taratibu, iwe ni riba ya chini ukilinganisha na kama angekwenda kukopa Benki, vinginevyo utaratibu huu hautatusaidia, hautotofautiana na hali ilivyo sasa kwamba riba zetu kwa wanaokopa ziko juu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda ni vizuri pamoja na kwamba haya yanaweza yakaja kwenye utaratibu wa kanuni zitakapotengenezwa, lakini sio vibaya nikitafadhalisha kwamba watakapokuwa wanatengeneza kanuni baina ya kampuni inayokopesha na yule mkopeshwaji, mkataba wa kumkopesha utoe muda wa mpito kwa maana ya nafuu (*grace period*). Siyo leo nachukua gari, mwisho wa mwezi huu naambiwa nianze kulipa. Kuwe na muda wa nafuu kumwezesha huyu mjasiriamali kuanza kutumia kile kifaa kuzalisha ili apate nguvu za kulipa deni ambalo anastahiki kulipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la *insurance* kwa maana ya bima, limetajwa katika sehemu ya 13(4). Lakini, katika namna ambayo haionyeshi kwamba hii bima iwe katika utaratibu upi tuliozoea, kuna bima ya mtu wa tatu, kuna bima ya wizi tu labda na moto na kuna bima pana zaidi ambayo inajumuisha yote haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba Bima tunayoikusudia hapa isiwe chini ya Bima pana ambayo inajumlisha matukio yote mabaya yanayoweza kusibu mkataba baina ya mkodishaji na mkodishwa, kwa lugha tuliyoizoea ya kigeni napendekeza iwe ni *comprehensive insurance cover*, hiyo ndiyo itakayotoa jawabu zuri kwa pande zote mbili, anayekodisha na anayekodishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri vilevile nikasisitiza hapa kwamba Bima hii iwe *endorsed* kwa wote wawili mkodishwaji na mkodishaji wote wawe ni *beneficiaries* ili mwisho wa siku linapotokea baya yule anyekwenda kulipwa asiwe mmoja tu wawe wote wawili kwa sababu wote wana *interest* katika mtambo utakaohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni suala la elimu, hii ni bidhaa mpya katika soko kwa utaratibu mpya. Kwa hiyo, waliohusika ni vizuri wakatusaidia kutuelimisha hasa mantiki yake, na kwa nini wanadhani huu ni utaratibu mkombozi kwa mjasiriamali wa kawaida ukilinganisha na utaratibu uliopo sasa hivi wa mtu anapotaka kukopa anakwenda benki tu. Lakini leo hii kutakuwa na benki; kutakuwa na taasisi za fedha na kutakuwa na makampuni ambayo yataanzishwa hususan kwa ajili ya shughuli hizi tu za kufanya mikopo ya karadha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu kwa wananchi kuhusu utaratibu mzima wa karadha itangulie utekelezaji wa sheria hii pindi itakapopitishwa. Baada ya kusema hayo nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia na kama nilivyosema hapo mwanzo na mimi vilevile nauunga mkono muswada huu upite na hatimaye uweze kufanya kazi iliyokusudiwa, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, sasa naomba nimwite Mheshimiwa Castor Ligallama na Mheshimiwa Prof. Mtulya ajiandae.

MHE. CASTOR R. LIGALLAMA: Ahsante Mwenyekiti, nashukuru kwamba muswada huu umekuja wakati muafaka, wakati wajasiriamali wetu wanahitaji vitu vingi katika uzalishaji hasa zana za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huku nyuma *NBC* ilikuwa na mikopo ya karadha na katika *conventional Banks* hizi ukiziangalia wengi wanafuata masharti wakiangalia kigezo cha *collateral*, lakini katika ukopaji kuna vitu vingi, *character* ni kitu muhimu sana. Labda niongelee mfano wa kitu ambacho kimefanyika with *success* na nchi nyingi wametuita kwenda kuwaeleza wenzetu tumefanyaje. Mimi nilikuwa mfanyakazi wa benki ya *CRDB* na tulikuwa tunatoa mikopo ya namna ya kukopesha rasilimali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Kigoma ambako nimefanya kazi kwa muda wa miaka 15, kulikuwa na mradi ambao tulishirikisha *FAO*, Serikali na Benki ya *CRDB*. Tulikuwa tunawakopesha wavuvi wa kule zana za uvuvi *credit in kind*, kwa hiyo, ukizungumzia mikopo hii ya rasilimali ni sawa kama tunaongelea mikopo ya *credit in kind* kwamba unampa mtu zana za kwenda kufanyia kazi. Tulikuwa tunawakopesha mashine za kuvulia, tunawakopesha nyavu, karabai, mitumbwi, kwa hiyo, mtu analipa asilimia 25 ya gharama hizo halafu kwa miaka mitatu analipa kidogo kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulianza na watu 20 mwaka 1983 lakini mpaka mradi unakwisha 1993 tukawa tumezungusha mikopo ile kwa wavuvi 1000, *it was a successful story*, mimi mwenyewe niliitwa kwenda kuelezea kwa nchi za Kusini mwa Afrika, Harare, Mozambique kuelezea tumefanikiwaje. Kwa hiyo, hicho kitu kwa mzalishaji mali mdogo na vigezo tulivyokuwa tunatumia hatukujali sana *collateral* kwa sababu wale watu walikuwa na nyumba za kawaida tu vijijini lakini tulichokuwa tunajali ni *character* na wakati wa *interview* tulikuwa tunatumia watumishi wa Serikali wa Vijiji. Sasa naomba hata hizi kampuni zitakazokuja kuanzisha karadha watumie zaidi *character* kuliko *collateral* au kumwanganalia mtu kwa sababu wengi tunaotaka wafaidike ni hawa wajasiriamali wadogo wadogo walioko Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwa ni *successful story* kutoka 20 kwenda 1000 na wavuvi wengi wakabadilika hali ya maisha, wengi wametoka kijijini wanakuja kuwekeza Mjini Kigoma. Bahati mbaya watu wa Kigoma hapa wametoka, wengi ni mashahidi na kazi tuliifanya kwa miaka 10. Kwa hiyo, ukopeshaji wa rasilimali sasa hivi kwa mfano, katika Wilaya yangu tunahitaji sana matrekta, tunahitaji sana *caterpillars*, *water pumps*, tuna mito lakini hatuitumii wakati wa kiangazi, lakini mzalishaji anahitaji *water pumps* tu kufanya kazi kwa mwaka mzima wa kilimo. Hivyo, tunapenda tufanye kwa kutumia fursa hizi za kutumia *character* zaidi kwa wale wataoanzisha makampuni haya na kuweka riba ndogo. Wakati tunawakopesha wale wavuvi Kigoma riba ya kawaida ya Serikali kwenye mabanki ilikuwa asilimia 30 lakini sisi tulikuwa tunafanya asilimia 15 na tukafikia hatua ya kufanikisha kitu hicho, na kama walivyosema wenzangu *at the end of the day* kama watu wamemaliza kulipa *instalments* zao hamna majadiliano, vile vitu vinakuwa vyao, kwa sababu *instalments* zile zina-take care mambo yote yaliyobaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine ni suala la *security* kwa maana ya *insurance* lazima lichukuliwe kama ni kitu muhimu sana kwa sababu kuna uharibifu unaweza kutokea katikati na nani ajulikane atakayelipa Bima. Katika zana za kilimo kwa mfano, Kampuni sasa hivi ziko nyingi zinaleta zana, wapewe fursa hiyo kwanza kabla ya vitu vingine. Zamani karadha ya *NBC* walikuwa wanazungumzia zaidi usafirishaji lakini tuzalishe zaidi. Kwa hiyo, naomba hizi kampuni au wale watakaopenda kuwekeza katika zana za kilimo hao ndiyo wapewe fursa kwanza kwa sababu ni eneo ambalo sisi wote tunahitaji liwekezwe kwa hali ya juu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine ni muda wa kulipa isiwe chini ya miaka mitatu ili kumwezesha yule mjasiriamali mdogo apate muda mrefu wa kujiandaa au kulipa mkopo wake. Hapo katikakati kuwe na muda ambao mkopaji na mkopeshaji wanaweza kukaa kwa vipindi maalumu kuangalia hali ya mradi wenyewe unavyokwenda. Inawezekana mtu akachukua kitu *right from the start* kikawana matatizo lakini kwa sababu wewe umempa kama kutakuwa na muda mnakutana kuongelea matatizo ili kuwe na uwiano sawa katika shughuli nzima ya uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa na haya ya kuchangia katika mradi huu na napenda kuunga mkono na naomba kampuni zitakazoanzishwa zipewe nguvu na zielekezwe zaidi kwenye uzalishaji mali hasa kilimo. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Castor Ligallama, sasa naomba kumwita Prof. Mtullya na Mheshimiwa John Cheyo ajiandae. Simwoni Prof. Mtullya na vile vile simwoni Mheshimiwa John Cheyo. Waheshimiwa Wabunge kwa orodha ya wachangiaji tuliokuwa nayo imekamilika, wachangiaji wote wamepata fursa ya kuchangia isipokuwa hawa ambao nimewaita dakika za mwisho na bahati mbaya hawapo, kwa hiyo, tuta-*windup* jioni na tutaendelea na shughuli zingine za Bunge jioni ya leo, hivyo naomba kuchukua fursa hii kusitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni.

(Saa 6.19 Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)

Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tukae. Kipindi cha asubuhi tulikuwa tumemaliza wote waliokuwa wamependa kuchangia, kwa hiyo, sasa tunaingia kupata ufafanuzi wa hoja mbalimbali, namwita mmoja wa Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Mzee.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kukushukuru kwa kunipatia nafasi jioni ya leo ili niweze kuchangia kwa kufafanua baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge kwa ajili ya muswada huu wa karadha za fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijafanya hivyo napenda kwanza nitoe maelezo kwa kifupi tu ili kila mmoja wetu aweze kufahamu kwa nini tumekuja na muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninazo nukta kama tatu hivi ili ziweze kuniongoza katika kutoa ufafanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza mageuzi katika sekta ya fedha tuliyoanza kuyafanya tangu mwaka 1991 hayajamsaidia kikamilifu mjasiriamali, lakini jambo la pili ni dhahiri kwamba wananchi wetu wengi wanajishughulisha na masuala ya kilimo na uvuvi. Tija wanayoipata hivi sasa kutokana na shughuli zao ni ndogo kutokana na vifaa wanavyovitumia ni duni.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ni ushiriki wa wananchi wetu hasa katika sekta ya ujenzi hasa barabara ni mdogo kutokana na vifaa wanavyovitumia au kutokuwa na vifaa ambavyo vinahitajika hivyo kufanya mapato yetu mengi kwenda nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la nne ni taratibu za mikopo zilizopo hivi sasa zinahitaji dhamana jambo ambalo wananchi wetu wengi hawana dhamana hizo. Kwa maana hiyo Wizara yangu imelazimika kuleta muswada huu ili kuwawezesha wananchi wetu wajasiriamali wadogo na wale wa kati nao kufaidika katika mageuzi haya ya sekta ya fedha tunayoendelea nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kidogo na mimi nitoe ufafanuzi wa hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:- Kwanza kulikuwa na hoja ya elimu kwa wananchi kwamba itolewe ya kutosha kuhusiana na mfumo huu wa karadha ya fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia hoja hii naomba niwatambue kama ifuatavyo:- Mheshimiwa Abdallah Kigoda, Mheshimiwa Missanga, Mheshimiwa Luhahula, Mheshimiwa Lyamba, Mheshimiwa Mwambalaswa, Mheshimiwa Mchemba, Mheshimiwa Mpesya, Mheshimiwa Massaburi, Mheshimiwa Diana Chilolo na Mheshimiwa Martha Umbulla .

Mheshimiwa Naibu Spika, wingi wa Waheshimiwa kuchangia katika eneo hili ni dhahiri kwamba eneo hili ni muhimu sana, na napenda kutoa ufafanuzi kama ifuatavyo:-

Ni kweli utaratibu wa karadha ya fedha ni mpya hapa nchini kwetu hivyo ipo haja ya kutoa elimu ya kutosha kwa umma mijini na vijijini, lakini vilevile napenda kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba Shirika la Fedha la Kimataifa *IFC* limeanza kutoa elimu tangu mwaka 2005 kupitia vyombo mbalimbali vya habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, baada ya sheria hii kupita na kutiwa saini na Mheshimiwa Rais, Elimu itaendelea kutolewa kwa faida ya wananchi wetu kwa kufanya warsha za kikanda ili wananchi wengi waweze kufahamu utaratibu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba *IFC* tayari imekwishaingia mkataba na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa maana ya

kuandaa mitaala ili suala hili lifundishwe katika kiwango cha shahada na vilevile kutoa mafunzo mafupi pale yatakapohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wabunge ni kwamba mpango huu au sheria hii iwasaidie zaidi wananchi wa vijijini. Waliotoa hoja hii, naomba niwataje: Mheshimiwa Missanga, Mheshimiwa Luhahula, Mheshimiwa Mchemba, Mheshimiwa Diana Chilolo, na Mheshimiwa Martha Umbulla .

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme kwamba nia ya sheria hii ni kuwarahisishia wajasiriamali wadogo wadogo na wale wa kati wa mijini na vijijini upatikanaji wa rasilimali kwa ajili ya shughuli zao. Tatizo lao lilikuwa ni ukosefu wa mitaji na dhamana, kwa hiyo, sheria hii imejaribu kuondoa tatizo lao na kufanya utaratibu ili waweze kupata vifaa au zana wanazozihitaji ili kukuza juhudi zao.

Mheshimiwa Nabu Spika, ni lazima tukubaliane kwamba zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania wanaoishi vijijini na ni wakulima, kwa maana hiyo, sheria hii au mpango huu utawafikia huko waliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wabunge ni suala la kuondoa urasimu katika upatikanaji wa vifaa, naomba nimnukuu Mheshimiwa Luhahula ambaye ndiye aliyetoa hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile mfumo wa karadha ya fedha hautakuwa na masharti magumu, ni dhahiri hakutakuwa na urasimu, lakini jambo la msingi hapa ni lazima tuwe nalo sisi Wabunge ili tutakaporudi majimboni kwetu tuweze kuwasaidia wananchi wetu kuwafahamisha ni mkopaji awe anafanya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwa wale ambao wanataka kuingia katika utaratibu huu ni muhimu kuelewa suala zima la sheria pamoja na mkataba kabla hajasaini kwa sababu unaposaini mkataba ni lazima mkataba ule uheshimiwe vinginevyo unaweza ukajikuta uko kwenye matatizo. Lakini jambo la msingi ambalo vilevile tunapaswa sisi kulifahamu ni suala zima kwa mkopaji kuwa mwaminifu katika kurejesha hili, ni muhimu sana ili uweze kuaminika na baadaye uweze kukopa vifaa vingine na vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wabunge ni suala la muda wa kulipia uwe mrefu zaidi hasa kwa vifaa vya kilimo na uvuvi, hoja hiyo ilizungumziwa na Mheshimiwa Lyamba, Mheshimiwa Mpesya na Mheshimiwa Diana Chilolo. Nataka niseme kwamba lengo la Taasisi ya Fedha Duniani (*IFC*) ni kuboresha mazingira ya biashara kwa wajasiriamali wadogo wadogo na wale wa kati. Kwa kuwa wananchi wetu wengi ni wakulima na wavuvi tunaona ipo fursa ya kuwasaidia wale watakaokopa zana za kilimo na uvuvi. Muda wa kurejeshamkopo unategemea zaidi kifaa kinachokopwa, hata hivyo, uhuru wa kukubaliana baina ya mkopaji na mkopeshaji ni dhahiri utakuwepo kwenye mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nimalizie kwa kujibu kwa kufafanua hoja mbili zilizotolewa na Mheshimiwa Lucy Owenya wakati akiwasilisha taarifa ya Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kwanza alielezea suala zima la kutafsiri *natural resources* katika rasimu ya muswada huu wa sheria. Napenda kumfahamisha kwamba suala la maliasili ni rasilimali ya Taifa ambayo haikupaswa kuwepo katika muswada huu. Kwa maana hiyo tumeliondoa, kwa hiyo, kipengele cha 3(C) tumekifuta na hakuna haja tena ya kukifanyia tafsiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili Mheshimiwa Lucy alizungumzia mamlaka ya Gavana yataingiliana na mamlaka ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha katika suala zima la kutunga Kanuni. Tumeliona hilo na tumeona kwamba kifungu namba 23(2) tukifute ili tumbakishie Waziri mamlaka yake ya kutunga Kanuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, sasa namwita mtoa hoja, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Uchumi.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu, utakaosaidia wananchi wetu wakiwemo wakulima na wajasiriamali wengine.

Ninapenda kushauri yafuatayo katika Muswada huu:-

1. Elimu itolewe kwa wananchi ili waweze kuuelewa vizuri; Wizara inaweza kutumia wataalamu mbalimbali, vinginevyo wananchi hawatafaidika.
2. Ugumu wa upatikanaji mikopo; Serikali ihakikishe wananchi wasisumbuliwe kuupata mkopo huo ulio ndani ya Muswada. Mkodishaji asije akajikita mjini pekee, lazima vijijini waende.
3. Kuondoa urasimu; ninaamini Muswada huu ukifanikiwa, inawezekana pakawepo urasimu mkubwa sana wa kupata mkopo huu. Ninaomba mashirika yatakayohusika, Serikali iyasimamie kwa karibu zaidi; madaraka yakasimiwe haraka kwenda chini.
4. Serikali inaimarisha ulinzi na usalama maeneo ambayo makampuni yataamua kuwekeza ili wasije kukata tamaa kutokana na kukosa utulivu.
5. Serikali ihakikishe mabanki yanakuwepo katika Makao Makuu ya kila wilaya, kwani kukosekana kwa huduma hii kunazorotesha huduma hii mfano, Bukombe

MHE. BASIL P. MRAMBA: Mheshimiwa Spika, ninafahamu kuwa, uamuzi wa *BLM* ulitaka Muswada huu uende sambamba na marekebisho kwenye Sheria ya *Hire Purchase* chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko. Ninalewa sheria hii iko kwenye mchakato lakini si kwa kasi iliyotarajiwa; ni muhimu Waziri wa Fedha akaingilia kati. *Hire Purchase* itatumiwa zaidi na wajasiriamali wadogo wadogo, wenye viwanda au biashara au hata uzalishaji wa aina nyingine, hasa vijijini. *SIDO* wana uzoefu mzuri na uelewa mzuri wa eneo hili. Wizara ya Fedha wana *interest* kwani ni aina ya mikopo inayoweza kufanywa na taasisi za fedha au nyinginezo na hivyo kuhitaji kutupiwa macho na *BOT* au Hazina kwa namna moja au nyingine.

Mheshimiwa Spika, ninashauri pia kuwa pengine *hire purchase, insurance* na hata *credit guarantee* zingeweza kuangaliwa kwa pamoja na *financial leasing*, kwa lengo la kuondokana na wajasiriamali kulipia kila kitu kwa fedha taslimu. Tuelewe kuwa mkopaji Mzalendo ni mtu au taasisi nyonge sana, asiye na uzoefu wala uelewa, wala utamaduni wa siku nyingi katika eneo hili; ni muhimu sana Waziri wa Fedha au mhusika akaona namna ya kumlinda sana mkopaji mdogo ili asifilisike na kupoteza mali au asidanganywe na wajanja au asikimbiie Mahakamani kuzuia mali inayochukuliwa pale anaposhindwa kulipa mikupuo. Mahakama zitumike kama *last resort*, mfano, kama majadiliano au udhamini fulani umeshindikana.

Mheshimiwa Spika, suala la riba (*interest rate*) ni muhimu kufanikisha *financial leases and hire purchases* kwa kuwa za chini kuliko katika benki, hasa kwa *SMES*. Serikali inaweza kutoa *subsidies* au *guarantees* za *interest rates* hasa kwa wanaokopa kuzalisha (kilimo, viwanda na kadhalika) au kufanyia biashara za nje.

Mheshimiwa Spika, ninashauri *financial leases or hire purchases* ziingizwe kwenye utaratibu wa *Credit Information Bureau* (wakopeshaji kupeana habari za wasiolipa).

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, ninapenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi, kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu muhimu, ambao una maslahi sana na wajasiriamali wetu.

Mheshimiwa Spika, vilevile ninawapongeza Waziri wa Fedha na Naibu Mawaziri wote wawili, kwa busara kubwa walizotumia kuwasilisha Muswada huu wa Sheria ya Mikopo ya Ukodishaji Rasilimali wa mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizi, ninaomba sasa nitoe mchango wangu kama ifuatavyo:-

(a) Elimu kwa Wajasiriamali: Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa Serikali ina lengo zuri kwa Watanzania, ninapata wasiwasi kuwa watakaokuwa wananufaika na mikopo hii ni wajasiriamali waliopo mijini, kwani ndiyo wenye uelewa wa kupata mikopo hii. Ninaomba Serikali itoe elimu kwa wajasiriamali walioko vijijini ili nao

waweze kupata mikopo hii na kupata uwezeshaji wa kuwekeza katika maeneo mbalimbali

(b) Mheshimiwa Spika, vilevile wajasiriamali wetu wengi wanashindwa kupata mikopo hii kwa ajili ya masharti kuwa magumu sana kwani mkopaji anatakiwa awe na nyumba yenye hati miliki kwa sababu wakulima na wajasiriamali wengi walioko vijijini hawana hati za nyumba au *lease*, hata mashamba yao hayana *lease*. Vilevile upimaji wa viwanja na utoaji wa hati na *lease*, unahitaji gharama sana kwa wajasiriamali walioko vijijini. Ninaomba Serikali ipunguze masharti ya utoaji mikopo ili wajasiriamali wengi hasa walioko Vijijini, waweze kukopesheka; ama upimaji wa viwanja na mashamba uwe bure kwani fedha zamikopo huanza kutumika kabla ya kuanza mradi wenyewe, ndiyo maana wengi hushindwa kuendelea na kukwama kulipa mkopo.

(c) Mheshimiwa Spika, vilevile ninapenda kuishauri Serikali kuwa, mikopo inayotolewa na Serikali au mashirika mbalimbali, inaondoa tija kwa wajasiriamali kwani ni viwango vya chini sana, havilingani na miradi yao; mfano, mkulima anapewa shilingi milioni moja hadi milioni tano, fedha hiyo hiyo anunue pembejeo na gharama za uendeshaji, haitoshi. Ninaishauri Serikali kuongeza kiwango cha fedha za kukopa kwa wajasiriamali wetu ili waweze kuzalisha zaidi ili kupunguza umaskini kwa Watanzania.

(d) Mheshimiwa Spika, ninapenda kuishauri Serikali kuwa, mteja anapokopeshwa apewe muda wa kutosha wa kuanza kuzalisha, ndipo aanze kurudisha mkopo kuliko ilivyo sasa. Vilevile riba ni kubwa, ipunguzwe ili mjasiriamali aweze kupata faida kupitia mkopo huo.

(e) Mheshimiwa Spika, pamoja na nia njema ya Serikali kwa Wajasiriamali, ninapenda kuishauri Serikali kutoa mikopo kwa wajasiriamali kwa wakati muafaka; mfano, wakulima mara nyingi hupata mkopo muda ambao sio wa kilimo na huwafanya kutumia fedha hizo kwa shughuli nyingine. Endapo muda wa kilimo ni Novemba basi Oktoba ili ajiandae vyema kwa kilimo kitakachotoa tija ,kitakachotoa mazao na kumwezesha kulipa mkopo bila wasiwasi pia urejeshaji wa mkopo uanze baada ya miezi sita ili apate muda wa kuzalisha.

(f) Mheshimiwa Spika, vilevile ninapenda Serikali itambue kuwa wajasiriamali wetu wa leo wanakwenda sambamba na teknolojia ya sasa, kwani wanakwenda shambani kwa magari lakini mafuta yamepanda, hata ushuru wa leseni ya barabara umepanda sana; hayo yote bado ni kikwazo kwa wajasiriamali wetu, hata mikopo wanayopata wanaona ni fedha ndogo sana. Hivyo basi, yote haya ni mambo ya kuyatazama upya ili kuleta tija kwa wajasiriamali wetu hasa walioko vijijini.

(g) Mheshimiwa Spika, mwisho, ninapenda kumalizia mchango wangu kwa kuunga mkono Muswada huu, nikitegemea hoja au mchango wangu utafikiwa kwa maslahi ya Watanzania.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, ninaunga mkono hoja kwa asilimia 100. Muswadahuu umekuja wakati mwafaka kumsaidia mjasiriamali mdogo wa Tanzania.

Serikali ifanye mkakati mahususi wa kuwaelimisha Watanzania kuhusu Muswada huu; vinginevyo, wajasiriamali watakaofaidi ni wale wa mijini tu ambako habari hufika haraka.

Watanzania wengi watakimbilia mashine ambazo ni rahisi kutumika kama vile malori, mabasi, matrekta na kadhalika, lakini vilevile viko *vulnerable* sana. Ninashauri bima itakayowekwa na Kampuni ya Karadha iwe ni ile pana ili kulinda gharama za mashine hizi zote.

MHE. BENSON M. MPESYA: Mheshimiwa Spika, ninaomba nianze kwa kuunga mkono Muswada huu ulioletwa na Waziri wa Fedha na Uchumi.

Muswada huu ni wa kibunifu mno, maana unalenga kiubua fursa za kiuchumi kwa watu wa kati na wa chini, ambao ndio walengwa katika suala zima *la poverty alleviation*. Ili kujenga mazingira ya kupunguza umaskini wa kipato ni bora Muswada huu ukazingatia yafuatayo: Muda wa kurejesha mkopo huu uwe mpana na uzingatie msimu wa mavuno wa maeneo ya vijijini; riba iwe ndogo ili iwe ni motisha kwa watu vijijini na kupunguza *rural-urban migration*; kwa kuanzia mkopo uwe ni wa kikundi; riba iwe asilimia moja, malipo yawe *quarterly* ikiwezekana; walipaji wapewe mafunzo ya awali; na wakopaji watembelewe na kushauriwa kadri inavyofaa.

Ninaishauri Serikali iipitishie Sheria hii haraka ili ianze kutumika kwa maslahi ya wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

MHE. CLEMENCE B. LYAMBA: Mheshimiwa Spika, ninapenda kushukuru kwa kupata nafasi ya kutoa mchango wangu kwa Muswada huu muhimu. Kwanza ieleweke kwamba, mfumo huu wa ukodishaji vifaa au bidhaa au mashine kwa wajasiriamali hasa vijijini ni mgeni kabisa. Wananchi wengi hawauelewi jinsi utakavyofanya kazi. Kwa hiyo ni lazima juhudi za pekee zifanyike kuhakikisha elimu na hamasa kubwa na ya kudumu, inaendelea kwa kuwatuma maafisa wengi vijijini kwenda kutoa elimu juu ya mfumo huu na ikiwezekana matangazo maalumu na *campaigns* zionyeshe katika vyombo vya habari ikiwa ni pamoja na katika runinga.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wakopaji katika mfumo huu kwa shughuli za kilimo wanakabiliwa na *risks* nyingi kama ukame na mafuriko ambavyo havitabiriki na athari hizi zinaweza kupunguza uwezo wa kurejesha malipo kwa mkopaji; ninashauri Serikali iangalie uwezekano wa kutafuta njia za kutoa *incentives* au ruzuku kwa wakopeshaji ili watoe masharti nafuu kwa wakopaji kwa shughuli za kilimo. Moja ya motisha inayoweza kuangaliwa ni kuwapa muda mrefu zaidi wa kurejesha malipo, pamoja na punguzo la kodi katika maeneo yanayowezekana.

Baada ya mchango huu, ninaunga mkono hoja.

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu, ingawa kwa kiasi kikubwa umechelewa. Ninaupongeza kwa sababu utawasaidia sana wajasiriamali kupata vifaa au mitambo kwa kutoa fedha kidogo badala ya kuhangaika kupata fedha zinazoweza ununuzi wa vifaa.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba:-

(a) Elimu ya kutosha itolewe kwa wananchi ili mpango huu ujulikane vizuri kwa wananchi kwamba, utasaidia kupiga vita dhidi ya umaskini, utasaidia kuinua mapato ya wananchi na vilevile kuboresha maisha yao.

(b) Suala la riba liangaliwe vizuri na tofauti ionekane; ukilinganisha na riba za mablenki, riba iwe ndogo.

(c) Mikopo mingi au mipango mingi ya kuwawezesha wananchi kama vile Mfuko wa Mheshimiwa Rais Kikwete; Mfuko wa Vijana na Wanawake; na *PRIDE*, inawafaidisha wananchi walioko Mijini na kuwakwaza au kuwabagua wananchi wa vijijini.

(d) Mheshimiwa Spika, je, mikopo ya karadha itawafikia vipi wale waliopo vijijini ambao ni takriban asilimia 80; Serikali itaweka utaratibu gani wa kuhakikisha wananchi wa vijijini wanafaidika na utaratibu huu?

(e) Makampuni yatakayofanya kazi hii ya kukodisha au kukopesha, yawe yenye sifa ya uadilifu na yalete vifaa safi na sio feki.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii.

MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS: Mheshimiwa Spika, Muswada huu ni mzuri na ninaomba upitishwe, lakini kuwe na usimamizi mzuri na wahusika kujali maslahi ya Watanzania na maendeleo ya nchi, pia kumfikia mwananchi yeyote apate faida ya Sheria hii.

Mheshimiwa Spika, Mikataba ya Sheria katika Muswada ifafanue vizuri pale panapokopwa au kodi zozote kwa pande zote hasa kwa kuzingatia wajasiriamali wetu, wana hali duni. Kwa hiyo, ninaomba Serikali iweze kusimamia vizuri kama walivyowasilisha Muswada huu kwa ushirikiano na wataalamu. Sina wasiwasi chini ya Mheshimiwa Waziri Mustafa Mkulo na Manaibu wake. Ninatumaini Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya itawezekana.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Naibu Waziri na wataalamu wote wa Wizara hii. Kwa kuwa nia ya Serikali ni kusaidia wajasiriamali ambao wana nia ya kujikwamua kutokana na umaskini na kujipatia maendeleo; ningeshauri Wizara baada ya Muswada kupitishwa na Rais, ni vyema elimu ikatolewa kwa kupitia vyombo vya habari kwa kuweka vipindi maalumu, kama vile Radio, TV na magazeti ili wananchi waelimike zaidi na kujua matumizi yake. Kwa kufanya hivyo, kutawaondolea woga au wasiwasi wa kukopa.

Sheria ikipitishwa basi nakala zisambazwe mikoani na wilayani ili waweze kusaidia kutoa elimu kuna wajasiriamali wadogo.

Wananchi washauriwe hasa wajasiriamali, elimu ya kuwa na hati za kumiliki ardhi ili watumie kama dhamana yao ya kupata mkopo. Riba zipunguzwe kwani ni kubwa sana katika Mabenki, ili yule anayeingia mkataba na kukodi asiumie zaidi.

Kodi ipunguzwe kwa vifaa vitakavyoingizwa hapa nchini ili isimumize mjasiriamali.

MHE. JANETH M. MASSABURI: Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Uchumi, kwa kuleta Muswada huu ambao ulikuwa unasubiriwa kwa shauku kubwa na wajasiriamali wetu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwanza, Serikali itoe elimu kwa umma kuhusiana na Muswada huu ili kila mwananchi au wajasiriamali, waelewe kabla ya kuomba mikopo hiyo. Hii itasaidia kupata uelewa katika suala hili la ukopaji wa vifaa vya kutendea kazi au vya kuzalishia mali, mazao na kuleta tija. Pili, kuwepo na utaratibu mzuri wa kulipa riba ndogo katika mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, muda wenye kuleta unafuu katika kulipa uzingatiwe; malipo yaanze kulipwa baada ya miaka miwili au mitatu ya uzalishaji. Vikundi vidogo vidogo vilivyoko vijijini, vielimishwe na kusimamiwa kwa ufasaha kwa lengo la kuviwezesha kupata vifaa hivyo na hasa matrekta ya bei nafuu na utalaamu.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu utapunguza vijana wetu kukimbilia mijini. Umuhimu upelekwe vijijini, ndiko kwenye malighafi (mazao).

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono Muswada huu muhimu sana kwa uchumi wa wananchi na hasa kwa wananchi/wajasiriamali wetu wadogo wadogo.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI): Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kutoa shukrani za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia Muswada huu ama kwa kuzungumza hapa Bungeni na wale wote ambao wamechangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwatambue Waheshimiwa Wabunge hawa kwa majina kama ifuatavyo:-

Kwanza, Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuzungumza ni Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, Mbunge wa Handeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mbunge wa Viti Maalum na Msemaji kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Yustus Katagira, Mbunge wa Kyelwa, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mbunge wa Tabora Mjini, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mbunge wa Kilombero na Naibu Waziri mwenzangu wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Omar Yusuph Mzee, Mbunge wa Jimbo la Kiembe Samaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi, naomba niwatambue Waheshimiwa Wabunge wafuatao: Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, Mbunge wa Handeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Luhahula, Mbunge wa Bukombe, Mheshimiwa Vuai Abdallah Hamis, Mbunge wa Magogoni, Mheshimiwa Clemence B. Lyamba, Mbunge wa Mikumi, Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, Mbunge wa Rombo, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini na Mheshimiwa Martha Umbulla, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Manyara.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi kwa kuunga mkono Muswada huu. Lakini pia napenda kuishukuru Kambi ya Upinzani kwa kuunga mkono vilevile Muswada huu. Naahidi kwamba Serikali itafanyia kazi michango na mawazo mazuri yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi na yale yaliyotolewa na Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

Naomba sasa nijikite kwenye kujibu hoja mbalimbali ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezitoa ama kwa maandishi au kwa kuzungumza hapa Bungeni leo asubuhi. Hoja hizi ziligawanywa katika mafungu manane na nne Naibu Waziri mwenzangu amekwishazigusia, kwa hiyo, nitagusia nne zilizobaki kimaungu. Kwanza ni riba iwe ndogo ili kuweza kusaidia wajasiriamali wadogo na Waheshimiwa Wabunge wafuatao walilisemea hili la riba:- Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Katagira, Mheshimiwa Mchemba, Mheshimiwa Mramba, Mheshimiwa Kaboyonga, Mheshimiwa Mpesya, Mheshimiwa Massaburi na Mheshimiwa Diana Chilolo. Pili, Serikali isimamie kwa karibu zaidi mpango huu wa mikopo wa karadha ya fedha. Mheshimiwa Vuai Khamis alilizungumzia jambo hili, Mheshimiwa Ruhahula alilizungumzia vilevile. Mheshimiwa Basil Mramba, Mheshimiwa Mchemba na Mheshimiwa Diana Chilolo.

La tatu kuwepo kwa benki au taasisi za fedha katika Makao Makuu ya Wilaya na Mikoa, alizungumzia suala hili Mheshimiwa Ruhahula na vifaa viwekewe bima na iwe kwa wote mkopaji na mkopeshaji, walilizungumzia Mheshimiwa Mwambalaswa na Mheshimiwa Kaboyonga. Naomba nijibu sasa hizi hoja moja moja kama nilivyozitaja.

Nikianza na hoja inayohusu riba iwe ndogo ili iweze kusaidia wajasiriamali wadogo na tunakiri kwamba riba kwa mikopo itolewayo hapa nchini na taasisi za fedha imekuwa juu kwa muda mrefu na Serikali imefanya juhudi kubwa kuhakikisha kuwa inashuka ili wananchi walio wengi waweze kukopa na kupata faida kutokana na shughuli watakazofanya kutokana na mikopo yenyewe.

Juhudi za Serikali za kupunguza riba zinajidhihirisha kuwa zimeanza kwa sasa na kwa kasi nzuri kupunguka kwenye dhamana za Serikali na pale hili linapotokea basi riba kwa ujumla wake katika benki za biashara na vyombo vingine vya fedha huwa zinafuata mkondo kwamba ile riba ya Benki Kuu ya *Treasury Bill* ya siku 364 inachukuliwa kama kigezo na kutoka pale ndipo sasa wanapoanza kukokotoa kiwango cha riba ambacho watatoza. Wastani wa riba kwa mfano za dhamana za Serikali umeshuka toka asilimia 17.10 mwezi Julai, 2007 hadi kufikia asilimia 11.40 mwezi Desemba, 2007 na mwezi Machi, 2008 zilikuwa asilimia 7.4 na ukishajumlisha na wanapokokotoa wale wenzetu katika vyombo vya fedha kwa kuongeza gharama zao na mara nyingi kuongeza vilevile wanachoona kwamba ni hatari iliyoko katika kukopesha, tunatarajia sasa kwamba riba ambazo zitatozwa kwenye benki zetu ni asilimia 12 au 14. Tunajua kwamba kuna wakati mwingine hata sasa hivi ziko kwenye *single digit*.

Kwa vile mwenendo wa riba za dhamana za Serikali huashiria riba za mkopo katika mabanki na taasisi zingine za fedha matarajio ya Serikali kwa hivi karibuni riba za mikopo zitapungua na kwa maana hiyo wajasiriamali wadogowadogo watakapoanza kufaidika na mikopo kutokana na utaratibu huu mpya wa vifaa basi riba zitakuwa zinawezekana kukopwa kwa wale wajasiriamali wadogo wadogo.

Hoja ya pili Waheshimiwa Wabunge ni kuitaka Serikali isimamie kwa karibu zaidi mpango huu wa mikopo wa vifaa. Sheria hii inampa Waziri wa Fedha na Uchumi mamlaka ya kutengeneza Kanuni zitakazowezesha utekelezaji wa Sheria hii. Hivyo kusimamia kwa karibu zaidi mpango huu wa mikopo kwa njia ya vifaa na ni nia ya Serikali, ni dhamira ya Serikali kuwa karibu sana na Sekta hii ili matarajio ambayo yamepangwa na malengo ambayo yamepangwa basi yawezekane. Tumesema kwamba tunatarajia kwamba kwa kukopa wananchi wetu kwanza wataweza kuongeza kipato chao lakini kutokana na hilo vilevile wataboresha maisha yao lakini uchumi kwa jumla na pato la Taifa litakua.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni kuwepo kwa benki au taasisi za fedha makao makuu ya Wilaya. Niseme hapa kwamba nia ya Serikali ni kupeleka huduma za kibenki vijijini. Na kama tulivyokwishasema mara nyingi Serikali inashirikiana kwa karibu na vyombo vya fedha kuwepo kwa hivi vyombo vijijini. Lakini tunapenda kusema kwamba ni vizuri tukazingatia kwamba Serikali kwa sasa hivi kwa kweli haimo kwenye biashara hii ambayo inaendeshwa na mabanki na taasisi zingine za fedha. Kwa hiyo, Serikali inachoweza kufanya ni kuwahimiza na kuwahamasisha wenzetu wasogeze huduma hizi vijijini na wanafanya hivyo. Hapa hatuzungumzii tu benki za biashara lakini tunazungumzia vyombo vingine vya huduma za kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali vilevile inaboresha mazingira ya kibiashara na ukuaji wa uchumi. Na hapo panapotokea hivyo basi benki zenyewe na taasisi za fedha zinafungua matawi kwenye ngazi hizi za Wilaya, mara nyingine zinafika kwenye ngazi za Tarafa bila sisi Serikali kuwa na sababu ya kuwahimiza. Lakini Benki Kuu vilevile tunaalewa kwamba ina utaratibu wa kutoa leseni kwa benki za jamii (*Community Banks*) ambazo na zenyewe zinaweza kuanzishwa kwa mitaji midogo ilimradi wananchi wa jamii husika wajipange vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema awali mazingira ya kibiashara na ukuaji wa uchumi ni kigezo kikuu ambacho mabenki na taasisi zingine za fedha hutumia kuamua kuanzisha matawi katika sehemu mbalimbali za nchi yetu. Kuanzishwa kwa huduma hii ya mikopo kwa njia ya vifaa, karadha ya fedha, tunaamini kutawezesha kuongezeka kwa mahitaji ya kibiashara katika maeneo mbalimbali pamoja na makao makuu ya Wilaya zetu na hivyo kuhamasisha mabenki na taasisi zingine ambazo siyo lazima ziwe za kibenki kufungua matawi huko na wananchi kupata fursa ya kukopa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa vifaa viwekewe bima na iwe kwa wote mkopaji na mkopeshaji. Jibu letu ni hili, mwekezaji aweze kuwa na imani ya kurejeshewa pesa yake iliyonunua kifaa cha mjasiriamali husika na ni lazima kifaa hicho kikatiwe bima. Sheria yenyewe tayari inamlazimu yule mkopaji kukata bima kwa ajili ya kile kifaa. Hii ni kutokana na ukweli kwamba endapo litatokea janga lolote la hatari basi mwekezaji atakuwa na imani kuwa hatapata hasara kwa kuwa bima ile atakayokuwa amekata ndiyo itakayomlipa ama kumpa kifaaa kingine badala ya kile cha awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaamini kwamba kile kifungu cha 13 ambacho kinalazimu vifaa hivi vikatiwe bima, tutaweza kujenga msingi imara wa karadha ya fedha kwa upande wa wawekezaji wa ndani na wa nje wataamini kwamba hawatapoteza kwa sababu siyo tu kwamba kile kifaa yule mtumiaji anatumia kwa uangalifu kama Sheria inavyotaka lakini vilevile kwamba kuna mtu wa tatu yaani bima ambaye ikiwa kile kifaa kitaharibika basi ataweza kufidiwa. Ulipaji wa bima unategemea makubaliano baina ya mkopaji na mkopeshaji kisha makubaliano hayo yatakuwa ni sehemu ya mkataba wa kisheria kama inavyotaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hoja za mwakilishi wa Upinzani, yeye aliamua kwenda karibu kifungu hadi kifungu na ningependa na mimi nirudie zile hoja zake ambazo alitaka majibu na hoja yake ya kwanza katika hotuba yake ilikuwa mikataba ya karadha ya fedha iwe na maudhui sawa (*standard agreements*) kama ilivyo mikataba ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa utaratibu wa karadha ya fedha kwanza unahusisha kampuni za karadha au benki zenye misingi ya kiutendaji ambayo haikufanana ambayo imetofautiana, na bidhaa za ukodishaji za aina tofauti, hazikufanana. Shughuli au biashara tofauti na mazingira ya matumizi ya bidhaa hizo vilevile vinatofautiana, na kutokana na tofauti hizi ni vigumu kuona jinsi ambavyo tunaweza kuwa na mikataba ambayo imefanana. Na ni kweli kwamba karadha ya fedha ni dhana ngeni kwa wananchi wengi nchini. Serikali kwa kushirikiana na asasi mbalimbali itaendelea kuwaelimisha wananchi wetu kuhusu masuala ya karadha ya fedha kama ambavyo

Serikali imekuwa ikifanya panapotokea jambo jipya kama hili. Tayari kwenye hili Serikali iliendesha Semina kwa Waheshimiwa Wabunge na hatutasita kuendelea kufanya hivyo kwa umma na kama tulivyosikia rai kubwa katika hoja hizi ni elimu kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kutokana na ile Semina basi kwa Wabunge kwa sababu ni wawakilishi wa wananchi na mara nyingi sisi ndiyo wenye majukwaa, kwa kweli tuna nafasi ya kuzungumza na wananchi. Mara nyingi kulikuwa labda mtu mwingine yeyote ukitoa Wachungaji na Mashehe tu. Matumaini ya Serikali ni kwamba basi Wabunge tutaungana katika kuwaelimisha wananchi wetu. Tuanzie hapo, Serikali kwa upande wake itafanya kila linalowezekana kufanya hivyo kupitia kwenye magazeti, TV zetu, Semina mbalimbali, vyama vya wafanyakazi na waajiri na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa Sheria iweke muda maalumu kwa karadha ya fedha kumpatia mkodishaji rasilimali. Kwa hiyo, akienda kuomba baada yamuda fulani iwe wiki mbili, mwezi mmoja basi awe kile kifaa amekipata. Kama nilivyoeleza katika jibu la msingi la hoja iliyotangulia, biashara ya karadha ya fedha itafanyika katika mazingira tofauti yatakayohusisha rasilimali tofauti ambazo upatikanaji wake utafanyika kwa utaratibu tofauti. Kwa mfano, unaweza kutaka wewe kifaa ambacho ni cha kutengenezwa ambacho muda siyo lazima udhihirike, lakini vilevile inawezekana wewe mkopaji ukachukua muda kutimiza masharti ya kupewa mkopo wa kifaa unachokitaka. Sisi tunaona kwamba kuweka muda maalumu ndani ya sheria ambapo kampuni za karadha na mabenki zitapaswa kuzingatia katika kumpatia mkodishaji rasilimali, kwanza kutaondoa ule uhuru wa wakopeshaji kushindana kwenye soko, watabanwa. Lakini vilevile tutakuwa tunaingiza kwenye Sheria jambo ambalo kwa kweli ni la kiutendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunadhani kwamba hapana, hili tuliache. Lakini niseme kwamba katika kutengeneza kuunda zile Kanuni basi ikionekana au ikidhihirika kwamba ni busara kufanya hivyo, basi tutafanya hivyo. Lakini niseme vilevile kwamba kampuni hizi za karadha na mabenki haya ambayo yatashughulikia na biashara hii siamini kwamba zitakuwa na uwezo wa kutoa mikopo hii kwa kasi iliyolingana. Wengine watakuwa na uwezo zaidi ya wengine. Kwa hiyo, kwa sababu hizi tunafikiri kwamba ni vema Sheria ikabaki kama ilivyo ili la msingi turuhusu ushindani. Moja ya mambo ambayo yamezungumzwa ni riba kwamba tufanye kila linalowezekana ili wakopaji waweze kuimudu. Njia mojawapo ya kushusha kiwango cha riba ni kusukuma ushindani katika biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya tatu ilikuwa ni tafsiri ya maneno *natural resources* ambayo mwenzangu amekwihalisemea hilo. Hoja ya nne ni kuhusu kuwa na kifungu katika Muswada kinachobainisha sharti la mkodishwaji kutokuwepo. Mkodishwaji rasilimali kulipa malipo ya awali kwa kampuni ya karadha ama chombo kingine cha fedha. Chini ya utaratibu mzima wa karadha ya fedha, suala la malipo ya awali siyo sharti la kisheria na tunaamini kwamba lisiwe sharti la kisheria. Kwanza tunatatizo kwamba yule anayekwenda kukopa siyo lazima awe na fedha za kulipa, tunachodai hapa kwamba hajaanza mazungumzo labda alipe asilimia fulani ya gharama

ambayo imetathminiwa kwamba itakuwa ya bei ya kile chombo. Kwa hiyo, kuingiza hili, tayari umekwishaweka kikwazo. Tunadhani kwamba sharti hili likabaki kuwa uamuzi wa kampuni ya karadha husika au benki wakati wa makubaliano na yule mkopaji. Maana yake pamoja na sheria hii msingi mkuu wa hii biashara ni makubaliano kati ya mkopaji na mkopeshwaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, taasisi za karadha, benki zitakuwa na uhuru wa kuweka au wa kutoweka sharti hili la kuwepo kwa malipo ya awali kwa wale ambao watakuwa wateja wao na itatokana na uamuzi wao. Tunazo kampuni zingine, tunaamini kwamba zitaona kwamba hili jambo ni muhimu, waanze moja kwa moja bila kumtaka yule anayetaka kukopa kulipa malipo ya awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilisema kwamba mjasiriamali ambaye hana mtaji atawezaje kuendesha biashara chini ya utaratibu wa karadha ya fedha. Utaratibu wa karadha ya fedha kama ilivyobainishwa katika Muswada una lengo la kuwawezesha wajasiriamali ambao tayari wako katika biashara ili kukuza biashara kwa kuongezewa mtaji. Kwamba kama hujaanza biashara yenyewe unianza sifuri. Kwamba tunasema hebu anza kwanza, kwa mfano, kama unataka kuingia kwenye biashara ya hoteli, unataka sasa ku-*equip* jiko ambalo ni la gharama, basi tunasema hebu jenga jengo lenyewe tulione. Lakini unataka kuwa mvuvi, hujawahi kutumbukia baharini, unataka kukopa mashua ile ambayo ina mota tunasema hapana, unaweza kutapika mle.

Kwa hiyo, unianza kwanza uvuvi halafu ndiyo uingie kwenye hii mikopo. Maana yake tukubaliane hata kama tukisema kwamba riba itakuwa ndogo, itakuwa chini, na hata tukijitahidi vipi ni kwamba bado ile riba itakuwa ni gharama. Kwa hiyo, huna biashara ambayo tayari iko jirani na kuanza kuzalisha uwezekano wa kutoweza kurejesha amakulipa zile kodi ambazo zinahusika katika mahusiano haya ni mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu vilevile unamlenga mjasiriamali ambaye tayari anafanya biashara lakini anahitaji mtaji wa kutosha ili kukuza ile biashara yake. Kwa hiyo, wajasiriamali ambao bado hawajaanza biashara na wanahitaji mitaji ya kuanzisha biashara, tunazo taratibu zingine ambazo wanaweza kuzitumia kwa ajili ya kupata mitaji. Ni pamoja na mikopo chini ya mpango wa Serikali ambao sasa hivi ni mpango wa kukuza uchumi na kuwawezesha wananchi na kukuza ajira lakini vilevile kuna mikopo ambayo inatolewa na vyombo vya fedha, asasi za fedha. Kwa mfano, *Pride* na *Saccos* hizi ambazo wananchi tunawaomba wajiunge nazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya sita gharama ya kurudisha rasilimali hasa kutoka kwa mkodishaji kwenda kwa taasisi ya karadha au benki baada ya muda wa ukodishaji kumalizika ni za nani? Endapo mkodishaji rasilimali hataweza kununua rasilimali aliyokodishiwa baada ya mkataba kumalizika, gharama za kurudisha rasilimali hiyo kwa mkodishaji itakuwa ni makubaliano baada ya mkodishaji na mkodishwaji kupitia mkataba wa karadha. Suala hili tunadhani si vyema, tunaamini si vyema likabainishwa ndani ya Sheria kwa kuwa makubaliano haya yatatofautiana kulingana na aina ya rasilimali ambayo inahusika katika mpango huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema pamoja na hii Sheria kuna mkataba ambao ni lazima uwepo kati ya yule anayekopa na yule anayekopesha, na tunao mkataba mwingine ambao haumhusu huyu anayekopa lakini ni kati ya yule anayekopesha na yule ambaye anauza kifaa chenyewe. Na tunachosema ni kwamba kwenye kuingia kwenye huu mkataba kwanza kuna umuhimu wa umakini, wa kufuata kifungu, kuelewa kifungu hadi kifungu kinasema nini, kina maana gani, na ndiyo sababu hata hapa tunasema Sheria isiweke kifungu kinachomtambua atakayelipa gharama hizi za kurudisha hiki chombo kwa yule mkodishajiendapo kitahitajika kurudishwa, badala yake itokanayo na makubaliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili ni kama linafanana na kwamba mwisho wa yote chombo kinakuwa ni cha nani, na naomba niseme hapa kwamba mawazo ya baadhi ya Waheshimiwa Wabunge ilikuwa kwamba ingekuwa vyema kwamba hiki chombo kitakuwa kwa yule mkodishaji. Lakini siyo lazima iwe hivyo kwa sababu siyo lazima mkataba wenyewe ufikie tamati ya gharama za ununuzi wa kile chombo ambazo atakuwa ameingia yule mkopeshaji. Kwamba mkataba unaoingiwa kati ya mkopeshaji na mkopeshwaji ni wa muda maalumu chini ya makubaliano ya ule mkataba. Baada ya muda ule kwisha basi mkataba ule uainishe kitakachotokea kwamba bado muda wa mkataba unaweza kuwa ni miaka mitano lakini baada ya miaka mitano bado yale malipo ya kodi, maana yake ni mkopo ambao unalipiwa kodi, bado hajamaliza kumrudishia yule mkodishaji gharama zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya saba ilikuwa kwa kuwa Kifungu cha 11, Kifungu kidogo cha (1) cha Muswada kinaeleza kwamba mkodishaji hatawajibika na suala la ubora wa bidhaa, kitakachokodishwa masharti ya bima na dhamana ya muuzaji wa vifaa yahusishwe katika ununuzi ili kuwalinda wakodishwaji endapo itatokea hitilafu kwenye vifaa au bidhaa inayohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unatambua umuhimu wa vifaa vitakavyohusika katika utaratibu wa karadha ya fedha kuwekewa bima ambapo kifungu cha 14, Kifungu kidogo cha (4) cha Muswada kinabainisha kwamba gharama za bima kwa vifaa vya ukodishaji zitalipwa kwa makubaliano baina ya mkodishwaji na mkodishaji. Aidha, utaratibu wa dhamana kwa bidhaa hizi kwa kawaida hutolewa na muuzaji wa kifaa husika kutegemea na aina ya kifaa ambapo muuzaji hutoa dhamana (*warrant*) kwa mnunuzi kwa kipindi maalumu ili kumlinda endapo itatokea hitilafu katika kipindi kilichowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyongeza hapo kwamba vilevile katika mauzo ya bidhaa, kuna Sheria ambayo inaainisha kwamba unapouza bidhaa fulani ama kifaa fulani, ni lazima kiweze kufanya kazi iliyokusudiwa ya kile kifaa ama iliyotengenezewa kwa mfano kama ukienda dukani, unanunua gari ni jipya inategemewa kwamba halitakufa baada ya kilomita 50. Huu msimamo ni wa siku nyingi katika Sheria za Manunuzi na uuzaji wa bidhaa ambao unatokana na chupa ya maji ya moto.

Kule Ulaya sheria hizi zilikotoka bwana mmoja akanunua chupa ya maji, ni ya mpira, kajaza maji ya moto, maana yake ni baridi kule, kaingiza chini ya blanketi, karibu na miguu, ikapasuka, akapata madhara. Akaenda Mahakamani, na Mahakama ilichoamua ni kwamba ile chupa ilitengemewa kwamba kwa sababu ilitengenezwa ili ikijazwa moto itumike bila kupasuka na kutoa madhara, basi yule ambaye aliathirika alikuwa na kesi na kwa hiyo akalipwa, na vivyo hivyo katika hili. Lakini zaidi ya hayo, sheria yetu inalazimu kwamba yule ambaye anauza ni lazima awe na hakika kwamba anachouza kitakwenda kufanya anayodai kwamba kile kifaa kitakwenda kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa mkodishaji wa kifaa kutowajibika kwa mkodishwaji itakapotokea uharibifu kwenye rasilimali iliyokodishwa. Hapa ni kama nilivyoeleza asubuhi wakati nawasilisha maelezo ya Muswada. Utaratibu wa karadha ya fedha unatoa nafasi kwa mkodishaji kuchagua mwenyewe aina ya rasilimali anayohitaji na kuanza kuitumia kana kwamba ni mali yake na bila ya kusumbuliwa na yule ambaye anamkodishia. Kutokana na haya kwamba yeye amekodisha chombo ambacho kachagua, anaamini kwamba ndicho kinachomfaa na yule ambaye anamkodishia kwa maana ya kumlipa yule aliyetengeneza ama aliye na chombo ambacho hakushiriki katika kukichagua basi sheria inasema si sahihi kwamba huyu ambaye amechagua chombo mwenyewe anaamini kinamfaa basi pale ambapo inatokea kwamba hakifai basi yule ambaye amemkodishia awe ndiye anayewajibika. Kwa hiyo, ni dhahiri kuwa kumwajibishamkodishaji endapo uharibifu wa kifaa utatokea wakati wa kipindi cha ukodishwaji si haki kwa kuwa mamlaka ya kumiliki ile *possession* na kutumia kifaa cha ukodishwaji yatakuwa chini ya mkodishwaji. Sheria inamtaka mkodishaji akitumie hiki kifaa kwa uangalifu na kwamba ingawaje kitazeeka na thamani yake itashuka lakini iwe inashuka kwa matumizi lakini sio kwa kutokana na hali nyingine ambayo sio matumizi yake halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada unatambua pia uwajibikaji kwa upande wa mkodishaji rasilimali ambapo kifungu cha 11(7) kinabainisha kwamba kwa uharibifu wowote wa kifaa utakaosababishwa na mkodishaji, mkodishaji atawajibika kumlipa mkodishwaji gharama zinazotokana na vitendo vya makusudi vya mkodishaji vilivyosababisha uharibifu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni kwa nini kifungu cha 12(1) kinampa mamlaka muuzaji wa rasilimali kuweka majukumu kwa mkodishwaji kuhakikisha ubora wa kifaa wakati mkataba wa ununuzi wa kifaa haumhusishi mkodishwaji. Kifungu cha 12(1) cha muswada, kinatambua kwamba mkataba wa ununuzi unahusisha mkodishaji na muuzaji tu na hivyo kwa upande mwingine mkodishwaji ambaye ndiye mtumiaji wa kifaa husika hatakuwa na haki ya kumdai muuzaji endapo itatokea hitilafu katika kifaa hicho. Ili kuweza kumlinda mkodishwaji ambaye sio sehemu ya mkataba wa ununuzi, kifungu cha 12(1) kinaweka sharti kwamba muuzaji wa kifaa atawajibika kwa mkodishwaji kuhusu ubora na uimara wa kifaa husika sawa na ambavyo atawajibika kwa mkodishaji kwa mujibu wa mkataba wa manunuzi. Na ni yale Waheshimiwa Wabunge niliyosema kwamba yule ambaye atakuwa ametengeneza hiki kifaa kamuuzia yule mkodishaji na yule mkodishaji kamkodishia mkodishwaji, basi ni jukumu lake kuhakikisha kwamba kile kifaa kinafaa kwa kazi ambayo kimekusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, na hoja namba 10, ndefu kidogo, inasema kwamba kwa kuwa kifungu cha 12(3) kinaelekeza kwamba mkodishwaji rasilimali ana uwezokisheria kumchukulia hatua muuzaji wa rasilimali endapo kutakuwa na hitilafu katika rasilimali husika. Kwa kuwa kifungu cha 12(4) kinaeleza kwamba mkodishaji anatakiwa tu kumsaidia mkodishwaji kudai haki zake kwa muuzaji, kwa hiyo basi ni dhahiri mkodishwaji hana mamlaka kisheria kuchukua hatua zozote za kisheria kwa muuzaji wa rasilimali kwa kuzingatia kwamba mkataba wa manunuzi ni kati ya muuzaji rasilimali na mkodishaji rasilimali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu hiki cha 12(3) kinaelekeza kwamba mkodishaji rasilimali ana uwezo wa kumchukulia hatua za kisheria moja kwa moja muuzaji rasilimali kuhusu hitilafu zitakazotokea katika rasilimali aliyokodishwa, ingawa mkataba wa manunuzi haumhusishi mkodishwaji rasilimali. Aidha, kifungu hiki kinabainisha kwamba endapo hitilafu itatokea katika kifaa husika, muuzaji rasilimali atawajibika aidha kwa mkodishaji rasilimali au mkodishwaji rasilimali na sio kwa pande zote mbili kwa wakati mmoja. Lakini sheria vilevile inabainisha kwamba ule mkataba wa kuuza kifaa husika ambao unampa mnunuzi yule ambaye baadaye ndio anakuwa mkopeshaji. Zile haki zake na zenyewe zinatiririka mpaka kwa mkodishaji. La pili, huyu mkodishaji analazimika kumsaidia huyu mkopaji kudai haki zake kwa huyu muuzaji. Na kama tutatazama kwenye ile sheria tutaona kwamba katika kile kifungu hakisemi *may* kinasema *shall*. Kwa hiyo, hakuna hiyari hapa ni lazima amsaidie huyu mkopaji apate haki zake chini ya mkataba huu wa manunuzi ingawaje mkopaji sio sehemu kimaandishi ya ule mkataba wa uuzaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya mwisho ni kuhusu tafsiri ya kifungu cha 11(2) ambayo inahitaji kutolewa ufafanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu hiki cha 11(2) kinakusudia kumlinda mkopaji (*lessee*) dhidi ya vipengele ambavyo vinaweza kuwekwa kwenye mkataba kulinda maslahi ya mkopeshaji (*lessor*) pale ambapo kunaweza kujitokeza matatizo katika umiliki wa rasilimali inayohusika kwenye mkataba wa karadha.

Baada ya kuondoka hapa Mheshimiwa mmoja alisema kwamba mkataba huu, sheria hii inamwonea sana mkopaji ambaye ni mdogo na inamlinda sana yule ambaye anakopesha ambaye atakuwa mara nyingi ni benki, au taasisi ya kibenki ama taasisi ambayo imeanzishwa kwa madhumuni maalumu. Lakini hiyo si kweli, moja ya matumizi makuu au linalojitokeza katika sheria hii ni kwamba wote watatu hawa, yule mkopaji, mkopeshaji na mwenye vifaa yule muuzaji, wote chini ya hivi vifungu vya sheria 11, 12 na 13 wana haki na wana majukumu vilevile ambayo yanahakikisha kwamba hakuna mmoja wao ambaye atamwonea mwingine au atadhulumiwa. Isipokuwa angalizo ni kwamba kwa kuwa baada ya yote kutakuwa na hii mikataba miwili, mmoja wa huu mkopo wenyewe na mwingine ule wa ununuzi wa vifaa basi ni lazima tuwe waangalifu katika kuingia na kusaini mikataba hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kifungu cha 11(2) kinaweka bayana kwamba mkopesaji (*lessor*) hataweza kutumia vipengele katika mkataba wa karadha kutotimiza wajibu wake kuhakikisha kwamba umiliki wa rasilimali inayohusika katika mkataba wa karadha hauna matatizo. Mkodishaji anawajibika kuhakikisha kwamba anapata umiliki kamili wa rasilimali inayohusika ili kuwezesha kubadili umiliki kutoka kwake (*lessor*) kwa mujibu wa mkataba wa karadha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Waheshimiwa Wabunge, karibu wote ambao wamechangia ama kwa maandishi au kwa kuzungumza, walizungumzia umuhimu wa kufikisha elimu ya muswada huu kwa wananchi.

Lengo naamini ili wananchi baada ya kuuelewa waweze basi kutumia kwa ajili ya kujipatia mikopo ya vifaa ambavyo tunaamini wanahitaji zaidi kuliko mikopo ya fedha. Na asubuhi tulisema kwamba tegemeo letu ni kwamba pale watakapokopa basi itakuwa ni fursa nyingine pamoja na zingine ambazo tayari Serikali imekwishaziweka bayana za kumwezesha huyu mwananchi kutumia hivi vifaa kwa ajili ya kuongeza kipato chake kwa ajili ya kuboresha maishayake. Lakini vilevile katika kuchangia kukua kwa uchumi pamoja na pato la taifa. Hilo ndilo tegemeo letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba nirudie tena kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge sana, kwanza, kwa kushiriki kwenye ile semina iliyohusu karadha hii ya fedha lakini vilevile kwa kushiriki katika kuwasilisha kwetu leo asubuhi na sasa hivi, na naomba muda utakapowadia wapitishie huu muswada ili baadaye Mheshimiwa Rais, akiusaini basi uwe sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Muswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa Mara ya Pili)

(Hapa Mwenyekiti (Mhe. Anne Makinda) Alikalia Kiti)

KAMATI YA BUNGE ZIMA

Muswada wa Sheria ya Mikopo ya Ukodishaji Rasilimali wa Mwaka 2007 (*The Financial Leasing Bill, 2007*)

Ibara ya 1

Ibara ya 2

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)

Ibara ya 3

MWENYEKITI: Ibara ya 3 Mheshimiwa Naibu Waziri mlizungumza kwamba mlikubaliana na mabadiliko ambayo Mheshimiwa alichangia kuhusu *natural resources*!

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI): Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetoa *amendment*, tumeifuta ile sehemu C kwa hiyo, haimo.

MWENYEKITI: Kwa hiyo, siyo mmetoa kwa maandiko? Ndio unatoa sasa?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI): Tumetoa *amendment*, tumetoa awali.

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)

Ibara ya 4

Ibara ya 5

Ibara ya 6

Ibara ya 7

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)

Ibara ya 8

MWENYEKITI: Mheshimiwa Juma Kaboyonga! Watu wamehama sasa siwajui wanakokaa!

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tuko sawa sawa kurasa zinazotajwa. Ukurasa wa saba, *Section* ya 8 ambayo inaanza na *the payment for use or leased*, si ndio? Mimi nina tatizo kwenye ibara hii kwa sababu inasema, nitaisoma kikamilifu, kwamba *computation*, samahani Mwenyekiti, *computation* ya zile *rental* itafanywa ili kuwezesha *recovery* ya *whole or substantial part of the value of the leased equipment*. Sasa kwa nini tusiwe *specific*? Tunalotafuta hapa ni *recovery* ya *whole* sio *substantial*. Ndio maana tunapata tatizo la kwamba mwisho wa siku *equipment* hii ni ya nani. Kama tungekuwa wazi kwamba *rentals* zitakuwa *computed on the basis of full recovery, so that at the end of the day equipment hii ownership* yake inakuwa ni ya mkodishaji. Kwahiyo, ninachoshauri kifanyike hapa ni kurekebisha ili *harmonisation* iwe for the whole and not substantial, tuwe na hoja tu whole, basi so that at the end of the day equipment hii ni mali ya mkodishwaji.

MWENYEKITI: Ekhee! mtoa hoja unaweza kusaidiwa na mtu mwingine yeyote. Nasema na wengine kusudi wawe wamejiandaa.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu hoja ya ndugu yangu Mheshimiwa Juma Kaboyonga kuhusu kifungu cha 8 kama ifuatavyo:-

Kwanza, hakuna shaka yoyote ama kutokubalika umiliki wa hiki chombo ni cha nani. Kufuatana na hii sheria mwenye miliki ya hiki chombo ni mkodishaji na hii iko kwenye kifungu nadhani tukienda mbele kidogo tutayakuta hayo, kwamba ni mali ya mkodishaji. Na ni lazima iwe hivyo kwa sababu huyu mkodishaji ndio anakinunua *outright* kwa yule muuzaji, halafu akishakinunua anakikodisha kwa yule ambaye atakopa ili huyu ambaye anakopa amlipe sasa kidogo kidogo, hilo ni moja. La pili kuhusu *harmonisation* katika kukokotoa *residual* wanaita *residual value*, thamani ya mwisho ya kifaa chochote ambacho ni cha kimitaji haiwezekani ukakokotoa ukafikia sifuri. Ndio sababu kuna dhana ya *residual value*, thamani ya kitakachobakia.

Lakini cha tatu ni kwamba katika hii mikataba ya karadha ya fedha sio lazima ifikie *residual value*, ni mikataba ya wakati. *The controlling factor* ni muda na hiyo imepita kwenye sheria nzima. Kwa hiyo, kutatokea kwamba yule mkopaji hata ule mkataba ambao atakuwa ameingia hautafikisha muda wa maisha wa kile chombo. Na kwa hiyo, atasema hiki chombo basi bwana mimi sikitaki tena manake ana *options* tatu mwisho wa ule mkataba, ama kukubali kukinunua kwa makubaliano kama watakuwa wamekubaliana hivyo awali, lakini la pili kurudisha kile chombo kwa yule ambaye atakuwa amemkodishia au ya tatu ni ku-*renew* ule mkataba.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Spika....!

Mwenyekiti: Mwenyekiti!

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI): Ndiyo ni Mwenyekiti, na maelezo yangu naomba yawe hayo na nimsihi tu ndugu yangu hapa nyuma Mheshimiwa Kaboyonga, tukubaliane kwamba haya ya *technical* tutaendelea nayo baadaye. (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Kuendelea baadaye hapana! Tunatunga sheria sasa. Mheshimiwa Juma, umeridhika nadhani! Kifungu hiki kinaafikiwa?

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 9

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima Bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 10

(Ibara ya 10 ilifutwa)

MWENYEKITI: Kutokana na kufutwa kwa ibara ya 10 hiyo iliyokuwa ya 11 itakuwa ya 10.

Ibara ya 10
Ibara ya 11
Ibara ya 12
Ibara ya 13
Ibara ya 14
Ibara ya 15
Ibara ya 16
Ibara ya 17
Ibara ya 18
Ibara ya 19Ibara ya 20

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 21

MWENYEKITI: Ibara ya 21 au 22? Mheshimiwa Juma Kaboyonga!

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Ni baada ya mabadiliko yaliyofanywa na mimi nimepotea maana yake natumia hii rasimu ya zamani. Kwa hiyo, ni 20 na.... ibara ibara ya....!

MWENYEKITI: Wewe sema ni Ibara gani?

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Tuko *part five*?

MWENYEKITI: Ndiyo.

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Kwa hiyo, *part five* ambayo tulikuwa tunaanza na 22?

MWENYEKITI: Sasa ni 21.

MHE. SIRAJU JUMA KABOYONGA: Sasa ni 21. Kutokana na mkanganyiko huo Mwenyekiti, ni vibaya kurudisha kikao chako nyuma lakini basi tena ndio imekwishapita. Ila moja, sehemu ya pili, kifungu cha 21(2), ndio nataka kuzungumzia hapo. Nataka nianze kwa kushauri kuwa tuiseme *a party* isipokuwa ni *parties*. Na mbele pale *lease agreement may, it should be shall*. Kwa sababu ukishaanzisha masjala ambayo

dhamira yake ni kwamba mikataba hii ikasajiliwe suala lisiwe tena *may*. Hayo ndiyo mapendekezo yangu kwa sasa.

MWENYEKITI: Hebu rudia hii ya *may*, ni kifungu gani?

MHE. SIRAJU JUMA KABOYONGA: Kifungu hicho hicho pale kati kati. Yaani 21(2), Umeipata?

MWENYEKITI: Mheshimiwa mtoa hoja, Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hili tutaafiki. Kwamba ile *may* basi iwe *shall* kwa maana kwamba hakutakuwa na chaguo, *there is no option*, lazima ifanyike.

MWENYEKITI: Na ile ya kwanza *a party* unakubali iondoke halafu iwe *parties*?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI): Hatuna ugomvi na hiyo vilevile Mwenyekiti, kwa sababu ni wote.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 22

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 23

MWENYEKITI: Haijatajwa ibara gani?

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Hapo hiyo ya 23.

MWENYEKITI: Sasa utakuwa na haraka na wewe kusimama, ninapo-pose mimi wewe simama!

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Sawasawa Mwenyekiti. Marekebisho yanafanywa ni kumwondoa Gavana kama sijakosea. Lakini tunazungumzia masuala ambayo vyombo vya fedha kwa maana ya mabenki na taasisi vitahusika.

Kwa nini tusimweke Gavana *to the extent* kwamba mabenki na taasisi za fedha zitahusika? Kwa sababu lazima ahusike kwa namna moja au nyingine, hatuwezi kumwondoa kabisa. Tumweke *with a caveat*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Juma, kifungu cha 22 kutokana na mabadiliko, tulikwishakisema kimepitia, ndicho kinachokuwa na Gavana katika kifungu kidogo (2). 23 hakina Gavana. Unazungumzia kifungu gani?

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Kwa mujibu wa rasimu niliyonayo Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kwenye *Part Six* ambayo inaanza na 23 kwa hiyo, tumefanya marekebisho pale si ndio?

MWENYEKITI: Tunaita 22 sasa.

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Tunaita 22? Kwa hiyo, ni kwamba, kama ni 22 nilikuwa naizungumzia 22(2) ambayo tumekwishapita.

MWENYEKITI: Tumepita na mabadiliko yake yalikuwa kwamba kile kinaondolewa.

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Sawa! Sasa hoja yangu ni kwamba kwa kuwa Gavana ni msimamizi wa shughuli za mabenki na taasisi za fedha na sheria hii ikipita yeye bado ana mamlaka, nadhani wangetafuta namna ya kumu-*accomodate* Gavana *to the extent* kwamba vyombo vya fedha kwa maana ya mabenki na taasisi zitahusika badala ya kukiondoa kabisa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mtoa hoja, tueleze kwa nini mlifikiria mwondoe?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Siraju Kaboyonga kuhusu hiki kifungu kwamba kwa kuwa Gavana anayo mamlaka chini ya sheria ya mabenki na taasisi za fedha za 2006 basi hata kama kuna taasisi ya kifedhsa ambayo itaingia kwenye hii biashara tunaamini Gavana atatumia hii sheria yake.

Sababu ya pili ni kwamba tayari kwenye kifungu kidogo cha (1) tuna Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya fedha ambaye amepewa mamlaka ya kutengeneza kanuni za kuendesha karadha ya fedha. Tunadhani si vyema Mheshimiwa Waziri, na Gavana ambaye tayari ana madaraka kama nilivyosema chini ya sheria nyingine wakawa kwenye kifungu kimoja maana yake kuna hatari ya kugongana kwa kweli.

Hiyo ndio sababu ya msingi. Lakini la tatu ni kwamba katika hii biashara tunaamini kwamba kuna taasisi zingine, kampuni zingine ambazo hazitakuwa za kifedha ambazo zitaingia kwenye karadha ya fedha na zenyewe sio vyombo vya fedha. Kwa hiyo, kutakuwa na mgawanyo wa vyombo ambavyo ni vya kifedha na ambavyo sio vya kifedha. Basi Gavana yeye ashughulike na vile ambavyo ni vya kifedha chini ya sheria yake na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, atengeneze Kanuni (*command regulations*) kwa zile ambazo si za kifedha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Juma?

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Kwa maana hiyo kuanzia kwenye *definition* za yale mambo ambayo yatahusika na sheria hii basi tungekuwa na *definition* ya *banking and financial institution* ili sheria hii isije ikawa iko *out completely hundred percent* bila kuwa na mahusiano na *Banking and Financial Institution*. Kama kwenye *definition* tutaweka *definition* ya *Banking and Financial Institution Act*, na kwa maana hiyo ile *Act* ita-apply huku vilevile, ikifikia hapo hatuna haja ya kumtaja Gavana moja kwa moja.

Vilevile tunaweza tukamtaja kwenye *definition* Gavana ni nani? Lakini *Banking and Financial Institution* iwepo kama *definition* huku mwanzo kwa sababu ita-apply.

MWENYEKITI: Mtoa hoja una maelezo ya ziada? Kama nilivyosema na wengine wanaweza kusaidia.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI): Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya ziada ni yale yale niliyotoa. Nafikiri kwamba Gavana tayari ana sheria yake, ana mamlaka yake na *authority* yake kutokana na sheria yake ya *Banking* na ya mabanki na taasisi za fedha za 2006. Na tayari kuna vyombo, kuna benki za biashara ambazo ziko kwenye biashara hii. Mheshimiwa Gavana tayari anavisimamia.

Kwa hiyo, kwa mawazo yangu hata ukiweka kwenye tafsiri kifungu kile cha 3, ukiweka tafsiri aliyoshauri Mheshimiwa Mbunge, sioni itakuwa na mantiki gani kwa sababu kama nilivyosema tuna jambo ambalo lina sura mbili hapa. Kwanza, ni kwenye sekta ya fedha na lingine ni kwenye! Siyo kwenye sekta, lakini nafikiri basi tukubali, basi tuweke kwenye *definition*. (Kicheko)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwanza kabisa *amendment* inayotoka kwenye *floor* na hasa inakuwa vizuri zaidi kama mtu amechangia, kwa hiyo, wale wanaojibu wanajiandaa. Lakini sasa hapa tukichukua *amendment* anayosema Mheshimiwa Kaboyonga ambayo imekuja kama sasa hivi, inaweza ikatimua kabisa sura nzima ya sheria. Kwa hiyo basi, tunakubaliana na *amendment* ambayo imeletwa iliyotumika kwenye Kamati iliyohusika na wakakubaliana hivyo. Hivyo, sasa tunakubali *amendment* kwamba kifungu hicho kinaondolewa kama ilivyoletwa kwenye *amendment*.

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na mabadiliko yake)

Ibara ya 24
Ibara ya 25
Ibara ya 26

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila ya mabadiliko yoyote)

(Bunge lilirudia)

Muswada wa Sheria ya Mikopo ya Ukodishaji Rasilimali wa Mwaka 2007
(The Financial Leasing Bill, 2007)

(Kusomwa Mara ya Tatu)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Sheria ya mikopo inayotolewa kwa njia ya ukodishaji rasilimali *(The Financial Leasing Bill, 2007)* kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake. Kwa hiyo, naomba kutoa hoja kwamba taarifa hiyo sasa ikubaliwe rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDEOEO YA VIJANA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Muswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, sasa Muswada umefikia hatua zake zote unasubiri tu kuwekwa saina na Mheshimiwa Rais. Ninalo tangazo moja tu kwamba Waheshimiwa Wabunge wa Chumba Namba 227, Jengo la Utawala. Na taarifa imetolewa na Mheshimiwa Mahenge, Katibu wa Kikundi hicho.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema hatuna shughuli nyingine kwa leo, naomba kuahirisha kikao mpaka kesho saa 3 asubuhi.

*(Saa 12:23 Jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa,
Tarehe 11 Aprili, 2008 Saa 3.00 Asubuhi)*